# Nipashe

Jumatano Mei 18, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580949
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

BREAKING NEWS
JACKPOT IMEPATA MSHINDI
TZS 1,255,316,060
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Rais Samia:** Ole wenu ma-DED kukodolea macho fedha za miradi

UKURASA 2




## KLOPP: LIVER HAIWEZI KUMSAJILI MBAPPE

UKURASA 22

# Ni mapinduzi

UKURASA 2

1. MBOLEA ILIYOSHEHENI NAFUU
2. WALIMA KOROSHO NI NEEMA TU
3. MABILIONI KWA VIJANA SHAMBANI
4. UPUNGUFU SUKARI WAPATIWA DAWA
5. OPERESHENI MAFUTA YA KUPIKIA



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakurugenzi watano MSD watumbuliwa

UKURASA 4

# Walimu waliokopa wafuatwa darasani

UKURASA 3

MICHEZO FAINALI UEFA LIVER VS MADRID DARAJANI UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (KFED), Waleed SH. Albahar, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Barabara ya Nyahua-Chaya yenye urefu wa kilomita 85.4, Tura, Uyui, mkoani Tabora jana. **PICHA: IKULU**

# Ni mapinduzi ya kilimo

**Na Romana Mallya**

NI mapinduzi! Ndicho unachoweza kusema kutokana na uamuzi wa serikali wa kuwekeza fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo kwa mwaka ujao wa fedha.

Katika kile kinachoweza kutafsiriwa kama kujibu kilio cha muda mrefu cha wabunge na wadau, kwa mwaka huo wa fedha serikali imepanga kutumia Sh. bilioni 751.123, kushuhudiwa ongezeko katika mafungu yote matatu kutoka Sh. bilioni 294.162 mwaka huu wa fedha, sawa na ongezeko la asilimia 155.34 .

Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, akiwasilisha bungeni jijini hapo jana, makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023, alibainisha wizara inatarajia kukusanya Sh. bilioni 126.118 kutokana na vyanzo mbalimbali.

Alisema sehemu kubwa ya fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha utafiti, kutoa ruzuku za mbegu za alizeti, ngano na miche ya michikichi.

Pia, kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, kuimarisha na kutoa huduma ya upimaji wa afya ya udongo, kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, ukiwamo ujenzi wa mabwawa ya kuvunia maji ya mvua.

Bashe pia alisema wamepanga kuimarisha upatikanaji wa masoko, upatikanaji wa mitaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfuko wa maendeleo ya kilimo utakaowezesha upatikanaji wa pembejeo.

Waziri huyo aliyataja maeneo mengine ni kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maghala, pia kuimarisha kilimo cha mashamba makubwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha maeneo maalum ya mashamba hayo na kutoa ruzuku ya mbolea mwaka 2022/23 pamoja na kuimarisha kilimo cha anga na maendeleo ya ushirika.

Kuhusu mafuta ya kula, waziri huyo alisema mahitaji yake nchini ni tani 650,000 kwa mwaka kulinganishwa na uzalishaji wa ndani ambao ni tani 300,000, hivyo takriban tani 350,000 huagizwa nje.

Alisema kati ya kiasi kinachozalishwa nchini, tani 270,000 sawa na asilimia 90 kinatokana na alizeti na kiasi kinachobaki kinachangiwa na mazao mengine ikiwamo michikichi, karanga, nazi, pamba na ufuta.

Alisema ili kujitosheleza kwa mahitaji ya mafuta ya kula, mkakati wa muda mfupi ni kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa alizeti kwa ziada ya tani 1,400,000 ili kuziba naksi ya tani 400,000 za mafuta ya kula ambapo mahitaji ya zao hilo ili kukidhi mahitaji ya ndani ni tani milioni 2.3 na wamejiwekea lengo kuzalisha tani milioni tatu ifikapo mwaka 2025 ili nchi iwe na tani milioni moja.

Alisema wanahitaji kulima eneo lenye ukubwa wa hekta milioni 2.4 na linahitaji tani 12,000 za mbegu kwa ajili ya uzalishaji wa tani 1,000,000 za alizeti.

"Ili kufikia lengo hili, wizara katika mwaka 2022/23 itachukua hatua mbili za kimkakati, pamoja na majukumu ya kawaida ya uhamasishaji na itazalisha na kugawa tani 5,000 za mbegu bora za alizeti kwa ruzuku na jumla ya Sh. bilioni 11," alisema.

Kwa zao la mkonge, Bashe alisema wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania itasimamia mkakati wa kuongeza uzalishaji kutoka tani 36,169.8 mwaka 2020/21 hadi tani 60,000 mwaka 2022/23 na kahawa kutoka tani 65,235 mwaka 2021/22 hadi tani 72,000 mwaka 2022/23.

Bashe alisema kwa zao la pamba wamepanga kuongeza uzalishaji kutoka tani 144,792 mwaka 2021/22 hadi tani 350,000 mwaka 2022/23 na chai kutoka tani 27,510 mwaka 2021/22 hadi tani 30,000 mwaka 2022/23.

"Tumepanga kuongeza uzalishaji wa tumbaku kutoka tani 58,295 mwaka 2021/22 hadi tani 95,000 mwaka 2022/23," alisema.

Waziri Bashe pia aliziagiza kampuni na viwanda vya mbolea kusajili mawakala wao Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ifikapo Mei 31, mwaka huu.

"Kampuni yoyote ambayo haitatekeleza agizo hili na kukubali kutumia mfumo utakaowekwa na TFRA wa kusimamia na kusajili kampuni, mawakala na kuweka mfumo wa Point of Sale (POS) kwenye maduka na ghala zao za mikoa na wilayani, serikali haitosita kumfutia leseni yake ya biashara," alionya.

Bashe alibainisha kuwa wizara inapitia upya muundo wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) kwa lengo la kuiwezesha kujiendeleza kibiashara na kutumika kama chombo cha serikali cha kuimarisha upatikanaji wa viuatilifu na katika mwaka wa fedha 2022/23, itaiwezeshwa kwa kupatiwa Sh. bilioni sita kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

**VIJANA NA KILIMO**

Waziri huyo alisema wizara inakamilisha mkakati wa Taifa wa kushirikisha vijana kwenye kilimo awamu ya pili (NSYIA II 2022-2027) baada ya ule wa kwanza kumaliza muda wake mwaka 2021.

Alisema katika utekelezaji wa programu hiyo ya 'Building Today for a Better Tomorrow' watazingatia utekelezaji wa masuala ya NSYIA II.

"Wizara kupitia mradi wa TANIPAC kwa kushirikiana na SIDO utatekeleza utengenezaji wa vihenge vya chuma kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa teknolojia hiyo kwenye maeneo ya uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula katika ngazi za kaya na kuongeza ajira na mapato kwa vijana," alisema.

Alibainisha kuwa kwa kutambua matatizo ya vijana, wizara imepanga kuongeza ajira 1,000,000 za vijana kwenye sekta ya kilimo ifikapo 2025 kwa kuanzisha programu yao hiyo ya Build Today for a Better Tomorrow.

Aliyataja mazao ya kipaumbele yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa mradi huo kuwa ni pamoja na alizeti, soya, ngano, sukari na mazao ya bustani ambapo jumla ya Sh. bilioni tatu zimetengwa. Kati yake, Sh. bilioni moja zitatumika kama dhamana ya mikopo kwa vijana.

Waziri Bashe pia aligusia mikakati ya wizara kukabiliana na uhaba wa sukari nchini, akibainisha kuwa wizara kupitia Bodi ya Sukari itaongeza uzalishaji wa sukari nchini kutoka tani 372,210 mwaka 2021/2022 hadi tani 450,000 mwaka 2022/2023.

Vilevile, Bashe alisema wizara inatarajia kutumia Sh. bilioni 150 kutoa ruzuku ya mbolea kwa mazao yote kwa lengo la kuleta unafuu kwa wakulima.

***Soma hotuba ukurasa wa 11-15**

# Samia awaonya wanaotolea macho fedha za halmashauri

**Na Halima Ikunji,** TABORA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaonya wakurugenzi wa halmashauri nchini wasizitolee macho fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wananchi na kwamba watakaothubutu 'kuzidokoa' watakiona cha moto.

Alitoa kauli hiyo jana katika sherehe za ufunguzi wa barabara ya Nyahua-Chaya yenye urefu wa kilometa 85.4 akiwa kwenye ziara yake ya kikazi ya siku tatu mkoani hapo.

Rais Samia alisema fedha zote za miradi zinatakiwa kutumika ipasavyo na kama ilivyoelekezwa na serikali ili wakurugenzi hao waepukane na mkono wa mrefu wa serikali.

Alisema serikali inatambua kilio cha wananchi na ndiyo maana inajitahidi kila hali kuhakikisha inatekeleza na kutatua shida zao.

Aidha, alisema serikali itaendeleza miradi yote iliyoanzishwa pamoja na kutafuta fedha zingine kwa ajili ya kuhakikisha kila kitu kinakamilika.

Alisema amesikia kilio cha wananchi wa Wilaya ya Uyui na ametoa fedha kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait Sh. bilioni 123 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

Katika hatua nyingine

Rais Samia aliwataka wananchi wasing'oe alama za barabarani ambazo zitawasaidia madereva kuona mbele kuna kitu gani ili kuepusha ajali zinazoendelea kutokea sehemu mbalimbali nchini.

Kadhalika walitakiwa kutunza miundombinu ya barabara na kuonya kufanya hivyo kutasababisha ajali kila siku katika barabara hiyo.

Alisisitiza lengo la serikali ni kuhakikisha barabara zote zinajengwa kwa kiwango cha lami katika maeneo yote yaliyobakia na kuiagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuhakikisha wanafanya kazi hiyo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Buriani, akitoa taarifa fupi mbele ya Rais alisema, Wilaya ya Uyui inazalisha asali ambayo inawapatia kipato wakazi wa eneo hilo.

Alisema katika fedha zilizotolewa za Uviko-19 zimetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Mkoa wa Tabora na wilaya zake.

Balozi huyo alimshukuru Rais kwa ujio wake na kutoa fedha kwa ajaili ya ujenzi huo wa barabara yenye urefu wa kilometa 85.4 kutoka Nyahua hadi Chaya.

Alisema katika fedha za UVIKO - 19 zilizotolewa zilitumika katika ujenzi wa vyuo vya ufundi katika Wilaya ya Uyui na Igunga mkoani humo.

Dk. Buriani aliahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kushirikiana na viongozi wenzake ili kuleta maendeleo kwa jamii.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Igalula mkoani Tabora, Venanti Daudi, alimwomba Rais Samia kusaidia ujenzi wa barabara ya kutoka Mpakani mwa Tabora hadi Tura.

Alisema kwamba katika jimbo lake, vijiji 48 havina umeme jambo ambalo linarudisha nyuma shughuli za maendeleo kwa wananchi wake.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, alimweleza Rais Samia kuwa Mfuko wa Barabara utaendelea kuboreshwa kila mwaka ili kuboresha miundombinu ya barabara katika mikoa yote nchini.

# Walimu waliokopa wafuatwa darasani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida taasisi za fedha zinazotoa mikopo zimedaiwa kuwanyang'anya kadi za benki walimu walioshindwa kulipa madeni na wakati mwingine kufuatwa madarasani kudaiwa katika Manispaa ya Shinyanga mkoani Shinyanga.

Baadhi ya taasisi hizo zimekuwa zikiwafuata walimu katika sehemu zao za kazi kuwadai madeni mbele ya wanafunzi bila kufuata au kuheshimu mikataba waliyoingia wakati wanakopeshana.

Hatua hiyo imetajwa kuwa sehemu ya vikwazo vinavyorudisha nyuma maendeleo ya elimu katika manispaa hiyo kwa kuwa walimu wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu wakihofia kuvunjiwa heshima mbele ya wanafunzi wao, kufungiwa ndani na kupokwa kadi zao za benki.

Mwenyekiti wa Chama cha Walimu (CWT) katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Meshack Mashigala alibainisha hayo juzi mkoani Shinyanga.

Alisema kila mwaka kumekuwa na matukio ya baadhi ya walimu kukamatwa na wakopeshaji wa mikopo aliyoiita 'umiza' na kufungiwa ndani katika ofisi zao wanaposhindwa kulipa mikopo kwa wakati, akisisitiza kuwa jambo hilo lisipotatuliwa wanafunzi wataendelea kukosa masomo na kushindwa kumaliza mihula.

"Walimu wangu wanapokopa tu riba inakuwa asilimia 20, wanakabidhi kadi za benki na kutoa namba za siri za benki wakati wa marejesho wanakuta riba imepanda hadi asilimia 100, hali ambayo hawezi kulipa na anaanza kuishi kama ndege na shuleni anashindwa kuhudhuria vipindi alivyopangiwa kufundisha," alisema Mashigala

Aliwataka wakopeshaji wa mikopo hiyo kuacha kujichukulia sheria mkononi kwa kuwakamata na kuwafungia katika ofisi za walimu badala yake wakawafungulie mashtaka kisheria na siyo kuwadhalilisha mbele ya wanafunzi na jamii inayowazunguka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, alithibitisha kutokea kwa matukio hayo na kubainisha kuwa walimu hao wamekuwa wakifika polisi kuomba barua ili waende benki kuomba kadi nyingine kwa madai kadi ya mwanzo imepotea.

Alisema kumekuwa na matukio mengi ya aina hiyo, hivyo kuwapo ishara ya udanganyifu, shida kuu ikibainika kuwa ni mbinu ya walimu kuzikwepa taasisi au watu waliowakopesha fedha kwa riba kubwa.

"Ukopeshaji wa mitaani siku zote unazaa shilingi kwa shilingi na wanapokopa hukabidhi kadi zao za benki na namba za siri na mwisho wa mwezi aliyemkopesha ndiye anakwenda benki kuchukua kiasi alichomkopesha, jambo ambalo ni kinyume cha sheria mtu kutumia akaunti ambayo siyo yake," alionya.

Kamanda Kyando aliwataka walimu wanapohitaji mikopo kwenda kukopa katika taasisi za kifedha zinazotambulika na serikali ambazo watakopa na kukuachiwa kiwango kinachotakiwa kisheria.

Kwa mujibu wa mwongozo wa utumishi, kiwango cha makato katika mshahara wa mtumishi hakipaswi kuwa chini ya theluthi ya mshahara wake wote.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Sophia Mjema, alisema walimu hao wanakosea kuingia katika mikopo hiyo huku wakijua inawaumiza.

Alisema kitu kibaya zaidi wanasamilisha kadi zao za benki pamoja na namba za siri na kumtaka Kamanda wa Polisi kuangalia namna ya kulitatua jambo hilo.

# Spika aelekeza magari ya viongozi kubana mafuta

**Na Romana Mallya**

SPIKA wa Bunge, Tulia Ackson, amesema katika kupunguza matumizi ya fedha, magari ya viongozi ambao hawapo kwenye itifaki ya vyombo vyao kuendelea kunguruma wakiwa wameshuka, yazimwe kwa sababu matumizi kwenye mafuta ni makubwa.

Aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma na kueleza kuwa magari ya viongozi ikiwa ni pamoja na ya mawaziri na manaibu waziri yanaendelea kuunguruma nje ya Bunge wakati wao wakiwa bungeni.

"Waheshimiwa wabunge mjue hili na upande wa serikali ninatamani tuone magari ya viongozi yakishashusha kiongozi siyo hapa bungeni tu nchi nzima dereva akishamshusha awe ni Mwenyekiti wa halmashauri, meya, Katibu Mkuu au kiongozi yoyote, ukiacha wale viongozi ambao kwa itifaki yao inabidi magari yaendelee kuwaka, mengine yote inabidi yazimwe na dereva ashuke kwenye gari.

"Ashuke kwa sababu matumizi ya



fedha kwenye eneo la mafuta yanakuwa makubwa sana kwa sababu ya magari kuendelea kuwaka wakati kiongozi hayupo kwenye gari, yupo kwenye mkutano wa saa mbili huku gari likiendelea kuwaka.

Kutokana na hilo, Spika Ackson aliomba hilo litazamwe.

"Hili mlitazame na Mheshimiwa Waziri Mkuu uko hapa tunatamani tuone mabadiliko kwenye hili eneo ili matumizi ya serikali yapungue kwenye eneo la mafuta," alisema.


## JOB VACANCIES ANNOUNCEMENT

### PHARMACEUTICALS AND MEDICAL DEVICES SALES REPRESENTATIVES

We are a Pharmaceutical, and Medical Devices Company. We import and distribute Pharmaceuticals and Medical Devices from Europe, Asia and other parts of the global.

We are looking for the qualified, motivated, people-oriented candidates to fill the job vacancies listed below in our company. The Pharmaceuticals and Medical Devices Sales Representative will be responsible for sales, promotion and marketing of our products. We also looking for a Biomedical Technician who will do the Repairs, services and installations of Medical Equipment.

**Job Title**

1. **Pharmaceutical Sales Representatives**

| Work Place | Number of Post |
|---|---|
| Arusha | 2 Posts |
| Dodoma | 2 Posts |
| Mwanza | 2Posts |
| Morogoro | 1post |
| Mbeya | 2 Posts |
| Zanzibar | 1 Post |
| Moshi | 1 Post |
| Dar es Salaam | 5 Post |

2. **Medical Devices Sales Representatives**

| Work Place | Number of Post |
|---|---|
| Dar es Salaam | 1 post |

3. **Biomedical Technician/Engineer**

| Work Place | Number of Post |
|---|---|
| Dar es Salaam | 1 Post |

**Key Requirement and Qualifications**

1. Diploma or Degree in the relevant field
2. Relevant Job Experience of more than two years.
3. The applicants must be willing to travel with little notice and havea good working knowledge of Tanzania regions.
4. Applicant should have good English and Kiswahili communication skills that will enable them to:

(i) Work on development and implementation of key marketing programs.
(ii) Provide Market updates, expense reporting and other required business reporting
(iii) Develop customer relationships and maintain a high level of customer satisfaction.
(iv) Proactively prospect for new customers and new opportunities.
(v) Solve a broad range of problems of varying scope and complexity.
(vi) Provide prompt response to all customer requests.
(vii) Applicant should have record of accomplishment of achieving sales targets around quota and sales forecastsand proactively drive the salescycle and forecastsales.
(viii) Applicant should have excellent computer skills to be able to make reports and presentations.
(ix) Applicant should be able to demonstrate

**Core Values of:** Innovation, Trust, Respect, Teamwork, Uncompromising Integrity, Speed, Focus and Accountability

**Mode of Application:**

**To apply, kindly submit your application with a detailed CV, photocopies of academic and other relevant certificates and names of three referees with their contacts to The Advertiser, P.O BOX 40385, DAR ES SALAAM, within two weeks form the date of this advertisement.**

**Please indicate your preferred work Station**

**Only short listed candidates with proven requirements and experience will be contacted.**

# Serikali yawatumbua wakurugenzi 5 MSD

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema wizara yake imeanza kuyafanyia kazi maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu Bohari ya Dawa (MSD) na kwamba wakurugenzi watano wa hapo wanawaondoa.

Aliyasema hayo juzi jioni bungeni alipokuwa anahitimisha hoja ya makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2022/23 ambayo ilipitishwa na wabunge wote kwa kura ya ndiyo.

Alisema wakurugenzi wanaoondoka ni Mkurugenzi wa Fedha, Mkurugenzi wa Manunuzi, Mkurugenzi wa Vifaa, Mkurugenzi wa Sheria na Mkurugenzi wa Utawala.

Alisema ameshaielekeza MSD kwamba watawapima kwa upatikanaji wa dawa za miezi minne na siyo mwezi mmoja.

Waziri Ummy alisema wamewaeleza kuwa wanataka dawa zote 290 pamoja na vifaa tiba vipatikane.

"Katika hili tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa maagizo yake tumeshaanza kuyafanyia kazi sambamba na Mheshimiwa Rais kubadilisha uongozi, Mtendaji Mkuu MSD pamoja na kumteua Mwenyekiti wa Bodi, tunawaondoa wakurugenzi watano wa MSD.

Waziri Ummy alisema wameshauriwa pia kuangalia mifumo ya usambazaji wa dawa ndani ya MSD na kwamba wataendelea kuitaka inunue dawa na vifaa tiba kutoka viwandani kwa kuzingatia mikataba ya muda mrefu.

"Ninaomba niseme jambo moja, nimepewa dhamana ya kusimamia sekta ya afya hatutakuwa na upendeleo wa ubora wa dawa na vifaa tiba kwa sababu tusiende kuwapa matatizo Watanzania kwa kutoangalia ubora," alisema.

Waziri huyo alimpa pole Mkurugenzi mpya wa MSD ambaye amepewa hongera kwa kumweleza kuwa ana kazi kubwa kwa sababu matumaini ya Rais na wabunge pamoja na yeye ni makubwa.

"Mheshimiwa Spika, tuseme (Mkurugenzi Mkuu) alikuwa ndiye mshauri wa serikali kuhusu masuala mazima ya dawa akiwa upande wa Ubalozi wa Marekani, Mwenyekiti wa bodi alikuwa mshauri wa serikali kwa upande wa Global Fund ambao ndiyo wanatupa dawa za Ukimwi, Kifua Kikuu (TB) na malaria.

"Juzi nilikuwa ninamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sawa nyie si mnatukosoa, mnashauri haya sasa nendeni mkafanye hayo ambayo mlikuwa mnaeleza."

Waziri Ummy alisema Mkurugenzi Mkuu MSD wamemwambia ndani ya miezi mitatu dawa zifike katika vituo na hospitali.

Kuhusu matumizi ya dawa katika ngazi ya hospitali alisema MSD inaweza kuzipeleka lakini anahoji madaktari na wataalamu waliopo huko wanazingatia miongozo ya matibabu ya taifa.

"Kwa sababu zipo taarifa tumezipata dawa ambazo zipo katika hospitali zilizoagizwa na mfamasia, daktari anaandika za kwake mwenyewe ambazo ni kinyume, hili tutalisimamia kwa kiasi kikubwa," alisema.

Aliwataka wabunge wasaidie jambo hilo wanapokaa kwenye mabaraza ya madiwani wahoji kamati za afya za kusimamia vituo kama zinafanya kazi na kufuatiliwa upatikanaji wa dawa.

Waziri huyo alisema mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) itawasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha mnyororo mzima wa dawa.

Pia alisema kamati imetoa maoni kuhusu matumizi holela ya dawa ambayo ameahidi wataendelea kuyafanyia kazi.

Kadhalika alitaja eneo la mwisho katika dawa kuwa watafufua na kuimarisha uzalishaji wa dawa kwa kuvifufua viwanda ambavyo vilikufa.

**BIMA YA AFYA**

Waziri Ummy alisema wataendelea kutoa elimu kuhamasisha umuhimu wa kuwa na bima ya afya ili wapate matibabu.

"Tutakamilisha haraka muswada wa sheria. Kwa upande wa huduma za kinga Mheshimiwa (Erick) Shigongo amesema vizuri pamoja na Dk. Pauline Nahato na Cecilia Pareso ni kweli ukiangalia hii bajeti imezungumzia tu tiba tunatakiwa kujieleza kwenye kuzuia, ndiyo maana ukiniuliza nichague kipaumbelechanguchakwanzasinafedhanitafanya chanjo za watoto hii ni moja ya kuwakinga.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati), akiagana na Mkurugenzi wa Shirika la Vijana TAYOA, Peter Masika, aliyemtembelea ofisini kwake, jijini Dodoma juzi, baada ya kuwasilishwa kwa bajeti ya Wizara ya Afya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi wa TMDA huru kesi ya bil. 58/-

**Na Grace Gurisha**

WATUMISHI watano wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) wameachiwa huru na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya Mkurugenzi wa Mashitaka nchini (DPP) kuwasilisha nia ya kutokuendelea na kesi dhidi yao.

Watumishi hao ni Charys Ugullum, Raymond Wigenge, Ezekiel Mubito, Adelard Mtenga na Abdallah Juma,ambao walikuwa wakikabiliwa na mashtaka ya kuisababishia mamlaka hiyo hasara ya Sh. bilioni 58.3 kwa kujilipa posho.

Wakili wa Serikali kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Hassan Dunia alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ritha Tarimo kuwa kesi hiyo ilikuja kwa ajili ya kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka.

"Lakini DPP amewasilisha maombi ya kutokuwa na nia ya kuendelea na mashtaka dhidi yao chini ya kifungu cha 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai," alidai Dunia

Kufuatia taarifa hiyo Hakimu Tarimo alikubaliana na ombi la upande wa mashtaka kwa kufuta kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 5 ya 2018 na kuwaachia huru washitakiwa hao.

Katika kesi ya msingi inadaiwa kati ya Mei na Desemba, 2016 katika Ofisi za Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA wakati huo) kwa sasa TMDA washtakiwa waliisababishia mamlaka hiyo hasara ya Sh. 58,390,000.

Ilidaiwa fedha zilikuwa ni posho za wafanyakazi waliokuwa wamesaini malipo yao jambo lililosababisha kujilipa mara mbili. Katika kesi hiyo, shahidi mmoja pekee ndiye aliyekuwa ametoa ushahidi wake.

# Wabunge wasikitishwa uchakavu wa nyumba NHC

**Na Romana Mallya**

WABUNGE wameonyesha kusikitishwa na nyumba zinazomilikiwa na Shirika la Nyumba Nchini (NHC) katika miji ambazo wamesema nyingi zimechakaa.

Katika semina ya wabunge iliyofanyika juzi iliyoandaliwa na NHC, wabunge hao walisema uchakavu huo umesababisha kutopendeza kwa maeneo hayo.

Mbunge wa Chakechake (CCM), Ramadhan Suleiman Ramadhan alisema nyumba nyingi zilizojengwa katika miji hazifanyiwi maboresho na hivyo hazifai tena katika miji.

"Matajiri nikiwamo ninaweza kujenga nyie mkapata faida na mimi nikapata faida,"alisema.

Mbunge wa Geita Mjini (CCM) Constatine Kanyasu alisema gharama kubwa za kujenga zinasababisha bei ya kupangisha nyumba za shirika hilo kuwa kubwa na kusababisha baadhi kuhama.

"Baadhi ya wapangaji tumehama Medelii kwa sababu bei ya kupangisha ni kubwa ukilinganisha na huko uraiani,"alibainisha.

Akieleza suala la uchakavu wa nyumba hizo kwenye miji, Mkurugenzi Mtendaji wa NHC, Nehemia Mchechu alisema kwa kufuata utaratibu itawachukua muda mrefu kukarabati ndiyo maana wameamua kwenda katika utaratibu wa ushirikiano kati ya sekta binafsi na umma (PPP).

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Allan Kijazi, alisema jambo la msingi ni kupata miongozo kwa mji wa Dodoma hasa kwa kuzingati una matetemeko ya ardhi.

Alisema ujenzi hufanyika kama ardhi inafaa kwa ujenzi.

"Kuna wakati mji wa Serikali (Mtumba) ilitokea matetemeko mawili, matatu lakini kuna baadhi ya majengo ya ofisi tayari yameshaathirika na matetemeko haya, baada ya uchunguzi kufanyika na kuonyesha kuwa kuna baadhi ya maeneo hayafai kwa ujenzi, ilibainishwa kuwa maeneo ambayo yana matatizo na hivyo yasiwe yanajengwa majengo yoyote," alisema.

Alisema kabla ya ujenzi serikali imekuwa ikizingatia kuchunguza eneo husika.

Akizungumzia miongozo ya ujenzi, Dk Kijaji alisema wako katika hatua za mwisho za kuandaa sera za nyumba na zikikamilika kutakuwa na miongozo kamili ya ujenzi.

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula alisema wakitaka kujenga nyumba yoyote katika halmashauri wamekuwa wakiangalia takwa (taste) ya mteja na ukubwa wa nyumba anayohitaji.

Kuhusu kuingia makubaliano na halmashauri ili waweze kununua majengo, Dk. Mabula alisema kuna halmashauri ziliingia makubaliano na NHC lakini mwisho wa siku waliingia katika mvutano wa kuchukua ama wasichukue nyumba hizo.

HABARI KITAIFA

# Mfanyabiashara mahakamani tuhuma kujipatia bilioni 13/- kwa udanganyifu

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Anthony Magoe (35), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na mashtaka matano yakiwamo kujipatia Sh. bilioni 1.3 kwa njia ya udanganyifu kwa madai ya kuonyesha sampuli ya madini.

Akisoma hati ya mashtaka juzi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Isaya kuwa mshtakiwa ana tuhuma mbalimbali zikiwamo za kughushi kibali kwa madai kimetolewa na Wizara ya Madini.

Alidai katika shtaka la kwanza, inadaiwa mshtakiwa alitenda kosa hilo kati ya Januari 18 na Februari 16 mwaka 2022 maeneo ya Jiji la Dar es Salaam, akijipatia Dola za Marekani 602,747 sawa na Sh. bilioni 1.3 kutoka Kampuni ya Macbrusa Pyt kupitia akaunti iliyoko benki ya CRDB huku akijifanya kuwa fedha hizo ni kwa ajili ya kuonyesha sampuli za madini.

Mwanga alidai kuwa katika shtaka la pili, mshtakiwa anadaiwa Februari 9, 2022, alighushi kibali cha kusafirisha madini kwa sampuli yenye kumbukumbu namba 11000911 akionyesha kwamba kimetolewa na Wizara ya Madini.

Katika shtaka la tatu, inadaiwa Januari 19, mwaka huu alighushi kibali cha kusafirisha madini kikionyesha kimetolewa na wizara hiyo.

Shtaka la nne, Mwanga alidai kuwa Januari 19, mwaka huu mshtakiwa alighushi kibali cha maombi cha kusafirisha madini kikionyesha kimetolewa na wizara.

> **Mshtakiwa pia anatakiwa kuwasilisha fedha taslimu Sh. milioni 750 au hati ya mali yenye thamani hiyo.**

Alidai katika shtaka la tano, inadaiwa Januari 19, 2022 alighushi risiti yenye kumbukumbu namba 920164000127430 kuonyesha kuwa ni halali na katika shtaka la sita inadaiwa siku hiyo alighushi nyaraka nyingine.

Baada ya kusomewa mashitaka hoyo, Magoe alikana kutenda makosa hayo ambapo upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa shauri hilo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Isaya alisema ili mshtakiwa awe nje kwa dhamana, anatakiwa kuwa na wadhamini wawili waaminifu wenye barua za utambulisho kutoka serikali za mitaa.

Mshtakiwa pia anatakiwa kuwasilisha fedha taslimu Sh. milioni 750 au hati ya mali yenye thamani hiyo.

Mdhamini mmoja kati ya hao alikuwa na hati ya mali isiyohamishika, mahakama iliahirisha kesi hiyo kwa muda kwa ajili ya kupeleka hati hiyo Wizara ya Ardhi ili ikaguliwe.

Ili kupisha ukaguzi huo, mshtakiwa alipelekwa rumande kusubiri masharti yake ya dhamana yakamilike.

# Shahidi akwamisha kesi wafuasi Chadema

**Na Vitus Audax,** MWANZA

Kesi inayowakabili wafuasi 19 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ya kufanya fujo kanisani jijini Mwanza imeendelea kupigwa kalenda baada ya mshtakiwa namba nne kati yao kutofika mahakamani.

Wafuasi hao wanakabiliwa na kesi namba 77 ya mwaka 2021, baada ya kukamatwa Agosti 15, mwaka jana katika Kanisa Katoliki la Kawekamo Jimbo Kuu la Mwanza.

Kutokana na mshtakiwa huyo kutofika mahakamani, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, Bonaventure Lema aliahirisha kesi hiyo hadi Juni 1, mwaka huu.

Hakimu Lema alisema jana ilikuwa siku ya kuanza kupeleka mashahidi wa upande wa Jamhuri baada ya upelelezi wa kesi hiyo kukamilika mwezi uliopita.

Wanachama hao Aprili 13, mwaka huu walisomewa maelezo ya awali ya kesi yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza na kukana, huku upande wa mashtaka ukiahidi kupeleka mashahidi saba wakiwamo viongozi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Kawekamo Jimbo Kuu la Mwanza na vielelezo vinne vya ushahidi.

Kesi hiyo ilifunguliwa Agosti 19, 2021 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mwanza.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na kosa la kufanya ghasia katika mkutano wa dini uliofanyika katika kanisa hilo Agosti 15, mwaka 2021 na kusababisha waumini washindwe kusikiliza neno la Mungu.

Wanachama hao pamoja na viongozi wa mikoa na kanda kwa pamoja walikana mashtaka hayo mnamo Agosti 19 mwaka jana.

Makada hao wa Chadema inadaiwa walifika kanisani hapo kwa ajili ya kumuombea mwenyekiti wao wa taifa, Freeman Mbowe ambaye alikuwa mahabusu kwa kesi ya ugaidi.

Wafuasi hao ambao wapo nje kwa dhamana tangu mwaka jana, jana walifika tena katika mahakama hiyo kwa ajili ya kusikiliza ushahidi wa shauri.

Washtakiwa hao wanatetewa na wakili Erick Muta na kesi yao imepangwa kuendelea Juni 1, mwaka huu kwa ajili ya kusikiliza ushahidi upande wa Jamhuri.


Mzigo Flexi



Faida bila jasho

Wekeza kuanzia **TZS 1,000,000 faidi riba** kila baada ya

- Mwezi
- Miezi 3
- Miezi 6
- Mwaka
- Miaka 3

Ukomo: Miaka 3
Kwa maelezo zaidi
Piga **0800 008 000**
Tembelea tawi lolote kujiunga

*Vigezo na Masharti Kuzingatiwa

CRDB BANK
Tunakusikiliza

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mamilioni ya wamachinga yanahitaji utaratibu mzuri

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan, aliongea na machinga kwa simu na kuahidi kuwa mwaka wa fedha unaoanza Julai mwaka huu, ofisi yake itatoa Sh. milioni 10 kwa kila mkoa kuwezesha shughuli zao.

Rais alimpigia simu moja kwa moja na kuzungumza na wamachinga waliohudhuria mkutano wa mafunzo ya viongozi wa machinga (SHIUMA), huku akiahidi ushirikiano na mazingira mazuri ifikapo mwaka huu wa fedha.

Uamuzi wa Rais kutoa fedha hizo ni jambo zuri kwa kuwa watakwenda kuwa na ofisi zinazokidhi mahitaji ya msingi, tofauti na awali ingewachukua muda kuchangishana ili kupata kiasi hicho au ofisi hiyo.

Huenda kwa kuwa na ofisi kutawafanya watambulike kwa maana ya kuwa na rejista ya wamachinga hao kila mkoa, ambayo itasaidia serikali kujua idadi yao na shughuli zao ili wanapotaka kupeleka huduma za kibenki, uwezeshaji na nyingine iwe rahisi zaidi.

Pia itasaidia kuona kama wanakua kibiashara au wanadidimia au inawezekana kuwasaidia wakue zaidi ili kutoka kuwa machinga hadi wafanyabiashara wa kati na juu, ili sasa watoe ajira kwa wengi na kuchangia uchumi wa nchi.

Hadi sasa machinga hawalipi kodi ya mapato inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), bali ushuru uliowekwa na halmashauri ambao unatofautiana kutoka eneo moja hadi jingine.

Sisi tunaona ni muhimu kuwa na mipango ya kufuatilia kwa karibu fedha hizo, kwa kuwa uzoefu unaonyesha zimewahi kutolewa fedha kwa makundi fulani lakini ziliishia mikononi mwa wachache.

Mathalani, serikali ya awamu ya nne ya Jakaya Kikwete iligawa Sh. bilioni moja kila mkoa, lakini baadaye ilibainika ziliwafikia wachache na nyingi ziliibwa na wachache ambao walifikishwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), huku wengine wakiachiwa kwa kukosekana ushahidi.

Fedha hizo zilenga kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwakopesha, lakini lengo halikufikiwa bali wachache walizitafuna bila huruma kwa wengine.

Kama haitoshi, serikali ikaja na utaratibu wa kila hamashauri kutenga asilimia 10 katika mapato ya kila halmashauri ya mapato yake kwa ajili ya kukopesha wanawake, vijana na wenye ulemavu, lakini wabunge wameeleza namna zilivyopigwa.

Mathalani, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mwaka jana na huu, ilionyesha fedha hizo haziendi kwa wahusika au zilizokwenda hazikurudishwa na sasa kuna madeni makubwa.

Baadhi ya wabunge walisema kuna baadhi ya watumishi wa umma waliamua kukopeshana fedha hizo kwa kivuli cha wananchi, lakini hazikurudishwa jambo ambalo inaonyesha lengo halikufikiwa.

Ndiyo maana tunasema hizi fedha watapewa machinga sawa, lakini ni lazima kuhakikisha zimefika kwenye mikono husika au ikiwezekana wajengewe ofisi na kununuliwa vifaa kwa utaratibu halali na wa wazi usio na urasimu.

Kuzitoa bila mpango maalum zitaishia kuingia kwenye historia kama ilivyokuwa kwenye mabilioni ya JK na makundi maalum ya halmashauri.

Tunatambua fedha hizi zitakaguliwa na CAG kwa kuwa zitatolewa kwenye bajeti ya serikali, hivyo ni lazima kuanza mapema kupunguza mwanya wa kupotea, ili mwakani tusipokee taarifa inayoeleza upigaji.

Pia ni muhimu serikali ikajenga mazingira wezeshi kwa watu kukua kibiashara kuliko kubaki kuwa machinga, kubaki, lakini kuwatambua maana wapo ambao kwa kuwa wako mtaani wanaonekana wadogo lakini bidhaa walizonazo hawana tofauti na aliye na duka maeneo ya Tandika au Tandale Dar es Salaam.

Lazima kuwe na tafsiri ya machinga kwa kadri ya mazingira yetu na kipimo chake, ili kuepusha nchi kukosa kodi kwa kuwa wengi wanakuwa machinga kwa kuwa hakuna kodi.

Ni muhimu serikali ikafungamanisha shughuli za kiuchumi ili mtu afanye kazi na kupata kipato aliko kuliko kila mmoja kuamini maisha mazuri au ukitaka 'kutoboa' lazima uje mjini, ambako wengi huishia kuwa machinga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ustawi, polisi jamii wasaidieni wanafunzi wasisote vituoni

Na Sabato Kasika

**WAZAZI** na walezi wamekuwa na mwitikio mkubwa wa kuwapeleka shuleni watoto wao, ili wapate elimu bila kujali kuwa wanaposoma ni mbali au karibu.

Pamoja na kuitikia wito huo, watoto kusoma mbali na nyumbani ni sawa kuwapa adhabu hasa wanafunzi wengi wa mijini.

Inapotajwa adhabu ni kutokana na wanafunzi wengine kusota vituoni wakiwa na njaa na wakati mwingine wakishindwa hata kwenda vyooni kujisaidia kwasababu vyoo ni vya kulipia na wenyewe hawana pesa zaidi ya nauli na kiasi kidogo cha kununua karanga au andazi walichopewa na wazazi au walezi.

Wanafunzi wengi wanaosoma sekondari za kutwa wanateseka kuamka alfajiri na kurejea nyumbani usiku hata wakati mwingine zaidi ya saa 3:00.

Ni kutokana na kukosa magari ya shule au usafiri wa shule na kutegemea daladala. Tatizo ni kubwa kwa watoto wa madarasa ya chini mfano darasa la kwanza.

Watoto hao wadogo wanasota vituoni wakisubiri magari, lakini hawawezi kugombea usafiri huo na matokeo yake wanabakia vituo muda mrefu bila kuwahi shuleni au kurudi nyumbani.

Hatukatai watoto kusoma shule za mbali lakini, ni vyema sasa serikali ikawa na mpango wa kuwasaidia ikibidi polisi jamii au maofisa wa ustawi wa jamii kwenye kata wakashirikiana kuwasaidia kwa kusimamia watoto ili wapandishwe kwenye mabasi wakati wa kwenda shule na kurudi nyumbani.

Wanafunzi wanafikia vituoni saa 11 alfajili wakisubiri usafiri ambao wanalazimika kuugombea na watu wazima. Wazazi, walezi, serikali na wadau wajiulize hali hii itaendelea mpaka lini?

Mtoto au watoto hao ni wadogo muda huo walitakiwa kulala lakini elimu ni ufunguo wa maisha wanatakuwa kuwa darasani.

Kinachotakiwa kutatua suala hili ni wazazi na walezi pamoja na jamii kuanza kushughulikia changamoto hiyo kwa kushirikiana na serikali za mitaa hasa ofisi za kata ili kupata maofisa ustawi watakaoshirikiana na polisi jamii kuwafikisha shule.

Inatisha kuona mtoto mdogo unakwama kituoni na sasa yanaanza kuwa mazoea katika miji mingi ya Tanzania, ndiyo maana ni wakati wa kuchukua hatua.

Ni wazi akifika shule amechoka hawezi kusoma akirudi nyumba amechoka je si kumuadhibu mtoto huyo?

Ni vyema wazazi na jamii kuangalia kuanzia sasa suala hilo hata kama shule haziko mbali bado watoto wanahitaji usalama kulindwa na kuepushwa na hatari na suala la usafiri salama halikwepeki.

Suala la kuwapa watoto usafiri kuenda pamoja na kuwapatia chakula cha mchana ili wanapotoka shuleni wawe na nguvu na kuwapunguzia uchovu na njaa.

Njaa inasababisha watoto kuchoka na kusinzia zaidi katika magari na muda mwingine kondakta anapata tena kazi ya kuwauliza wanashuka wapi ili wawashushe vinginevyo watapitilizwa.

Kuna wazazi au walezi ambao wanaona kuliko kuwaamsha watoto usiku na kukumbana na changamoto za usafiri wanaona ni vyema kuwapeleka watoto wao vijijini wakaishi na babu na bibi zao vijijini na kusoma shule za mbali.

Hii inasadikiwa itampunguzia mtoto usumbufu hasa wa usafiri ndani ya daladala bila kujua kuwa watoto wanakosa uangalizi na wanaweza kutumbukia kwenye maangamizo hata tabia za kihalifu.

Wazazi na walezi wanatakiwa kuliangalia sana suala la watoto na kuwasaidia kutengeneza na kutegemeza maisha yao.

Wakati huu serikali na Wizara ya Elimu zinapofanya juhudi za kuboresha elimu ni vyema pia wadau washirikishwa kutoa moani yao ya namna ya kuboresha elimu kwenye eneo la usafiri hasa kwa wanafunzi wa mijini.

# Mawakili wamkwamisha Maimu kujitetea kortini

Na Grace Gurisha

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA), Dickson Maimu, ameshindwa kujitetea tena katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili, kutokana na mawakili kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) wanayoendesha kesi hiyo kupewa kazi maalum.

Hayo yalidaiwa jana na Wakili wa Serikali kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Nickson Shayo, na Wakili wa Maimu, Wabeha Kung'e, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Evodia Kyaruzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Shayo alidai kesi ililetwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa upande wa utetezi lakini mawakili kutoka ofisi ya DPP ambao wanashirikiana nao katika kesi hiyo wamepata dharura kufika mahakamani, hivyo wanaomba ahirisho.

Baada ya Shayo kubainisha hayo, Kung'e alibariki ahirisho hilo kwa kudai kuwa alipigiwa simu na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladslaus Komanya na kumweleza kwamba walitaka kuja kuendelea ila wamepewa kazi maalum. "Kwa mazingira haya hatuna pingamizi kwa ombi la upande wa mashitaka la kutaka kesi iahirishwe," alidai Kung'e.

Hakimu Kyaruzi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Mei 31,2022 kwa ajili ya kuanza kusikilizwa utetezi wa washtakiwa.

Maimu alidai atakuwa na mashahidi siyo chini ya 20 na vielezo 10 baada ya upande wa mashtaka kuleta mashahidi 26 na vielelezo 45 na hakimu kujiridhisha kuwa washtakiwa wana kesi ya kujibu.

Mbali na Maimu, washtakiwa wengine ni aliyekuwa Mkurugenzi wa Sheria wa mamlaka hiyo, Sabina Raymond, Meneja wa Biashara, Xavery Kayombo, Aveln Momburi na George Ntalima.

Shahidi wa mwisho katika kesi hiyo, Ofisa wa TAKUKURU, Emmanuel Koroso, alidai kuwa Mkurugenzi wa Sheria wa Mamlaka hiyo, Sabina Raymond alishuhudia utiwaji saini mkataba uliongizia serikali hasara ya Dola za Marekani 551,500.

Akiongozwa na Wakili Komanya, Koroso alidai wakati akifanya mahojiano na Sabina, alimweleza kuwa yeye ndiye alikuwa msimamizi wa masuala yote yanayohusu sheria NIDA ikiwamo kusimamia na kushuhudia utiaji saini wa mikataba mbalimbali.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka mbalimbali ikiwamo kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175.



Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Hussein Katanga (kulia), akizungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja (wa pili kulia), wakati alipotembelea eneo la Bandari kavu Kwala Mkoa wa Pwani. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

## Serikali yatangaza vita wavuvi haramu

**Na Mbaraka Kambona,** MWANZA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali itawekeza nguvu kubwa kukomesha uvuvi haramu katika Ziwa Victoria baada ya hatua kadhaa zilizochukuliwa awali ikiwamo kuwashirikisha wavuvi wa Kanda ya Ziwa kutokuzaa matunda.

Ndaki alitoa kauli hiyo alipokuwa akiongea na wadau wa sekta ya uvuvi katika kikao cha kujadili changamoto wanazokabiliana nazo wanaofanya shughuli zao katika Ziwa Victoria kilichofanyika mkoani Mwanza Mei 16, 2022.

Alisema mwaka jana serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya uvuvi waliandaa mpango shirikishi ambao ulianisha kila mdau na jukumu lake katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria, lakini matokeo yake wadau hao hawakujali na sasa uvuvi haramu umeongezeka maradufu.

"Uvuvi haramu sasa hivi ni mkubwa kwenye ukanda wetu wa Ziwa Victoria na sisi wizara tumepewa jukumu la kusimamia rasilimali hizi, Rais atatushangaa sana kuona wizara iliyopewa dhamana ya kuhakikisha rasilimali hizi zinalindwa, hazilindwi, sasa wakati tunatafuta mbinu endelevu ya kulinda rasilimali hizi, kuanzia sasa kwenda mbele tutatumia nguvu kuzuia uvuvi haramu," alisema.

Kadhalika alisema kuwa serikali haitavumilia watu wachache wenye kutaka kujinufaisha wao binafsi huku akiongeza kuwa watawashughulikia wote wanaojihusisha na uvuvi haramu kuanzia wavuvi, wasambazaji wa nyavu zisizo halali, na watakamata vyombo vyote vitakavyotumika kubebea au kuhifadhi mazao yaliyovuliwa kwa njia ya haramu katika mikoa yote inayozunguka ukanda wa ziwa.

Aidha, Waziri Ndaki aliwaeleza wadau wa uvuvi kuwa serikali imepokea changamoto zao na watazifanyika kazi, lakini nguvu kubwa kwa sasa itawekwa katika kupambana na uvuvi haramu kwa sababu kama rasilimali za uvuvi zikitoweka hizo changamoto nyingine kama za tozo na utafutaji wa masoko hazitakuwa na maana yoyote.

Naye Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia sekta ya uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema kuwa serikali imesikiliza kilio cha wavuvi kuhusu tozo na imezishughulikia kwa kiasi kikubwa na hivi karibuni michakato ikikamilika serikali itatoa maelekezo ambayo anaamini yatakuwa na nafuu kubwa kwa wavuvi.

# Marekani yasaidia mafunzo ya Kiingereza

Na Mwandishi Wetu

UBALOZI wa Marekani nchini, umeendelea kutekeleza programu za Access ambazo huimarisha stadi za Kiingereza kwa vijana kutoka jamii masikini.

Programu zinawajengea uwezo katika stadi za uongozi na raia wawajibikaji katika maeneo ya Kigoma, Dodoma na Pemba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ubalozi huo jana jijini Dar es Salaam, Ofisa wa Kanda wa Programu za Kiingereza (Regional English Language Officer - RELO), Diane Millar, anayesimamia programu ya Wizara ya Mambo ya Nje Marekani inayotoa mafunzo ya Kiingereza na kuwaendeleza walimu kitaaluma katika nchi 15 za Afrika Mashariki, alitembelea Tanzania kuanzia Mei 15, mwaka huu.

Aidha, katika ziara hiyo, alikutana na viongozi wa serikali, viongozi wa taasisi za kielimu na vyama vya walimu, pamoja na kuzindua programu mpya za mafunzo ya Kiingereza.

Pia, aliendesha warsha za mafunzo kwa walimu na kuangalia matokeo ya programu za Marekani nchini Tanzania.

Akiwa kwenye maeneo hayo, Millar alizindua programu mpya za mafunzo ya Kiingereza (English Access Microscholarship Program - Access) ambazo zitatekelezwa hadi mwaka 2024.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa, programu za Access huimarisha stadi za kiingereza kwa vijana kutoka jamii masikini, huku ikiwajengea uwezo katika stadi za uongozi na kuwa raia wanaowajibika.

Ilisema kwa kawaida wahitimu wa programu hiyo huwa viongozi katika shule zao, hufanya vizuri zaidi katika mitihani yao na hupata fursa nyingi na nzuri zaidi za kujiendeleza kielimu.

"Wahitimu hawa siyo tu hupata kazi nzuri zaidi bali pia hutengeneza nafasi za kazi katika jamii zao. Washiriki wa programu hizi huwa na uwezo zaidi wa kushindania fursa za kushiriki katika programu za mabadilishano na masomo nchini Marekani,"ilifafanua taarifa hiyo. Nchini Tanzania, programu hizo zimeshafanyika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Unguja, Pemba, Mwanza, Tanga, Mbeya na Lindi huku wanufaika wakiwa ni 500.

Millar alikutana pia na viongozi na wanachama wa Chama cha Walimu wa Kiingereza Tanzania (TELTA) na Chama za Walimu wa Kiingereza Zanzibar (ZAPELATO) na kufanya nao kazi ya kuandaa na kuendesha warsha kwa walimu katika mikoa hiyo.

Akiwa Dar es Salaam, alikutana na wahitimu wa programu maalumu iitwayo Kinful program, inayoendeshwa na ubalozi na kufadhiliwa na ofisi ya RELO.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, ililenga kuwajenga wanafunzi wa sekondari mkoani humo, Morogoro na Mtwara katika stadi za kijamii na kujitambua, matumizi ya teknolojia za kidijitali, fikra na tafakuri tunduizi, uongozi na stadi za kiingereza. Ilisema kuwa wahitimu walieleza jinsi programu hiyo ilivyowasaidia kuwa wanafunzi wazuri na wanaowajibika na kujituma zaidi, kwa kuwafanya kuwa viongozi wanaojiamini na wenye kujali hisia za wengine, pamoja na kusikiliza na kuzungumza kiingereza.

# Rais Mwinyi atoa pole shule iliyoungua moto

**Na Mwandishi Maalum,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametuma salamu za pole kwa wanafunzi pamoja na walimu wa Shule ya Sekondari ya Kengeja Ufundi kisiwani Pemba kutokana na kuungua moto kwa bweni la wanawake katika shule hiyo.

Katika salamu hizo za pole, Rais Dk. Mwinyi alieleza jinsi alivyopokea kwa mshtuko na huzuni taarifa za tukio hilo lililotokea jana, likisababisha uharibifu wa jengo hilo, vitanda, vifaa vya kusomea vya wanafunzi pamoja na vifaa vingine vya matumzi ya wanafunzi.

Katika salamu hizo za pole, Rais Mwinyi alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itachukua juhudi za makusudi katika kuhakikisha inaweka mazingira mazuri mbadala wakati huu kwa wanafunzi hao pamoja na kuhakikisha hali ya daghalia (bweni) hiyo inarejea kama ilivyokuwa mwanzo ili waendelee na masomo yao.

Rais Mwinyi pia alitumia fursa hiyo kuzitaka taasisi husika kufanya uchunguzi wa kina juu ya ajali hiyo ya moto ili majanga kama hayo yasitokee kwa mara nyingine tena, hasa ikizingatiwa kwamba tayari matukio kama hayo yamesharipotiwa hivi karibuni katika Shule ya Utaani na Madungu kisiwani humo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Massoud, viashiria vya mwanzo vya tukio hilo la moto vinaonyesha kwamba linatokana na hitilafu ya umeme lakini hakuna mwanafunzi aliyepata majeraha ya moto huo na wanafunzi wote wako salama.

Alisema athari zaidi imetokea kwa kuungua jengo pamoja na vifaa vyote vya wanafunzi vilivyokuwamo ndani huku akisema kwamba serikali ya mkoa inaendelea na uchunguzi juu ya tukio hilo sambamba na kuwasilisha misaada mbalimbali kwa ajili ya wanafunzi hao ili waendelee na masomo yao ipasavyo.



Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Lyidia Shio (kulia), akitoa elimu kuhusu masuala mbalimbali ya kodi kwa mafundi seremala Kongowe wilayani Mkuranga mkoani Pwani jana, wakati wa kampeni ya utoaji elimu kwa mlipakodi ya mlango kwa mlango inayoendelea wilayani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mkenda aipongeza NMB udhamini Wiki ya Ubunifu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameishukuru Benki ya NMB kwa kushiriki na kudhamini maonyesho ya Kitaifa ya Wiki ya Ubunifu iliyoanza jana katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Waziri Mkenda aliyasema hayo alipokuwa anaongozana na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Othman Masoud Othman ambaye ndiye aliyekuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa maonyesho hayo walipotembelea banda la Benki ya NMB.

"Tuna kila sababu ya kuishukuru Benki ya NMB kwani wamekuwa karibu na Wizara ya Elimu na kutupa sapoti, wameisaidia sana wizara hasa katika kuhakikisha vijana wanakuwa wabunifu hata katika masomo yao," alisema Prof. Mkenda.

Mkenda aliongeza kuwa NMB imekuwa karibu na wizara hata katika utoaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi kuanzia ngazi ya diploma hivyo kusaidia wanafunzi wengi kujiunga na vyuo kuanzia mwaka ujao wa masomo.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alimweleza Makamu wa Pili wa Rais kuwa Benki ya NMB ina thamini sana ubunifu na kwa kupitia bunifu mbalimbali, Benki ya NMB imekuwa ikiibuka na masuluhisho bora zaidi ambayo yamekuwa na manufaa kwa benki na sekta ya fedha kwa ujumla.

"Benki ya NMB inathamani sana ubunifu kwani kupitia ubunifu ndipo tumewaletea wateja wetu na Watanzania kwa ujumla masuluhisho bora ambayo ndiyo yamekuwa yakifanya benki yetu kuendelea kuwa na mafanikio makubwa zaidi," alisema Mlozi.

# Shahidi alivyougua ghafla kizimbani kesi ya mauaji

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

SHAHIDI wa tatu wa Jamhuri, Robert Kasuhuke ameugua akiwa kizimbani na kushindwa kutoa ushahidi wake katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita kwenye kesi ya mauaji ya kukusudia inayowakabili washtakiwa watatu.

Washtakiwa hao ni Juma Gulaka, Juma Kasanana na Bahati John wote wameshtakiwa kwa tuhuma za kumuua January Kasuhuke kwa kukusudia kwa kumcharanga mapanga shingoni, kichwani na mguu wake wa kushoto na kufariki dunia papo hapo.

Aliugua ghafla juzi jioni baada ya kuitwa na karani wa Mahakama hiyo, Ignas Kalihamwe na baada ya kuapishwa, shahidi huyo alinyoosha mkono na kusema mapigo ya moyo yanaenda hivyo asingeweza kuendelea kutoa ushahidi.

Jaji wa Mahakama hiyo, Liliani Itemba aliamuru shahidi huyo apewe kiti akae, lakini shahidi huyo alikataa ndipo Jaji Itemba akamwambia Wakili wa Serikali James Pallangyo amtoe shahidi huyo nje ili akapate hewa.

Upande wa Jamhuri ulikuwa ukiongozwa na mawakili wawili wa serikali ambao ni James Pallangyo na Monika Matwe na upande wa utetezi wa washtakiwa ulikuwa ukiongozwa na mawakili watatu wa kujitegemea ambao ni Laurent Bugoti, Erick Rutehanga na Nestory Kuyula kila mmoja anamtetea mshtakiwa mmoja mmoja.

Baada ya dakika 20 kupita Wakili wa Serikali Pallangyo aliomba Jaji Itemba ili aweze kumleta shahidi mwingine kwa sababu shahidi Robert Kasuhuke aweze tena kuendelea na ushahidi wake kwa sababu hali yake haikuwa imetengemaa.

Jaji Itemba alikubaliana na ombi hilo na Pallangyo akamleta shahidi mwingine kwa ajili ya kutoa ushahidi.

Shahidi wanne upande wa Jamhuri, Simoni Kashusha (59) mkazi wa Mtaa wa 14 Kambarage akiongozwa na Wakili wa serikali Pallangyo, alidai kuwa mwaka 2010 alikuwa mjumbe wa nyumba 10 na Machi 31, mwaka 2010, majira ya saa tatu asubuhi akiwa anafanya usafi wa mazingira nyumbani kwake walifika askari polisi wawili wakiwa wamevaa kiraia na kumwambia kuwa aongozane nao kwa jirani yake Rubeni Simoni kwa ajili ya upekuzi.

Alidai baada ya kufika nyumbani kwa Simoni waliingia ndani na Simoni aliwapeleka hadi chumbani kwake na kuinua godoro na kutoa kelia ya baiskeli, na alipoulizwa Rubeni Simoni kelia hii ya baiskeli ni ya nani alijibu ni yake anataka aipake rangi.

Alidai baada ya majibu hayo ndipo ndugu wa marehemu Barabara Kasuhuke aliitambua kelia hiyo kuwa ni ya baiskeli ya marehemu January Kasuhuke baada ya ndugu wa marehemu huyo kutambua kelia hiyo wote kwa pamoja waliandika majina yao kisha wakasaini na baada ya kusaini polisi walimchukua Samoni na kuondoka naye katika kituo cha polisi Geita.

Baada ya shahidi wa upande wa Jamhuri kumaliza kutoa ushahidi wake, mawakili watatu wa kujitegemea walimuuliza Jamhuri maswali kama ifuatavyo;

Wakili: Shahidi wakati mnaingia kwenye nyumba ya Rubeni Simoni ulikuwa unajua ni kitu gani kinafanyika?

Shahidi: Hapana.

Wakili: Shahidi uliona Rubani akiwakagua askari polisi?

Shahidi: Hapana.

Wakili: Shahidi ni mara ngapi unashiriki katika upekuzi wa aina hiyo?

Shahidi: Ni mara nyingi tu.

Wakili: Je, unawajuwa watu waliohusika kwenye tukio la mauaji?

Shahidi: Hapana.

Baada ya mawakili watatu wa kujitegemea kumaliza kumuuliza shahidi wa upande wa Jamhuri maswali, Wakili wa serikali alimuuliza shahidi wake maswali ya kama ifuatavyo;

Wakili: Shahidi askari polisi walikuwa wamevaa makoti?

Shahidi: Hapana walikuwa wamevaa kiraia nguo za kawaida.

Wakili: Shahidi kelia hiyo ya baiskeli inaweza kuwekwa kwenye mfuko?

Shahidi: Hapana kelia hiyo haiwezi kuwekwa kwenye mfuko kwa sababu ni kubwa.

Baada ya upande wa Jamhuri kumaliza kuuliza maswali shahidi wake aliomba mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kuendelea na kusikiliza mashahidi wengine waliyobakia.

Jaji Itemba alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hadi leo kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine waliyobakia.

Akisoma hati ya mashtaka jana msaidizi wa kumbukumbu wa Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Ignas Kalihamwe, alidai hapo mahakamani kuwa Februari 3, mwaka 2010, katika eneo la msitu wa Samina Mkoa wa Geita washtakiwa wote kwa pamoja walimuua kwa kukusudia January Kasuhuke kwa kumcharanga mapanga shingoni, kichwani na mguu wake wa kushoto na kufariki dunia papo hapo.

HABARI KITAIFA

# Mbunge ataka MSD ifumuliwe ipasavyo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, ametaka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ifumuliwe ipasavyo hadi madereva badala ya kuitazama menejimenti peke yake.

Akichangia juzi makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/23, Chikota alisema wafanyakazi wa kati wana uwezo wa kumkwamisha mkurugenzi wa taasisi.

"MSD wanasambaza dawa ukiona kama kuna madereva wanaotaka kukwamisha utendaji kazi anauwezo wa kumwambia ofisa utumishi huyu ni CEO wa nane kwenye hii taasisi hanibabaishi na akashindwa kupeleka dawa kwa wakati, kufumuliwa kwa MSD kusiwe ni kwa bodi na menejimenti pekee, twende hadi madereva na watumishi wa kati,"alisema.

Alieleza kuwa lengo ni MSD itekeleze majukumu yake ipasavyo. Aidha, alimpongeza Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kwa kutoa takwimu za kweli kuhusu hali ya upatikanaji wa dawa ambayo kwa sasa ni asilimia 51.

"Nakupongeza waziri maana huko nyuma tulikuwa tukiletewa takwimu lakini kihalisia hazikuwa za kweli umeona badala ya kuwadanganya Watanzania umeamua kusema ukweli,"alisema.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa maagizo aliyoyatoa kuhusu MSD na kwamba kuna kazi ya kufanyika kwa kuwa mafanikio ya taasisi hayategemei menejimenti.

Kuhusu upotevu wa dawa, Chikota alitaka udhibitiwe hasa kwa wanaojificha kwenye mgongo wa dawa.

"Bajeti ya MSD inapaswa kuongezwa na tulifanya marekebisho ya sheria kwamba wanaweza kujenga viwanda vya dawa, wa mradi pale Keko ambao unahitaji mtaji ili wazalishe dawa zenye ubora na kuuza nchi jirani,"alisema.

Kadhalika, alisema zinahitajika jitihada za makusudi katika kuajiri watumishi wa afya kwa kutoa kibali maalum ili kuondokana na upungufu uliopo wa asilimia 55.

"Changamoto hii ni kubwa sana hasa tunapokwenda maeneo ya vijijini kwa mfano katika jimbo langu la Nanyamba kuna upungufu wa asilimia 79 kuna mahitaji 425, waliopo 106 tu naomba tutoe kibali maalum, kituo kama Majengo hakuna madaktari kuna wauguzi tu ndio wanaotoa huduma hii ina madhara makubwa sana,"alisema.

Alisema pamoja na serikali kujenga vituo vya afya lakini bado kunahitajika kibali maalum cha kuajiri watumishi ili kutoa huduma kwenye vituo hivyo.

"Naomba Mheshimiwa Ummy na timu yako muongeze idadi ya watumishi kwenye Hospitali ya Kanda ya Kusini ili wananchi wapate huduma za kibingwa. Nipongeze serikali kwa kutenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya kununua vifaa muhimu kama MRI, vifaa hivyo msambazaji alete kwa wakati ili kuleta huduma iliyokusudiwa,"alisema.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (watatu kulia), akitapa maelezo kutoka kwa Meneja Mradi wa Zantel, Mohamed Ahmed Jai, apotembelea kukagua shughuli ya ujenzi wa minara ya mawasiliano ya Tigo-Zantel, Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ushirika waongeza uzalishaji korosho

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

CHAMA Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Wilaya ya Tunduru (TAMCU LTD) kimejipanga kuongeza uzalishaji wa zao la korosho kutoka kilo 25,284,493 za msimu wa mwaka 2021/2022 hadi kilo 32,000,000 katika msimu 2022/2023.

Hayo yaliainishwa na Meneja Mkuu wa TAMCU, Imani Kalembo, wakati akitoa taarifa za maandalizi ya msimu mpya wa korosho kwa wajumbe wa mkutano mkuu wa kawaida wa 19 wa chama hicho.

Alisema kuwa katika kipindi cha msimu wa mwaka 2021/2022 TAMCU iliweka malengo ya kukusanya na kuuza korosho kilo milioni 25, lakini ilikusanya na kuuza kilo 25,284,493 zenye thamani ya Sh. 50,471,797,263.00 na hivyo kuvuka malengo kwa asilimia 101.14.

Akizungumzia uzalishaji wa zao la mbaazi katika msimu 2021/2022 ambapo zao hilo liliuzwa kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani ambapo minada sita ilifanyika wakulima wa wilaya hiyo waliuza kilo 4,111,845 zenye thamani ya Sh. 5,235,425,002.00 .

Manjaule aliendelea kuelezea kuwa kufutia hali hiyo uzalishaji wa mbaazi uliongezeka kutoka kilo 2,206,296 za msimu 2020/2021 hadi kilo 4,111,845 zilizo zalishwa katika msimu wa mwaka 2021/2022.

Alisema hata hivyo kupitia vikao vya chama kikuu kupitia maoteo ya uzalishaji katika msimu wa mwaka 2022/2023 wamepanga kuongeza uzalishaji hadi kilo 5,451,000.

# NEMC yafunguka athari za mazingira bomba la mafuta

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Usimamizi na Utunzaji Mazingira (NEMC), limesema ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoliani Tanga hautasababisha athari za mazingira kama inavyovumishwa na wanaharakati mbalimbali.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam, na Mkurugenzi Mkuu wa baraza hilo, Dk. Samuel Gwamaka, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kufafanua uvumi huo.

Alisema kuna upotoshaji mkubwa unaofanywa na baadhi ya vyombo vya habari vya mataifa ya nje kwamba utekelezaji wa mradi huo utakuwa na athari kubwa za mazingira jambo ambalo sikweli.

"Mmesikia kwenye vyombo vya habari na wanaharakati wanapinga ujenzi wa hili bomba na taarifa zimesambaa sehemu mbalimbali na nchi jirani tumeona watu wakipinga wakidai kutakuwa na athari za mazingira.

"Sasa kwa sababu suala la athari za mazingira linasimamiwa na NEMC tumeona tuweke ukweli hapa wananchi waelewe tusipotoshwe na watu wengine ambao wala hawahusiki kwenye huu mradi wa mafuta," alisema Dk. Gwamaka.

Mkurugenzi alisema bomba hilo linatarajiwa kujengwa na maandalizi yote yameshaanza na unatekelezwa kwa ubia baina ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda na Kampuni ya TOTAL Energies.

Dk. Gwamaka alisema bomba hilo litakuwa na urefu wa kilomita 1,148 litapita katika mikoa nane na wilaya 24 na kwenye eneo la Chongoleani Tanga ambapo ndipo mwisho wa bomba hili itajengwa bohari kubwa na miundombinu ya kuhifadhia mafuta.

"Niwahakikishie Watanzania kwamba NEMC imehakikisha mradi huu unazingatia masuala yote ya hifadhi ya mazingira kabla na wakati wa utekelezaji wake, ulisajiliwa kwenye baraza mwaka 2017 na Kampuni ya TOTAL ambao ndio wawekezaji karibu miaka mitano iliyopita," alisema.

"Walipewa usajili namba 6725 kwa ajili ya mchakato wa kufanya tathmini ya athari za mazingira (EIA) na kampuni elekezi zilizofanya tathmini hiyo ni pamoja na Kampuni ya Uingereza na Kampuni ya Tanzania wakiwa wataalamu washauri," alisema.

Alisema NEMC ilijihakikishia kwamba wanazingatia athari za mazingira na kushirikisha wadau muhimu kwenye mikoa nane na wilaya 24 na vijiji vyote ambako bomba linapopita na taasisi za serikali na za binafsi maoni yao yalichukuliwa kuhusu mradi huo.

Alisema mwaka 2019 timu ya wataalamu kutoka NEMC na wataalamu wa sekta mbalimbali walifanya ziara sehemu bomba hilo litakapopita na tathmini ya EIA ilifanyika kwa awamu mbili ambapo wadau wengi walihusika kutoa maoni yao.

Dk. Gwamaka alisema NEMC ilijihakikishia na kuhakiki andiko la tathmini linazingatia na kuweka mipango yote ya kuhifadhi mazingira na masuala ya kijamii na kushirikisha wadau muhimu wa mikoa yote nane na wilaya zote 24 ambapo bomba hilo litapitia.

Alisema mapitio ya tathmini ya athari za mazingira ilifanyika kwa awamu mbili ambapo tathmini ya kwanza ilihusisha kikao cha kupata maoni ya wadau wote kuanzia ngazi ya kitaifa wizara zote na mikoa yote.

Alisema awamu ya pili ilikuwa ni kikao cha kamati ya wataalamu (technical advisory committee kilichofanyika Aprili 2009 kwa kushirikisha wataalamu wa NEMC, vyuo vikuu na taasisi za serikali na wawakilishi wa mradi na baada ya kikao cha tathmini mradi uliidhinishwa na waziri wa mazingira na kupatiwa cheti mwaka 2019.

"Mradi huu umefuata sheria zote za nchi hii na kanuni zote inazosimamia miradi na mazingira na uwekezaji ndiyo maana ukapitishwa na tukawapa cheti na tunafuatilia kuona kama tuliyokubaliana yanatekelezwa," alisema.

Alisema hatua za awali za ujenzi wa miundombinu muhimu zimeanza baada ya watu waliokuwa kwenye maeneo bomba litakapopita kulipwa fidia.

"Baraza linafuatilia kwa karibu kila kinachoendelea ili kuona kama kinachofanyika kinaendana na andiko la tathmini ya athari kwa mazingira na tunafanya vikao vya majadiliano kutatua changamoto zinazojitokeza," alisema Dk. Gwamaka.

# Wabunge waihoji serikali uvujaji wa mitihani nchini

WABUNGE wameibana serikali kueleza namna ilivyojipanga kukomesha kuvuja kwa mitihani nchini.

Hata hivyo, serikali imewatoa hofu wabunge kwa kuweka wazi hatua mbalimbali za kudhibiti vitendo hivyo huku ikidai kuwa kwa sasa usahihishaji wa mitihani utafanyika kwa mtandao (emarking).

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko, akiuliza swali bungeni jana, alisema bado uvujaji wa mitihani unaendelea na kutaka kujua ni kwa namna gani serikali itakomesha tabia hiyo.

"Tumeshuhudia wazazi na watoto wasio na hatia kubebeshwa mzigo wa kufutiwa matokeo na wakati mwingine kufungiwa, je ni kwa namna gani serikali itaondoa mzigo huu?" Alihoji.

Mbunge wa Newala Vijijini (CCM), Maimuna Mtanda, alihoji mkakati wa serikali wa kuongeza posho kwa wasimamizi ili kuondokana na udanganyifu na uvujaji wa mitihani.

Mbunge wa Viti maalum (CCM), Maryam Mwinyi, alitaka serikali kutokusubiri udanganyifu wa mitihani ndio itoe adhabu.

Mbunge wa Viti maalum (CCM), Yustina Rahhi, alisema kitendo cha kutumia polisi kusimamia mitihani kinasababisha wanafunzi kupata taharuki na kushindwa kufanya vizuri.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, alisema serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kwa lengo la kukomesha tabia ya udanganyifu katika mitihani ya Taifa ikiwamo mitihani ya kumaliza elimu ya msingi, sekondari na vyuo.

" Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa walimu, wasimamizi wa mitihani na wadau wote wa elimu kuhusu athari za udanganyifu katika mitihani ili kuhakikisha kuwa wanatekeleza jukumu la usimamizi wa mitihani hiyo kwa uadilifu na kwa kuzingatia kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa kwa ajili ya uendeshaji wa mitihani,"alisema.

Alitaja hatua nyingine ni za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za nchi na zinachukuliwa kwa walimu, wasimamizi na wadau wote wanaohusika katika kusimamia mitihani pale ambapo ilibainika pasi shaka kuwa wameshiriki katika kosa hilo.

Alibainisha kuwa serikali itaendelea kuwachukulia hatua kali kwa mujibu wa sheria kwa wahusika wote wanaojihusisha na udanganyifu wa mitihani ili kuhakikisha kuwa nchi inapata wataalamu wenye sifa stahiki.

Hata hivyo, alisema suala la kuvuja mitihani halipo na mara ya mwisho ilivuja mwaka 2008 na ilikuwa somo la hisabati.

"Matukio ya udanganyifu ni baada ya mitihani kufunguliwa, suala la uvujaji tulishatokomeza sasa tunashughulika na udanganyifu wa mitihani,"alisema.

Kuhusu posho, Kipanga alisema taratibu za usahihishaji mitihani kwa sasa zinakwenda kubadilika na kwamba kwasasa wapo kwenye majaribio ya mitihani ya ualimu na baadaye itakuwa kwa mitihani ya kidato cha nne na sita.

Alisema itapunguza gharama ya walimu kusogea kwenye maeneo ya kusahihisha na pia imejipanga kuboresha posho kwa wasimamizi na wasahihishaji wa mitihani.

Akizungumzia kuhusu polisi, Kipanga alisema polisi hawasimamii mitihani na hawaingii kwenye chumba cha mtihani bali ni sehemu ya kikosi kazi cha usalama wa mitihani.

## Serikali yafanya utafiti sifa mbao za matumizi

WIZARA ya Maliasili na Utalii, imefanya utafiti kuhusu tabia na sifa za mbao za matumizi kutoka kwenye miti isiyofahamika sana kutokana na kuwapo na tatizo la upatikanaji wa miti migumu hasa jamii ya mninga na mkongo.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja alieleza hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Naghenjwa Kaboyoka.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema zabuni za serikali zinataka viwanda vya samani kutengeneza kwa kutumia mbao za mninga na mkongo. "Je, serikali haioni imefika wakati wa kutumia mbao za mitiki ambayo ina ubora sawa na mninga na mkongo?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Masanja, alisema utafiti huo uliolenga kutambua tabia na sifa za kimwonekano, kiufundi na kianatomiki za mbao za miti isiyojulikana sana, ulionyesha kuwa mti wa mitiki, una sifa ama sawa au zinazokaribiana sana na miti ya mkongo na mninga.

"Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huo, serikali inaangalia uwezekano wa kuongeza miti mipya iliyofanyiwa utafiti katika orodha ya miti iliyoainishwa katika sheria ya manunuzi inayosimamiwa na PPRA ili itumike katika kutengeneza samani za serikali,"alisema.

Awali, alibainisha kuwa shughuli za ujenzi na utengenezaji wa samani ambazo kiuhalisia zimekuwa zikikua sambamba na ongezeko la watu, zinategemea sana rasilimali ya misitu kama chanzo cha malighafi.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kulia), akiwa na Naibu wake, Antony Mavunde, wakiingia bungeni kwa ajili ya kuwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, kwenye vikao vya Bunge la bajeti vinavyoendelea, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Ataka mkakati udhibiti magari ya mizigo K'koo

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Asha Abdallah Juma, ametaka mkakati wa kudhibiti magari yanayopakua na kupakia mizigo katika maeneo ya Kariakoo, jijini Dar es Salaam.

Maeneo hayo ni Mtaa wa Msimbazi na barabara ya Morogoro mkoani Dar es Salaam, ili kupunguza msongamano ambao umekuwa kero kwa wananchi.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema bado kuna kero ya magari hayo na yanahatarisha usalama na afya za wananchi wa maeneo hayo.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema katika kudhibiti magari makubwa yanayopakia na kupakua mizigo kwenye eneo hilo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweka utaratibu wa kudhibiti magari hayo kwa kutoa vibali Maalum vinavyowaruhusu kuingia mjini.

"Kama ilivyotamkwa kwenye Kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo za Matumizi ya Barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala (ambayo ndiyo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa sasa) za mwaka 2015,"alisema.

Hata hivyo, alisema mtu yeyote atakayeingiza lori au kontena bila kibali atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Sh.50,000 hadi Sh. 300,000 kulingana na uzito wa gari au kifungo kisichozidi miezi 12 jela au vyote kwa pamoja.

"Pia halmashauri kwa kushirikiana na vyombo vingine, ina utaratibu wa kutoa elimu kwa madereva, wamiliki wa magari makubwa na kwa umma ili kuwapa uelewa wa athari zinazotokana na uingizaji wa magari makubwa kiholela," alisema.

Kadhalika, alisema Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ina mpango wa kujenga maegesho ya kisasa katika eneo la Mnazi Mmoja kwa ajili ya magari mbalimbali yakiwamo ya mizigo.




Habari zote na Augusta Njoji

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2022/23

## VIJANA NA KILIMO



Sh. bilioni moja zitatumika kama dhamana ya mikopo kwa vijana ili kuongeza ushiriki wa vijana kwenye kilimo na kuzalisha ajira

## RUZUKU YA MBOLEA

Wizara inatarajia kutumia Sh. bilioni 150 kutoa ruzuku ya mbolea kwa mazao yote



## UZALISHAJI KOROSHO

Kupitia Bodi ya Korosho Tanzania, wizara imepanga kuongeza uzalishaji kutoka tani 238,555.81 mwaka 2021/2022 hadi tani 400,000 mwaka 2022/23.



## UZALISHAJI SUKARI

Wizara kupitia Bodi ya Sukari itaongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 372,210 mwaka 2021/2022 hadi tani 450,000 mwaka 2022/2023.



## BAJETI YA KILIMO

Imeongezeka kwa mafungu yote matatu kutoka Sh. 294,162,071,000 mwaka 2021/22 hadi Sh. 751,123,280,000 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 155.34



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe

AJENDA 10/30
KILIMO NI BIASHARA

WWW.kilimo.go.tz | YouTube kilimo Tv | Wizara_ya_kilimo | tzagriculture





# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA HUSSEIN MOHAMED BASHE (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2022/2023

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya mwaka 2021/2022 na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023 ya Wizara ya Kilimo ambayo inagusa maisha ya watanzania.

3. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza mwaka mmoja tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu. Katika kipindi hicho, sekta ya kilimo imeongezewa bajeti katika maeneo ya utafiti wa kilimo, huduma za ugani, umwagiliaji na uzalishaji wa mbegu; na kuimarisha masoko ya mazao ya kilimo. Aidha, niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kuendelea kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema ili awatumikie watanzania.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuhimiza kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na yeye mwenyewe kuwa mkulima.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake za kusimamia na kuendeleza mazao ya kimkakati na maendeleo ya ushirika nchini na yeye kuwa mkulima.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb.), Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb.) kwa kuendelea kukusaidia kikamilifu katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Nawapongeza pia Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo. Ninaahidi kwa Mheshimiwa Rais, Chama Cha Mapinduzi, wananchi wa Jimbo la Nzega mjini na watanzania wote kwa ujumla kwamba nitatumikia nafasi ya ubunge na uwaziri kwa bidii, maarifa, weledi na uadilifu ili kuweza kufikia malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na matarajio ya watanzania.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa furaha ninampongeza Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Mbunge wa Jimbo la Dodoma mjini kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo. Nitashirikiana naye kikamilifu katika kuleta mageuzi kwenye sekta ya kilimo nchini na hivyo kuwaletea wananchi maendeleo na kuondoa umasikini na kuifanya sekta ya kilimo kuwa msingi mkuu wa ajira nchini. Pia, ninamkaribisha Bw. Gerald Mweli, Naibu Katibu Mkuu aliyehamishiwa Wizara ya Kilimo kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, na Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Almas Athumani Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kwa ushirikiano mzuri na ushauri makini ambao wameendelea kuutoa kwetu wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/2022, na Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2022/2023.

   Ushauri wao umezingatiwa na tunaahidi kuendelea kushirikiana kwa ukaribu na Kamati katika kuendeleza kilimo hapa nchini.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninapenda kuishukuru Kamati ya Bajeti kwa maoni na ushauri walioutoa wakati wa majadiliano ya utekelezaji na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Ninapenda kutumia fursa hii kuihakikishia kamati kuwa maoni na ushauri wao umezingatiwa kwenye mpango na pia utazingatiwa katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/2023.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.) pamoja na timu yake ya wataalam kwa kutupa nafasi ya kutusikiliza, kujadiliana na kushauriana kuhusu namna bora ya kutekeleza vipaumbele vya Sekta ya Kilimo na kuipa sekta kipaumbele katika Mpango wa Bajeti ya Serikali.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwapongeza Mhe. Emmanuel Peter Cherehani kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Shinyanga, Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mhe. Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako Tukufu limepata pigo la kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Elias Kwandikwa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji Mhe. William Tate Ole Nasha na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa Mhe. Irene Alex Ndyamkama. Ninatoa pole kwa wabunge, familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na wapendwa wetu. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina!

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee ninawashukuru viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano wao na bidii yao katika kazi. Ninamshukuru sana Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde (Mb), kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Ninamshukuru Bw. Andrew Wilson Massawe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, na Profesa Siza Donald Tumbo, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa ambao wanaoendelea kuutoa.

**1.1 Mchango wa Serikali katika Sekta ya Kilimo kwa Awamu zote Sita za Uongozi**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Kwanza, ilitambua Tanzania kama nchi ya Wakulima na Wafanyakazi na kuwekeza katika kilimo hususan katika maeneo yafuatayo:- Vyuo vya Utafiti na Mafunzo, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Mashirika ya Umma yanayosimamia Kilimo, Bodi za Mazao na Vyama vya Ushirika. Pia ilihamasisha kilimo na lishe kupitia programu na kampeni mbalimbali ikiwemo Ukulima wa Kisasa, Kilimo cha kufa na kupona, Chakula ni Uhai, Mtu ni Afya, Elimu ya Kujitegemea na Siasa ni Kilimo. Aidha, katika kipindi hicho, msisitizo uliwekwa katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kufikia kiwango cha kuongoza kimataifa kwa baadhi ya mazao ikiwemo korosho na mkonge kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1 Ukurasa namba 10 na Kielelezo Na. 2. Ukurasa namba 11 kwenye kitabu cha hotuba yangu.**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Pili, ilifanya mageuzi ya uchumi yaliyokuwa kichocheo katika maendeleo ya kilimo ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sera ya Kilimo ya mwaka 1983. Aidha, Serikali ilipunguza vikwazo katika biashara ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa kwa ajili ya ustawi wa wananchi.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Tatu, iliimarisha Taasisi na kusimamia utawala bora, ilibinafsisha Mashirika ya Umma na Mashamba ya Umma, iliboresha Bodi za Mazao kwa kuzifanya Bodi hizo kuachana na biashara na badala yake kuwa Bodi za Udhibiti na Uendelezaji wa Mazao.
    Pia kwa kipekee iliunda Wizara ya Masoko na Ushirika na kuimarisha ugatuaji wa madaraka kwa kuimarisha Serikali za Mitaa ambapo huduma za ugani za Kilimo na Mifugo zilihamishiwa TAMISEMI.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Serikali ya Awamu ya Nne ilianzisha na kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP I), Programu ya Modenizesheni ya Ushirika, KILIMO KWANZA na SAGCOT. Pia, ilianzisha Benki ya Kilimo, Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo na taasisi mbalimbali ikiwemo Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Taasisi hizo zilianzishwa ili kuendeleza ufanisi wa kutoa huduma kwa wakulima katika upatikanaji wa pembejeo, miundombinu ya kilimo na ushirika.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Tano, ilianzisha na kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Pia, iliboresha na kuwekeza kwenye miundombinu ya barabara, reli, bandari, nishati, viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege kwa lengo la kuchochea uwekezaji katika sekta za uzalishaji.

20. Serikali pia, ilihamasisha ukuaji wa uchumi unaotegemea maendeleo ya viwanda vya kusindika na kuchakata mazao ya kilimo (*agro-processing*) ikiwemo viwanda vya sukari, mafuta ya kula, pamba na nafaka. Aidha, ilianzisha Mpango wa Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (*Blueprint*) na kutumia sera za kikodi kulinda viwanda vya mazao ya kimkakati yakiwemo sukari na mafuta ya kula.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** ukizingatia utekelezaji wa awamu zote tano, Serikali za Awamu ya Kwanza na Awamu ya Nne, ziliwekeza katika msingi mkuu wa uzalishaji. Serikali za Awamu ya Pili na ya Tatu zilifanya kazi kubwa ya kufungua biashara na kuweka mifumo ya kitaasisi. Serikali ya Awamu ya Tano ilifanya kazi kubwa ya kujenga miundombinu mbalimbali ambayo ni muhimu katika kuchochea uzalishaji, uongezaji wa thamani na usafirishaji.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhihirisha kwa vitendo utashi wa kisiasa kwa kutambua kuwa maendeleo ya uchumi yatatokana na sekta za uzalishaji hususan Sekta ya Kilimo. Azma hiyo itafikiwa kwa kuwekeza katika maeneo ya kimkakati ya utafiti, uzalishaji wa mbegu bora, uimarishaji wa huduma za ugani, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na uhifadhi wa mazao na uimarishaji wa upatikanaji masoko ya mazao ya kilimo.

23. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP-II) na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuwekeza na kufanya biashara katika Sekta ya Kilimo.

**1.2 Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Kilimo**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka mmoja cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali imeongeza bajeti ya utafiti wa kilimo kutoka Shilingi Bilioni **7.35** hadi Shilingi Bilioni **11.63**, huduma za ugani kutoka Shilingi Milioni **603** hadi Shilingi Bilioni **11.5**, umwagiliaji kutoka Shilingi Bilioni **17.7** hadi Shilingi Bilioni **51.48** na uzalishaji wa mbegu kutoka Shilingi Bilioni **5.42** hadi Shilingi Bilioni **10.58.**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza fedha za ununuzi wa nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) kutoka Shilingi Bilioni **19** mwaka 2020/2021 hadi Shilingi Bilioni **119** mwaka 2021/2022. Hadi Aprili, 2022 fedha hizo zimewezesha ununuzi wa tani 183,045.384 za mpunga, mahindi na mtama ambazo zitauzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za ugani katika kipindi hicho, Serikali imewezesha ununuzi wa Pikipiki 7,000 kwa ajili ya maafisa ugani ili kurahisisha usafiri; vishikwambi (*Tablets*) 384 kwa maafisa Ugani 384; visanduku vya ufundi (*Extension kits*) 6,700 kwa maafisa ugani; na vifaa vya kupima Afya ya Udongo (*Soil Scanner*) 143 kwa Halmashauri 143. Jumla ya Shilingi Bilioni **9.29** zimetumika kununua vifaa hivyo.

27. ***Mheshimiwa Spika***, eneo linalomwagiliwa limeongezeka kutoka hekta 695,045 mwaka 2020/2021 hadi hekta 727,280.6 mwaka 2021/2022. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 60.6 ya lengo la kufikia hekta milioni 1.2 ifikapo 2025 kama inavyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imesimamia dhana ya kilimo ni biashara kwa kuimarisha mahusiano ya kimataifa ambayo yamefungua fursa ya masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi. Jitihada hizo zimewezesha kupatikana kwa fursa za masoko mapya ya mazao nje ya nchi ikiwemo soko la parachichi katika nchi za India na Afrika Kusini, ndizi nchini Kenya na mchele nchini Ubelgiji baada ya kukidhi viwango vya ubora.

29. Aidha, upatikanaji wa masoko umeongeza mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi ikiwemo mchele kutoka tani 184,521 zenye thamani ya Shilingi Bilioni **176.49** mwaka 2020 hadi tani 441,908 zenye thamani ya Shilingi Bilioni **476.8** mwaka 2021. Vilevile, mahindi kutoka tani 92,825 zenye thamani ya Shilingi Bilioni **58.02** mwaka 2020 hadi tani 189,277 zenye thamani ya Shilingi Bilioni **72.4** mwaka 2021 na parachichi kutoka tani 6,702 zenye thamani ya Shilingi Bilioni **14.93** mwaka 2020 hadi tani 12,250 zenye thamani ya Shilingi Bilioni **24.95** mwaka 2021. **Kielelezo Na.3. Ukurasa namba 18 wa kitabu cha hotuba yangu.**

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Serikali imeongeza mtaji katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kutoka Shilingi Bilioni **60** hadi Shilingi Bilioni **268** sawa na ongezeko la asilimia 346.7. Kutokana na ongezeko hilo, TADB imeweza kutoa mikopo ya Shilingi Bilioni **116.63** kwenye miradi 197 ya maendeleo na kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa tangu kuanzishwa kwa benki kufikia Shilingi Bilioni **482.4**. Aidha, benki hiyo imewezesha wakulima 1,527,175 kupata dhamana ya mikopo ya kiasi cha Shilingi Bilioni **144**.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imewezesha kupunguza riba za mikopo ya kilimo katika benki za biashara kutoka kati ya asilimia 17 na 20 hadi kufikia asilimia tisa (9). Punguzo hilo limewezesha wakulima kununua pembejeo kwa ajili ya uzalishaji, kuanzisha na kufufua viwanda vidogo ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

32. Pia, Serikali imetoa ruzuku za pembejeo za kilimo kwa mazao ya korosho, tumbaku na pamba zenye thamani ya Shilingi Bilioni **178.84**. Kadhalika, katika kipindi hicho Serikali imewezesha uundaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika na ununuzi wa magari 15, pikipiki 137 na kompyuta 82 kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vyama vya ushirika nchini. Jumla ya Shilingi Bilioni **2.44** zimetumika kuunda mfumo na kununua vitendea kazi hivyo.

33. Mafanikio mengine na matokeo ya ziara ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi mbalimbali ni kama ifuatavyo:
    i. Nchini Ufaransa – Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imesaini mkataba wa mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya Euro milioni 80 (sawa na Shilingi Bilioni 210) wenye lengo la kuimarisha benki hiyo ili kutoa mikopo ya muda mfupi na mrefu kwa sekta ya kilimo nchini;
    ii. Uwekezaji mkubwa katika sekta ya Mbolea – kwa sasa Kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited kutoka Burundi kinajenga kiwanda kikubwa cha mbolea katika Jiji la Dodoma chenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 180 na kinatarajiwa kutoa ajira za kudumu kwa wafanyakazi takriban 3,000 na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mbolea tani 600,000 kwa mwaka.
    Mbali na jitihada hizo, pia jitihada kubwa za kufungua masoko kwa ajili ya mazao ya kilimo ambapo hapo awali ilikuwa ni moja ya changamoto kubwa inayotukumba hivyo tunapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kutokana na juhudi zake za kuimarisha mahusiano na mataifa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na mataifa mengine jambo ambalo limechochea;
    i. Uondoaji wa vikwazo 56 vya biashara kati ya 64 vilivyokuwepo kati ya nchi ya Tanzania na Kenya hii ikiwa ni mafanikio ya utekelezaji wa makubaliano kati ya Viongozi wa Nchi hizo mbili. Jitihada hizo zimepelekea ukuaji wa biashara kati ya Tanzania na Kenya kufikia Dola za Marekani Milioni 905.
    ii. Upatikanaji wa soko la China kwaajili ya mazao (maharage ya soya na muhogo), jambo ambalo limetoa fursa ya soko la uhakika kwa wakulima wa mazao hayo nchini.

**1. HALI YA UPATIKANAJI WA CHAKULA**

34. ***Mheshimiwa Spika***, mahitaji ya chakula kwa mwaka 2021/2022 yamefikia tani milioni 14.83 ambapo tani milioni 9.44 ni za nafaka na tani milioni 5.38 ni mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji hayo ukilinganisha na upatikanaji wa tani milioni 18.66 kwa mwaka 2021/2022, Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 126. **Maelezo ya kina yanapatikana Ukurasa namba 22 hadi 24 wa kitabu cha hotuba yangu.**

**2. UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022**

**Maeneo ya kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2021/2022**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imetekeleza vipaumbele vifuatavyo; (i) Utafiti wa kilimo; (ii) Upatikanaji wa pembejeo; (iii) Kuimarisha kilimo cha Umwagiliaji; (iv) Huduma na mafunzo ya ugani; (v) Upatikanaji wa Masoko; (vi) Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji; na (vii) Kuimarisha Kilimo Anga.

**4.1 Makusanyo ya Maduhuli**

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi Bilioni **34.49** kupitia Fungu 43 na Fungu 05. Hadi Aprili, 2022, Wizara imekusanya Shilingi Bilioni **4.88** sawa na asilimia **14** ya makadirio. Serikali inaendelea kuboresha, kuimarisha na kutoa elimu ili kuongeza makusanyo.

**4.2 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Billioni **294.16**. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni **81.9** ni za matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni **211.24** ni za miradi ya maendeleo.

38. Hadi Aprili, 2022 Shilingi Bilioni **68.66** sawa na asilimia **83.82** ya fedha za matumizi ya kawaida zimetolewa na kutumika. Aidha, Shilingi Bilioni **83.2** ya fedha za maendeleo sawa na asilimia **39.38** ya fedha zilizotengwa zimetolewa na kutumika. Kati ya fedha za maendeleo za ndani zilizotengwa, Shilingi Bilioni **65.29** sawa na asilimia **55.7** zimetolewa na kutumika.

**4.3 Utekelezaji wa Maeneo ya Kipaumbele kwa mwaka 2021/2022**

**1.1.1 Utafiti wa Kilimo**

39. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa mbegu nchini, TARI imezalisha mbegu mama tani 19.998 na mbegu za awali tani 197.77. Kati ya mbegu za awali zilizozalishwa, tani 16.97 zimepelekwa ASA na tani 180.8 zimepelekwa sekta binafsi kwa ajili ya kuzalisha tani 5,933.1 za mbegu zilizothibitishwa. Vilevile, TARI imezalisha mbegu za msingi tani 134.60 ambazo zitawezesha uzalishaji wa tani 26,000 za mbegu zilizothibitishwa za mazao ya alizeti, maharage, mahindi, ngano, mtama, mpunga, ufuta, karanga, pamba na shayiri.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI imefanya utafiti kuhusu nafasi mpya ya kupanda pamba ambayo ni sentimita 60 kutoka mstari hadi mstari na sentimita 30 kutoka mche hadi mche badala ya nafasi ya awali ambayo ilikuwa ni sentimita 90 kwa sentimita 40. Nafasi hiyo mpya itaongeza mavuno kutoka wastani wa kilo 710 hadi kilo 1,422 kwa hekta. Aidha, TARI Ukiruguru wamebuni mashine ya kupanda pamba (*fabricate*) yenye uwezo wa kupanda ekari moja (1) kwa saa moja (1) hadi masaa matatu (3) badala ya masaa 11 kwa jembe la mkono.

41. Nitumie fursa hii, kuwapongeza Dauson Malela, Robert Cheleo Alphonce na Dkt. Paul Saidia ambao ni watafiti wa TARI-Ukiriguru kwa ubunifu wao wa kugundua na kutengeneza mashine hiyo rahisi ya kupandia.

**1.1.2 Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo**

**a. Mbegu bora**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2022 upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani 49,962.35 sawa na asilimia 26.68 za mahitaji ya tani 187,197 kwa mwaka. Kati ya mbegu hizo, tani 35,199.39 zimezalishwa ndani ya nchi, tani 11,340.2 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na sekta binafsi na tani 3,422.80 ni bakaa ya msimu uliopita.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imesambaza kwa wakulima tani 2,000 za mbegu za alizeti zenye thamani ya Shilingi Bilioni **5.84** kwa utaratibu wa ruzuku. Mbegu hizo, zimesambazwa katika mikoa ya Dodoma, Singida, Simiyu, Manyara na zinatarajiwa kuzalisha tani 400,000 za alizeti zitakazozalisha mafuta ya kula ya wastani wa tani 100,000.

44. Aidha, TARI imezalisha tani 37 za mbegu za ufuta na kusambaza tani 25 kwa wakulima na tani 18 za mbegu za karanga na kusambaza tani 15.5 kwa wakulima.

45. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia ASA, TARI, Bodi za chai, pamba, mkonge, korosho, pareto, kahawa na vikundi vya wakulima vimezalisha miche bora milioni 32.30 na mbegu tani 95,764 na kusambaza miche milioni 24.44 na mbegu tani 95,794 kwa wakulima (**Jedwali Na. 5. Ukurasa namba 42 wa kitabu cha hotuba yangu).** Aidha, Bodi ya Pamba Tanzania imesambaza tani 15,548 za mbegu za pamba kwa wakulima zinazotosha kupandwa katika hekta 621,920.

**b. Mbolea**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji na uingizwaji wa mbolea nchini ambapo hadi Aprili, 2022 tani 436,452 za mbolea zimepatikana sawa na asilimia 63 ya mahitaji ya tani 698,260 ya msimu wa 2021/2022. Kati ya hizo, tani 274,973 zimeingizwa kutoka nje ya nchi, tani 43,579 zimezalishwa nchini na tani 117,900 ni bakaa ya msimu wa 2020/2021 (**Jedwali. Na. 7 ukurasa namba 49 wa kitabu cha hotuba yangu).** Hadi Aprili, 2022 Bodi ya Tumbaku Tanzania kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika imesambaza mbolea NPK tani 20,689.9 na CAN tani 5,066.7 kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija.

**c. Viuatilifu**

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 upatikanaji wa viuatilifu vya udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya mimea umefikia lita 106,000 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni **3.11**. Hadi Aprili, 2022 jumla ya lita 34,817 za viuatilifu zimesambazwa kwa ajili ya kudhibiti nzi wa matunda na viwavijeshi.

48. Pia, Wizara imeiwezesha maabara ya TPHPA kupata ithibati na kusaidia mazao

ya kilimo yatakayopimwa katika maabara hiyo ili kukidhi viwango vya masoko ya kimataifa. Aidha, Wizara kupitia mradi wa Kudhibiti Sumu Kuvu (TANIPAC) imeendelea na ujenzi wa Kituo cha udhibiti wa visumbufu kibaolojia ambao hadi sasa umefikia asilimia 65 na utagharimu Shilingi Bilioni **3.82** hadi kukamilika.

**d. Zana za Kilimo**

49. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha matumizi bora ya zana za kilimo, Wizara imeingia mkataba wa kuanzisha Vituo Jumuishi vya Utoaji wa Huduma za zana za kilimo nchini (*mechanization hubs*) na kampuni ya AFTRADE. Tathmini ya maeneo yanayofaa kuanzisha vituo hivyo imebaini vituo 13 vimekidhi vigezo na taratibu za kuiwezesha Kampuni hiyo kuanza kazi zinaendelea.

**1.1.3 Huduma na Mafunzo ya Ugani**

50. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imewezesha uanzishwaji wa mashamba darasa 695 kati ya hayo alizeti 378 na pamba 317. Vilevile, imeanzisha mashamba ya mfano 672 kati ya hayo alizeti 415 na pamba 257 katika mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu. Pia, maafisa ugani wa maeneo hayo wamepatiwa tani 10.5 za mbolea, viuatilifu (*ekapack*) 1,617 na viuagugu (*ekapack*) 1,584. Serikali imechukua hatua hiyo, ili kurahisisha utoaji wa mafunzo ya kilimo bora cha alizeti na pamba kwa vitendo.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kukarabati miundombinu ya Vyuo 12 vya Mafunzo ya Kilimo nchini ambapo ukarabati wa miundombinu iliyopangwa katika vyuo sita (6) umefika wastani wa asilimia 95 na vyuo sita (6) vimefikia wastani wa asilimia 40.

52. Aidha, mafanikio mengine katika kuimarisha huduma za ugani ni kama nilivyoeleza kwenye mafanikio ya mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita.

**1.1.4 Umwagiliaji**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na ujenzi wa skimu sita (6) zenye ukubwa wa jumla ya hekta 9,349 katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Tabora, Mbeya na Manyara ambapo Shilingi Bilioni **12.06** zitatumika hadi kukamilika. Aidha, ukarabati wa skimu nane (8) zenye jumla ya hekta 3,711 katika mikoa ya Tanga, Dodoma, Iringa, Katavi na Rukwa unaendelea ambapo jumla ya Shilingi milioni **917.5** zitatumika hadi kukamilika.

54. Aidha, taratibu za manunuzi zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa skimu nane (8) zenye jumla ya hekta 5,930 zilizopo katika mikoa ya Katavi, Ruvuma, Morogoro, Iringa, Simiyu, Mbeya na Tabora. Jumla ya Shilingi Bilioni **3.7** zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa skimu hizo hadi kukamilika.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika katika skimu nne (4) na unaendelea katika skimu 23 zilizopo katika mikoa ya Iringa, Tabora, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Dodoma, Mtwara, Manyara, Singida, Geita na Mwanza. Ujenzi wa skimu hizo utafanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023. Jumla ya Shilingi Bilioni **1.48** zitatumika kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**1.1.5 Masoko na Mifumo ya Masoko**

56. ***Mheshimiwa Spika***, katika kufungua masoko mapya ya mazao, Wizara imeshiriki kwenye maonesho ya Dubai Expo 2020 yaliyofanyika Dubai- Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Mafanikio yaliyopatikana ni kusainiwa kwa hati saba (7) za makubaliano kwa ajili ya kushirikiana katika kuendeleza sekta ya kilimo. Mashirikiano hayo yamejikita katika ujenzi wa vituo vya kuchanganya mbolea na viuatilifu ( *fertilizer and pesticide blending facility/ies* ), upatikanaji na matumizi bora ya zana za kilimo, miundombinu ya umwagiliaji, uhifadhi na usafirishaji mazao.

57. Mafanikio mengine ni ushirikiano katika kupoka na kuhodhi masoko ya mazao ya kilimo ambapo tarehe 03 Mei, 2022 shehena la kontena lenye tani 22.3 za parachichi aina ya HASS lilipokelewa Mumbai India ikiwa ni matokeo ya mkataba uliosaniwa kati ya *Tanzania Horticulture Association* (TAHA) na India.

58. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, tani 6,794 za singa zenye thamani ya Shilingi Bilioni **21.8** na bidhaa mbalimbali za mkonge tani 711 zenye thamani ya Shilingi Bilioni **2.14** zimeuzwa kwenye soko la ndani.

59. Aidha, tani 20,606.64 za singa zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni **33.77** na tani 866 za bidhaa mbalimbali za mkonge zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni **2.46** zimeuzwa kwenye soko la nje. Vilevile, tani 73,028 za kahawa zenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani Milioni **142.26** zimeuzwa kwenye soko la nje.

60. Kadhalika, tani 53,594.35 za soya zimeuzwa katika nchi za India, China, Rwanda na Kenya ikilinganishwa na tani 2,647 zilizouzwa msimu wa 2019/2020. Pia, tani 231,103 za korosho ghafi; tani 144,405 za pamba; tani 60,819 za kahawa; na tani 6,875 za kakao zimeuzwa kwenye soko la nje.

**1.1.6 Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Kilimo**

61. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuthamini mchango wa sekta binafsi kama kichocheo cha ukuaji wa Sekta ya Kilimo, usalama wa chakula, uongezaji wa thamani, kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, kuongeza ajira na uhakika wa masoko ya mazao ya kilimo. Taarifa ya Utekelezaji wa ASDP II kupitia sekta binafsi inaonesha kuwa kampuni 606 za sekta binafsi, Asasi za Kiraia 47 na Mashirika yasiyo ya Kiserikali 64 yamewekeza katika kilimo.

62. Aidha, Wizara imeratibu majukwaa 52 ya majadiliano na Sekta Binafsi kwa mazao ya asilia ya biashara, nafaka, mikunde, bustani na mbegu za mafuta ya kula kwa ajili ya kutatua changamoto za kikodi na kisera.

**1.1.7 Wabia wa Maendeleo**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha mahusiano ya kimataifa kupitia wabia wa maendeleo ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kukuza uchumi kutokana na uwekezaji katika Sekta ya Kilimo. Hadi Juni, 2021 jumla ya Shilingi Trilioni **30.7** zimetumiwa na wabia wa maendeleo katika utekelezaji wa miradi 199 ya Sekta ya Kilimo. Maeneo yaliyozingatiwa ni pamoja na masuala ya vijana katika kilimo, masoko, mbegu, afya ya mimea, uhifadhi wa mazingira, lishe, huduma za ugani, utafiti, uhifadhi wa mazao, mitambo, uimarishaji wa miundombinu ya umwagiliaji na uhifadhi na kuongeza thamani.

**1.1.8 Taasisi za Fedha na Upatikanaji wa Mitaji**

64. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi za Fedha zimeendelea kuwa muhimu katika upatikanaji wa mitaji kwenye Sekta ya Kilimo. Taarifa ya utekelezaji wa ASDP II hadi Juni, 2021 inaonesha kuwa Taasisi za Fedha ikiwemo Benki ya CRDB, NMB, TADB na TIB zilitoa mikopo ya Shilingi trilioni **1.26** katika kuendeleza Sekta ya Kilimo.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi iliunda kamati ya viongozi ya kushughulikia mifumo ya ugharamiaji wa Sekta ya Kilimo ikiwemo kupunguza riba ya mikopo. Kupitia kamati hiyo, Wizara imefanya majadiliano na Benki za biashara na kuwezesha wakulima kupata mikopo. **Mfano,** TADB imetoa jumla ya mikopo ya thamani ya Shilingi Bilioni **116.36** kwa ajili ya pembejeo za kilimo kwa mazao ya kahawa na kufufua vinu vya kuchambua pamba vya Kahama, Chato, Mbongwe, Bukombe, Lugeye, Manawa, Sola na kiwanda cha mafuta ya chikichi cha Trolle Meesle Tanzania Ltd kilichopo mkoa wa Kigoma.

66. Vilevile, TADB kupitia Mfuko wake wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (*Smallholder Credit Guarantee Scheme*) imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni **144** kwa wakulima 987 pamoja na wadau wengine wa kilimo hususan AMCOS na wajasiriamali wadogo na wa kati katika Sekta ya kilimo.

**1.1.9 Uzalishaji wa Mazao**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Kilimo inahusika na uzalishaji wa mazao zaidi ya 90 katika kanda saba (7) za kilimo. Mazao hayo yanajumuisha mazao ya asilia ya biashara, mazao ya mafuta, mazao ya chakula na mazao ya bustani.

68. Katika mwaka 2021/2022 uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ya tumbaku, pamba, kahawa, chai, pareto, sukari, korosho na mkonge umeongezeka kutoka tani 898,966.8 hadi tani 938,586.81 na uzalishaji bado unaendela kwa mazao ya chai, pareto na mkonge (**Jedwali Na. 15. Ukurasa namba 91 wa kitabu cha hotuba yangu**).

69. Aidha, uzalishaji wa mazao ya chakula yanayojumuisha mahindi, mpunga, mtama, uwele, mikunde, ngano, ndizi, mihogo na viazi umeongezeka kutoka tani milioni 18.19 mwaka 2020 hadi tani milioni 18.66 mwaka 2021 ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 2.6 (**Jedwali Na.16. ukurasa namba 99 wa kitabu cha hotuba yangu).**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mazao ya bustani, uzalishaji umefikia tani milioni 7.3 ikilinganishwa na tani milioni 7.56 mwaka 2020/2021, sawa na upungufu wa asilima 3.4 (**Jedwali Na. 18 ukurasa namba 107 wa kitabu cha hotuba yangu**). Upungufu huo umesababishwa na athari za Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO 19) uliopelekea usafirishaji wa mazao hayo nje ya nchi kuathirika.

**Sukari, Ngano na Mafuta ya Kula**

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza malengo ya Serikali ya kuondoa utegemezi wa mazao na bidhaa za kilimo zenye uhitaji mkubwa ambazo huagizwa nje ya nchi kama vile mafuta ya kula, ngano na sukari. Katika mwaka 2021/2022, Wizara imesambaza kwa wakulima tani 2,000 za mbegu za alizeti kwa ruzuku ya Shilingi Bilioni **5.84**. Mbegu hizo zimesambazwa katika mikoa ya Dodoma, Singida, Simiyu na Manyara kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula.

72. Aidha, mbegu hizo zitatoa mavuno ya mbegu za alizeti ya kukamua tani 400,000 ambazo zitazalisha mafuta ya kula tani 100,000. Sambamba na zao la alizeti, Wizara imeendelea kutekeleza mpango wa muda mrefu wa kuzalisha miche bora ya chikichi na kuigawa bure kwa wakulima ambapo jumla ya miche 896,029 imesambazwa katika mikoa ya Kigoma, Mbeya, Mtwara, Kagera, Tanga na Katavi.

73. Vilevile, hadi Aprili, 2022 wakulima 7,588 wa zao la alizeti wameingia mikataba na kampuni mbalimbali ili kuzalisha tani 28,000 ambazo watawauzia kwa bei kati ya Shilingi 750 na 900 kwa kilo.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, uzalishaji wa ngano umefikia tani 70,288 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 1 za ngano kwa mwaka. Uzalishaji mdogo wa ngano unatokana na tija ndogo; uhaba wa mbegu bora zenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya soko; na mabadiliko ya tabianchi. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imetenga Shilingi milioni **750** kwa ajili ya utafiti na uzalishaji wa mbegu za ngano.

75. Aidha, imetathmini na kuainisha aina sita (6) za mbegu zinazohitajika na wanunuzi ambazo ni Lumbesa, Mbayuwayu, Chiriku, Sifa, Kariege na Riziki C1. Mbegu hizo, zitatumiwa na wakulima kuzalisha ngano kwa kuingia mikataba na wanunuzi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiagiza ngano nje ya nchi.

76. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuongeza uzalishaji wa sukari ili kufikia lengo la kuzalisha tani 700,000 ifikapo 2025. Hadi Aprili, 2022 uzalishaji wa sukari umefikia tani 370,000 sawa na asilimia 94 ya lengo la kuzalisha tani 375,000 kwa mwaka 2021/2022.

77. Vilevile, Wizara imeendelea kushirikiana na wazalishaji wa sukari ili kutekeleza mpango wa kuongeza uzalishaji katika viwanda vya Kilombero, Kagera, Mtibwa na TPC kwa kupanua mashamba, kusimika mitambo mipya ya kuchakata miwa na kuongeza tija na kujenga miundombinu ya umwagiliaji. Hatua hizo, zinalenga kuongeza uzalishaji wa sukari kufikia jumla ya tani 635,012 mwaka 2025.

78. Sambamba na miradi iliyopo, Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania inasimamia utekelezaji wa miradi mipya ya Bagamoyo na Mkulazi II. Ujenzi na usimikaji wa kiwanda cha sukari Bagamoyo umefikia asilimia 90 ambapo uzalishaji utaanza Juni, 2022. Kiwanda hicho kitazalisha tani 35,000 kwa mwaka. Aidha, ujenzi wa msingi wa kiwanda cha Mkulazi II umefikia asilimia 30 na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka.

79. ***Mheshimiwa Spika***, miradi mipya iliyopo katika Wilaya ya Kasulu (Kigoma) kupitia kampuni ya Rai Group unaotarajiwa kuzalisha tani 250,000 na mradi wa Rufiji (Pwani) wa Kampuni ya Lake Agro Ltd unaotarajiwa kuzalisha tani 30,000 ipo katika hatua za awali za kumilikishwa ardhi ya uwekezaji wa viwanda vya sukari.

80. Kadhalika, Bodi ya Sukari Tanzania imeingia makubaliano na TEMDO kujenga mtambo wa kuchemsha mbegu pamoja na kubuni kiwanda kidogo cha sukari chenye uwezo wa kuchakata tani 10 za miwa kwa saa.

**1.1.10 Uanzishaji wa Mashamba makubwa ya Kilimo**

81. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, katika mataifa mbalimbali duniani, Wizara imepokea wawekezaji wenye nia ya kuwekeza kwenye mashamba makubwa yatakayo wahusisha wakulima katika mazao ya alizeti, ngano, mpunga, mahindi ya njano, soya, chikichi, zabibu na miwa.

82. Ili kufanikisha uwekezaji huo Wizara imetambua hekta 178,000 kwa ajili ya uanzishaji wa mashamba makubwa katika mikoa tisa (9). Vilevile, Wizara inaendelea kushirikiana na uongozi wa mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa, Pwani, Kigoma, Tabora, Dodoma na Katavi ili kutambua maeneo yanayofaa kwa uwekezaji wa mashamba makubwa kwa ajili ya uzalishaji wa mazao hayo.

**1.1.11 Kuimarisha Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo**

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao nchini, Wizara imekarabati ghala tisa (9) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 3,000 katika Mkoa wa Ruvuma ambapo ukarabati umefikia asilimia 62.5. Wizara kupitia CPB imekamilisha ukarabati wa ghala za Kiteto (tani 1,000), Mbugani – Dodoma (tani 30,000) na vihenge Mkoani Arusha (tani 38,000) ambapo jumla ya Shilingi Milioni **700** zimetumika kukamilisha ukarabati wa ghala na vihenge hivyo.

84. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani imekarabati ghala tisa (9) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,700 na kujenga ghala moja (1) lenye uwezo wa kuhifadhi tani 500 katika mikoa ya Dodoma na Kigoma.

85. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi unaotekelezwa na NFRA, Wizara imeendelea na ujenzi wa vihenge ambao umefikia asilimia 90.64 na ujenzi wa ghala na miundombinu mingine ambao umefikia asilimia 66.5 na Dola za Marekani Milioni **55** zitatumika hadi kukamilika. Mradi huo ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 250,000. Aidha, ujenzi wa ghala 14 kupitia mradi wa TANIPAC umefikia wastani wa asilimia 60. Ghala hizo zikikamilika zitahifadhi tani 21,500. Jumla ya Shilingi Bilioni **14.4** zitatumika kujenga ghala hizo. **(Jedwali Na. 19 ukurasa namba 112 wa kitabu cha hotuba yangu).**

**1.1.12 Uongezaji Thamani wa Mazao ya Kilimo**

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia CPB imeongeza thamani ya mazao ya nafaka tani 4,089.96. Kati ya hizo mahindi ni tani 2,990.26 ambazo zimezalisha unga tani 2,242.65 na pumba tani 747.565 na alizeti ni tani 1,099.70 ambazo zimezalisha mafuta lita 307.916

**1.1.13 Maendeleo ya Ushirika**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeratibu uuzaji wa tani 597,298.58 za mazao zenye thamani ya Shilingi Trilioni **1.55** kupitia vyama vya ushirika kwa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala **(Jedwali Na. 20 ukurasa namba 115 wa kitabu cha hotuba yangu).**

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Tume imeratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ambayo itamilikiwa na Vyama vya Ushirika kwa asilimia 51 na taasisi na watu binafsi watamiliki asilimia 49. Lengo la kuanzishwa Benki hiyo ni kurahisisha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima. **Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji yanapatikana kuanzia ukurasa namba 29 hadi ukurasa namba 130 wa kitabu cha hotuba yangu.**

**4. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

89. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Kilimo inawasilisha bajeti mbele yako wakati dunia inaendelea kupitia changamoto kubwa mbili, vita kati ya Ukraine na Urusi pamoja na athari UVIKO-19. Changamoto hizo zimeleta mabadiliko ya mifumo ya ugavi duniani na gharama za usafirishaji za bidhaa na huduma kimataifa katika uchumi wa dunia na kwa kipekee mifumo ya uzalishaji na usambazaji wa mbolea duniani na biashara ya mazao ya kilimo.

90. Kufuatia hali hiyo, bei ya mbolea imepanda kwa wastani wa zaidi ya asilimia 100. mfano, DAP imepanda kwa Dola za Marekani 396 kwa tani mwaka 2019 hadi Dola za Marekani 948 kwa tani mwaka 2022, Urea kutoka Dola za Marekani 249 kwa tani hadi Dola za Marekani 723 kwa tani, CAN imepanda kutoka Dola za Marekani 210 kwa tani hadi Dola za Marekani 520 kwa tani na SA kutoka Dola za Marekani 128 kwa tani hadi Dola za Marekani 403 kwa tani.

91. Bei ya mafuta ya kula katika soko la dunia imepanda kutoka Dola za Marekani 1,631 Machi, 2021 hadi Dola za Marekani 2,250 Machi, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 38. Aidha, bei ya ngano imepanda kutoka Dola za Marekani 178.24 kwa tani mwaka 2020 hadi Dola za Marekani 294.03 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 65.

92. Hali hiyo, imesababisha nchi kukabiliwa na mfumuko wa bei unaoingia (*Imported inflation*) kutokana na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi hali inayoathiri ustawi wa wananchi. Aidha, athari za UVIKO-19 na mgogoro unaoendelea kati ya Ukraine na Urusi kutokana na tafiti mbalimbali za kimataifa utaathiri mifumo ya uzalishaji na usambazaji wa bidhaa mbalimbali hadi kufikia mwaka 2025.

93. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti ya Wizara katika mwaka 2022/2023 unalenga kujenga msingi imara wa muda mrefu wa ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa kiwango cha asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 pamoja na kujenga msingi wa kukabiliana na athari za majanga ya kiuchumi na kijamii ikiwemo UVIKO-19 na vita ya Ukraine na Urusi, kulinda sekta na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Wizara inachukua hatua hizo kwa kuzingatia kuwa Sekta ya Kilimo (mazao) ni mwajiri mkuu wa nguvukazi ya Taifa na mchangiaji mkuu wa Pato la Taifa.

94. ***Mheshimiwa Spika***, kiwango cha ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 kitachangia katika kupunguza umasikini kwa asilimia 50. Azma hiyo, itaongozwa na Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/2022 – 2025/2026); Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013; Mwongozo na Mpango wa Bajeti wa mwaka 2022/2023; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020-2025; na Hotuba ya Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipolihutubia Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021.

95. Aidha, mpango umezingatia Malengo Endelevu ya Maendeleo 2030 (SDGs); masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, vijana, kutokomeza ajira kwa watoto katika Sekta ya Kilimo, VVU na UKIMWI.

96. ***Mheshimiwa Spika***, ili kufikia lengo la ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa asilimia 10 ifikapo 2030, Bajeti ya mwaka 2022/2023 ni msingi muhimu kufikia lengo kuu hilo. Aidha, ili kufikia lengo hilo Wizara imejiwekea malengo yafuatayo:

- i. Kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula ndani ya nchi na kuuza nje ya nchi. Pia kufanya mwelekeo wa uzalishaji wa mazao ya chakula kuwa wa kibiashara;
- ii. Thamani ya mauzo ya mazao nje ya nchi kuongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 1.2 hadi Dola za Marekani Bilioni 5 ifikapo mwaka 2030;
- iii. Kuongeza idadi ya mashamba makubwa (Block farms/Commercial farms) kutoka 110 mwaka 2020 hadi 10,000 mwaka 2030;
- iv. Kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta 8,500,000 sawa na asilimia 50 ya eneo lote linalolimwa nchini ifikapo 2030 ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kupitia kilimo cha umwagiliaji kutoka asilimia 10 hadi asilimia 50;
- v. Kutengeneza ajira za vijana na wanawake katika sekta ya kilimo zitakazofikia milioni 3 ifikapo mwaka 2025;
- vi. Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda vya kuongeza thamani ya mazao na bidhaa za kilimo kufikia asilimia 100 ifikapo 2030;
- vii. Kuongeza upatikanaji wa mitaji na mikopo kutoka kwenye Sekta ya Fedha kutoka asilimia tisa (9) mwaka 2022 hadi asilimia 30 ifikapo mwaka 2030;
- viii. Kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna kutoka asilimia 35 hadi asilimia tano (5) ifikapo mwaka 2030;
- ix. Kuondoa upungufu wa mafuta ya kula na kulifanya zao la alizeti kuwa moja ya mazao yatakayozalishwa kutosheleza mahitaji ya ndani na mauzo nje ya nchi. Vilevile, kuwekeza katika mashamba makubwa ya chikichi na kuondoa mfumo wa kilimo cha chikichi kwa mashamba madogo chini ya ekari moja (1);
- x. Kuongeza mauzo ya Mazao ya Bustani (Horticulture) kutoka Dola za Marekani Milioni 750 kwa mwaka kufikia Dola za Marekani Bilioni 2 mwaka 2030;
- xi. Kujitosheleza kwa uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi na kuvipa vipaumbele viwanda vya ndani vya mbolea na matumizi ya chokaa ili kupunguza gharama za uzalishaji; na
- xii. Kujitosheleza kwa mahitaji ya mbegu bora na kuuza mbegu nje ya nchi kupitia ushirikishaji wa Sekta Binafsi.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji wa malengo hayo siyo ya muda mfupi, bali yanajenga msingi wa kuwa na matokeo yatakayohakikisha mwendelezo wa ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa muda mrefu, ukuaji wa Pato la Taifa, ajira, mapato ya fedha za kigeni, malighafi za viwanda na kujihakikishia usalama wa chakula nchini na kuuza ziada nje ya nchi.

98. Takwimu zinaonesha kuwa ifikapo mwaka 2050, idadi ya watu duniani itafikia Bilioni 9.7 na Bilioni 8.5 ifikapo mwaka 2030. Afrika itafikia Bilioni 2.4 mwaka 2050 na Bilioni 1.6 mwaka 2030. Vilevile, ifikapo mwaka 2050, Tanzania itakuwa na idadi ya watu milioni 135 na milioni 79 mwaka 2030 ambapo mahitaji ya chakula nchini yatafikia tani Milioni 18.8. Wakati huo huo mahitaji ya chakula Duniani yataongezeka kwa wastani wa asilimia 50. (FAO, 2018).

99. Athari za mazingira zitashusha uzalishaji wa mashambani kwa asilimia nne (4). Hii ni fursa kwa atakayejiandaa na ni majanga kwa ambaye hatajiandaa hivyo matumizi ya teknolojia na uwekezaji kwenye tekenolojia ndiyo mwarobaini pekee utakaotatua hatari hii.

100. Aidha, biashara ya chakula katika soko la Afrika itafikia Dola za Marekani Trilioni 1 ifikapo mwaka 2030 hii itafungua fursa za ajira kwenye mnyororo wa thamani. Kutokana na ongezeko hilo la idadi ya watu duniani, kama Taifa lazima tujiandae sasa, ili kufaidika na fursa hiyo ya kibiashara na kujihakikishia usalama wa chakula na ukuaji endelevu wa uchumi wetu na kulifanya Taifa kuwa huru.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara imepanga kutekeleza maeneo ya kipaumbele yafuatayo ili kufikia malengo tajwa:-

- i. Kuimarisha utafiti,
- ii. Kutoa ruzuku ya mbegu za alizeti, ngano na miche ya chikichi,
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo,
- iv. Kuimarisha na kutoa huduma ya upimaji wa afya ya udongo ili kuwezesha wakulima kutambua aina na kiwango cha mbolea kinachohitajika katika mashamba yao;
- v. Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo ujenzi wa mabwawa ya kuvunia maji ya mvua;
- vi. Kuimarisha huduma za ugani na kuhamasisha kilimo cha ukanda kutokana na Ikolojia za kilimo (Tanzania Agricultural Growth Corridor);
- vii. Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo;
- viii. Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa Mitaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo utakaowezesha upatikanaji wa pembejeo kwa mfumo wa ruzuku pindi inapotokea athari za kiuchumi;
- ix. Kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ghala katika ngazi ya Kijiji, Kata na Tarafa ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna kutoka asilimia 35 hadi 5 ifikapo mwaka 2030;
- x. Kuhamasisha Kilimo cha Mashamba makubwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha maeneo maalum ya mashamba makubwa, kwa kuyatengenezea miundombinu na kuwapatia wananchi kwa makubaliano maalum hususan

kwa zao la chikichi;
xi. Kuanza kutoa ruzuku ya mbolea mwaka 2022/2023;
xii. Kuimarisha Kilimo Anga, na
xiii. Kuimarisha maendeleo ya ushirika.

**4.1. Kuimarisha Utafiti**

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, mahitaji yetu kama nchi ya mbegu bora ni tani 652,250 na sasa tunazalisha tani 35,199. Ili kuondoa tatizo hilo, Wizara imeongeza bajeti ya utafiti na uzalishaji wa mbegu za msingi kutoka **Shilingi Bilioni 11.63** mwaka 2021/2022 hadi **Shilingi Bilioni 40.73** mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 250.

**103.** Hatua hiyo itawezesha upatikanaji wa mbegu za awali na za msingi kutoka tani 226.5 zinazozalishwa sasa hadi tani 1,453 ambazo zitakazokidhi mahitaji ya kuzalisha mbegu bora tani 452,650 zitakazosambazwa kwa wakulima na kufanya kufikia lengo kwa asilimia 69.4 ifikapo 2025.

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, sehemu ya Bajeti ya utafiti ya mwaka 2022/2023 itatumika kuanza safari kama Taifa ya kulinda, kusafisha na kuzalisha mbegu zetu za asili kupitia Taasisi yetu ya Serikali – ASA na ifikapo mwaka 2025, mbegu zetu za asili zitapatikana madukani kama ambavyo mbegu zilizoboreshwa zinavyouzwa madukani.

**4.2. Kuimarisha Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo**

**Mbegu bora**

**105.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imedhamiria kuhakikisha inajitosheleza kwa mahitaji ya mbegu hususan kwa mazao ya mahindi, alizeti, soya, ufuta, ngano, maharage, kunde, mpunga, mtama, choroko, dengu, shayiri na karanga. Kwa mwaka 2022/2023, jumla ya **Shilingi Bilioni 43.03** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha ASA kuzalisha tani 127,650 za mbegu bora kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. **Jedwali Na. 22. Uk. 144 wa kitabu cha Hotuba yangu.**

**Mbolea**

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto ya athari za kupanda kwa bei ya mbolea duniani, ambapo hali hiyo inatazamiwa kuendelea hadi mwaka 2023/2024 na katika kulinda uzalishaji wetu na kuwalinda wakulima wa Tanzania, Wizara inatarajia kutumia Shilingi Bilioni 150 kutoa ruzuku ya mbolea kwa mazao yote kwa utaratibu utakaoelezwa wakati wa kuwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali. Ruzuku hiyo haitakuwa ya kudumu bali itatolewa kwa kipindi maalum kulingana na mahitaji ya nyakati. Aidha, utaratibu wa kutoa ruzuku kwa wakulima kupitia mfumo wa mazao kujigharamia yenyewe (*own crop financing*) utaendelea kutekelezwa.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni kheri Wizara ya Kilimo isifanye jambo lolote kwa mwaka 2022/2023 bali wakulima wa Tanzania wapate ruzuku ya mbolea itakayowafanya wazalishe, walinde nchi yetu, walinde ukuaji wa uchumi, walinde mapato yetu ya nje (*export earnings*) na kulilinda Pato la Taifa.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu ninaagiza kampuni na viwanda vya mbolea nchini kusajili mawakala wao TFRA ifikapo tarehe 31 Mei, 2022 ili kurahisisha utoaji na usimamizi wa ruzuku. Katika kuimarisha usimamizi wa utoaji wa ruzuku, mifuko ya mbolea itawekwa misimbomilia (*bar codes*) na lebo ya **RUZUKU** ili kutofautisha na mbolea zitakazoendelea kuuzwa sokoni bila ruzuku.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** kampuni yoyote ambayo haitatekeleza agizo hili na kukubali kutumia mfumo utakaowekwa na TFRA wa kusimamia na kusajili kampuni, mawakala na kuweka mfumo wa *Point of Sale* (POS) kwenye maduka na ghala zao za mikoani na wilayani, Serikali haitosita kumfutia leseni yake ya biashara. Mpango huu wa ruzuku ya mbolea utawapa kipaumbele wazalishaji wa mbolea ndani ya nchi ili kulinda viwanda vyetu, ajira na usalama wa nchi.

**110.** Wizara itaendelea kuwalinda na kuwawezesha wawekezaji katika viwanda vya ndani vya kuzalisha mbolea ikiwemo kiwanda cha ITRACOM chenye uwezo wa kuzalisha tani 600,000 za mbolea kwa mwaka. Vilevile, kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi nyingine za Serikali itawezesha upatikanaji wa vivutio vya uwekezaji wa kiwanda cha mbolea Minjingu ili kiweze kuongeza uwezo wa kuzalisha mbolea kutoka tani 100,000 kwa mwaka hadi tani 300,000 kwa mwaka.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na mazungumzo na Wizara ya Nishati kuhusu kufufua mradi wa kuzalisha mbolea ya Urea kwa kutumia gesi asilia. Vilevile, itaiwezesha Kampuni ya TFC ya Serikali **Shilingi Bilioni 6** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kama mtaji na itapitia upya muundo wake kwa lengo la kuiwezesha kampuni hiyo kujiendesha kibiashara na kutumika kama chombo cha Serikali cha kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo hususan mbolea na viuatilifu.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuwahakikisha wazalishaji wadogo wa mbolea za kilimo hai (*organic*) na chokaa kuwa itaendelea kuwalea, kuwalinda na kuwahakikisha masoko ili kupunguza gharama za kuagiza mbolea za aina hiyo kutoka nje ya nchi.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu, tunawahamasisha vijana wabunifu ambao wanaweza kuzalisha mbolea za kilimo hai (*organic*) waje Wizara ya Kilimo ili waweze kusaidiwa.

**Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo**

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itakamilisha utaratibu wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo. Mfuko huo utatumika kutoa ruzuku ya pembejeo; kuwezesha uhimilivu wa bei za mazao (*stabilization fund*) kutokana na athari za majanga, mdororo wa uchumi; na kugharamia uwekezaji katika miundombinu ya uzalishaji, uongezaji wa thamani na uhifadhi wa mazao ya kilimo**.**

**4.3. Kuimarisha Umwagiliaji**

**115.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kujenga mabwawa 14 yenye uwezo wa mita za ujazo milioni 131.5 na kujenga skimu mpya 25 zenye jumla ya hekta 53,234 katika mikoa 14. Vilevile, Tume itaboresha, itakarabati na kukamilisha skimu 30 zenye jumla ya hekta 41,771 katika Mikoa 10. Katika kutekeleza mpango huo, jumla ya **Shilingi Bilioni 256.2** zitatumika. Mpango huo utaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 95,005 kutoka hekta 727,280.6 mwaka 2021/2022 hadi hekta 822,285.6 sawa na asilimia 68.5 ya lengo la hekta milioni 1.2 ifikapo 2025 kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

**116.** Ongezeko hilo litaongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo, kama mpunga kwa tani 403,020 zenye thamani ya takriban **Shilingi bilioni 345.4** na vitunguu kwa tani 374,426 zenye thamani ya takriban **Shilingi bilioni 2.9** na hivyo kuongeza Pato la Taifa. Vilevile, uwekezaji huo unakadiriwa kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 475,000.

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, Tume pia itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu 42 zenye ukubwa wa hekta 91,357 katika Mikoa ya Katavi, Iringa, Mbeya, Rukwa, Songwe, Dodoma, Kagera, Mwanza, Pwani, Kigoma, Tabora, Geita, Singida, Arusha, Morogoro, Manyara, Njombe na Mtwara zitakazojengwa mwaka 2023/2024.

**118.** Vilevile, itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabonde ya kimkakati 13 yenye jumla ya hekta 272,617 ambayo ni bonde la mto Kilombero (53,000), Ifakara (4,000), Ruvuma (26,066), Ruhuhu (3,700), Rufiji (64,896), Ziwa Viktoria (20,470), Mto Suguti (4,800), Makondeko (9,000), mto Lukuledi (4,680) Malagarasi (7,000), Kasinde (15,000), Songwe (3,005) na skimu nane (8) za kimkakati zenye jumla ya hekta 30,900 za Bugwema (Musoma), Mtambo (Hai), skimu za Mto Umba (Lushoto/Mkinga) skimu za Mkomazi (Korogwe), skimu ya Bonde la Kiru (Babati), skimu za Ngomai/Kibaigwa (Kongwa), skimu ya Gereza la Kalilankulukulu (Tanganyika) na Litumbandyosi (Mbinga). Ujenzi wa skimu na mabonde ya kimkakati utafanyika katika kipindi cha mwaka 2022/2023 na 2024/2025.

**119.** Pia, Tume itanunua mitambo 12 kwa ajili ya ujenzi wa skimu; itanunua vifaa vya upimaji (*land survey equipment*); itanunua magari 38 kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa miradi kupitia Ofisi za Umwagiliaji za Mikoa; na itajenga Ofisi 17 za Umwagiliaji za Mikoa. Jumla ya **Shilingi Bilioni 59.6** zitatumika kutekeleza mpango huo.

**120.** Wizara itafungua Ofisi 146 za Umwagiliaji za Wilaya ambazo zitakuwa na Wahandisi wa umwagiliaji, Mafundi Sanifu Ujenzi na Maafisa Kilimo. Watumishi hao kwa kushirikiana na watumishi waliopo Ofisi ya Rais - TAMISEMI watasimamia miradi ya umwagiliaji katika Wilaya zao na kusimamia ukusanyaji wa ada za huduma za umwagiliaji.

**121.** Aidha, watumishi hao watakuwa chini ya Ofisi za Tume ya Umwagiliaji na kuwajibika moja kwa moja kwa Wizara ya Kilimo. Mfumo huo wa usimamizi wa miradi ya umwagiliaji utawezesha kuokoa upotevu wa mapato ya takriban **Shilingi Bilioni 100** kwa mwaka kutoka katika skimu za umwagiliaji.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, Kwenye eneo hilo la umwagiliaji, Wizara imeongeza bajeti kutoka Shilingi Bilioni 46.5 hadi Shilingi Bilioni 361.5 ambalo ni ongezeko la asilimia 677. Uwekezaji huu matarajio yake ni kuongeza mtandao wa umwagiliaji kwa hekta 95,005, kuwa na ofisi za umwagiliaji za wilaya 146 na magari 38 kwa ajili ya ofisi za umwagiliaji za mkoa pamoja na kutengeneza ajira 475,000.

**4.4. Kuimarisha Huduma za Ugani**

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kuimarisha huduma za Ugani ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao nchini, itawezesha upatikanaji wa huduma ya upimaji wa afya ya udongo kwa wakulima kama huduma ya msingi na ya lazima. Huduma hiyo itaenda sambamba na kusajili wakulima na kuwaweka kwenye Kanzidata maalum. Aidha, kila mkulima atapewa cheti kitakachoonesha afya ya udongo katika shamba lake ili kumwezesha kuzalisha mazao kulingana na afya ya udongo wa shamba lake.

**124.** Ili kufikia azma hiyo, Wizara itanunua na kusambaza vifaa vya kupimia afya ya udongo kwa maafisa ugani wa Halmashauri 122; vishikwambi 6,377; na visanduku vya ugani (*Extension Kits*) 400 katika Halmashauri 46. Vilevile, Wizara itakamilisha ufungaji wa mfumo wa GPS kwa pikipiki zote na kuweka mfumo wa usimamizi wa huduma za ugani na kuwezesha kila afisa ugani anapata sare ambazo atavaa akiwa kazini.

**125.** Aidha, itawezesha uanzishwaji wa mashamba ya mfano 400 na mashamba darasa 400 kwa mazao ya kimkakati na kipaumbele katika Mikoa ya Singida, Simiyu, Morogoro, Njombe, Ruvuma, Kilimanjaro, Manyara, Tabora, Mara, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa na Dodoma.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaanzisha mfumo utakaowawezesha maafisa ugani kuwatambua wakulima bora watakaotumika kutoa huduma za ugani kwa wakulima wengine. Katika kuondokana na tatizo la upungufu wa maafisa ugani, wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya kilimo katika ngazi zote kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara itaanza mfumo wa kuwapeleka katika mafunzo ya vitendo kwa mwaka mmoja kabla ya kuhitimu masomo yao na eneo hili Serikali itashirikiana na Wadau wa Maendeleo.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kulinda ardhi ya kilimo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, itawezesha upimaji wa ardhi ya kilimo na kuitangaza kwenye Gazeti la Serikali na kuilinda.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaanzisha kituo cha huduma za mawasiliano ya kilimo (*Call centre*) kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa ushauri wa kitaalam na taarifa za masoko kwa wadau wa kilimo. Aidha, Wizara itaandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Huduma za Ugani na kuusambaza kwa Sekretarieti za Mikoa 26 na Halmashauri 185.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaanza kukarabati vituo 200 vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (WARCs) ambavyo vitatumika kwa ajili ya shughuli za kilimo. Jumla ya **Shilingi Milioni 400** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati wa vituo hivyo.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kuagiza Halmashauri zote ambazo Vituo vya Rasilimali za Kilimo vilijengwa wakabadilisha matumizi yake kuanzia tarehe 1 Julai, 2022 Wizara itaanza kukarabati na kutumia vituo vyake kwa ajili ya mashamba ya mfano na vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo.

**1.1.1. Mazao ya Mafuta**

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni tani 650,000 kwa mwaka ikilinganishwa na uzalishaji wa ndani ambao ni tani 300,000 na takriban tani 350,000 huagizwa nje ya nchi. Kati ya kiasi kinachozalishwa nchini, tani 270,000 sawa na asilimia 90 kinatokana na zao la alizeti na kiasi kinachobaki kinachangiwa na mazao mengine ikiwemo chikichi, karanga, nazi, pamba na ufuta.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuziba nakisi ya takriban tani 400,000 za mafuta ya kula, tunahitaji kuzalisha tani milioni 1.4 za alizeti. Kwa sasa tunazalisha wastani usiozidi tani 700,000 ambazo zinatupatia mafuta wastani wa tani 270,000. Ili kuzalisha tani milioni 1.4 za alizeti zitakazopelekwa kiwandani kukamuliwa kuziba nakisi ya tani 400,000 za mafuta ya kula tunahitaji tani 9,454.58 za mbegu bora. Kwa maana hiyo, mahitaji yetu ya alizeti ili kukidhi mahitaji ya ndani ni tani milioni 2.3.

**133.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imejiwekea lengo la kuzalisha tani milioni 3 za alizeti ifikapo mwaka 2025 ili kama nchi tuwe na mafuta ya alizeti tani milioni 1, tunahitaji kulima eneo lenye ukubwa wa hekta milioni 2.4. Aidha, eneo hilo la kilimo linahitaji tani 12,000 za mbegu, kwa ajili ya uzalishaji wa tani milioni 1 za mafuta ya alizeti.

**134.** ***Mheshimiwa Spika***, Ili kufikia lengo hilo, Wizara kwa mwaka 2022/2023 inachukua hatua tatu za kimkakati, pamoja na majukumu ya kawaida ya uhamasishaji, Wizara itazalisha na kugawa tani 5,000 za mbegu bora kwa ruzuku Jumla ya Shilingi Bilioni 11 zitatumika kuzalisha mbegu hizo. Katika mwaka 2023/2024, Wizara itagawa tani 10,000 na mwaka 2024/2025 itazalisha na kugawa tani 15,000. Shughuli hiyo ya uzalishaji wa mbegu itafanywa na ASA na kuingia mikataba na Kampuni binafsi kwa ajili ya kuzalisha mbegu na Wizara kuzigawa kwa wakulima kwa ruzuku.

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, hatua ya pili, Wizara inajadiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuweka motisha ya kikodi kwa viwanda vinavyozalisha mafuta ya alizeti nchini kwa kuwaondolea kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Utafiti uliofanywa na Wizara unaonesha kuwa Serikali itapoteza mapato ya kodi ya Jumla ya Shilingi Bilioni 59.3 katika kipindi cha miaka mitatu ambapo kwa mwaka itapoteza kati ya Shilingi Bilioni 20.5 na Bilioni 18.9. Upotevu huo utapungua kila mwaka katika kipindi cha miaka mitatu kwa kuwa viwanda vitaongeza uzalishaji kwani kwa sasa viwanda hivyo vinafanya kazi chini ya asilimia 30 ya uwezo wake.

**136.** Baada ya kipindi cha miaka mitatu, uzalishaji katika viwanda hivyo utafikia asilimia 100 na Serikali itakusanya mapato zaidi kupitia PAYE, kutokana na ongezeko la ajira linalokadiriwa kufikia watu 171,000 kwa mwaka wa kwanza na kukua mpaka watu 717,000 ifikapo 2026/2027. Mapato mengine yatakayoongezeka ni pamoja na kodi ya mapato na ushuru wa mazao. Makusanyo hayo yataongeza mapato ya Serikali hivyo upotevu ulioelezwa hapo awali ni wa muda mfupi. Hali hiyo itafanya viwanda vyetu vinavyochuja mafuta mara mbili (*double refinery*) kuwa shindani na kupunguza ugumu wa maisha kwa watanzania na kuwafanya kuwa na kipato cha ziada (*disposable income*) nakutumia fedha zao kwenye matumizi mengine ya kijamii.

**137.** ***Mheshimiwa Spika***, hatua ya tatu, Wizara imeanza kuvitaka viwanda vinavyochuja mafuta mara mbili (*double refinery*) kununua mafuta ghafi yanayozalishwa na wazalishaji wadogowadogo (*backyard processors*) ambao wengi wao ni wanawake na vijana ambao wanalima alizeti na kuikamua kwa mashine ndogondogo za SIDO na kuyapanga mafuta barabarani.

**138.** ***Mheshimiwa Spika***, mkulima anayelima ekari moja (1) na kukamua mafuta yake na kuuza kwa bei ya leo iliyopo sokoni anapata faida ya Shilingi 1,530,000. Mkulima anayelima ekari moja (1) na kuuza alizeti aliyovuna anapata faida ya Shilingi 420,000 tu. Wizara inaendelea kuhamasisha kutengeneza madaraja mawili ya wasindikaji ambao ni wasindikaji wa awali na wasindikaji wa upili (*Primary* na *secondary processors)*.

**139.** Ili kumlinda mkulima, mzalishaji, muuzaji na mlaji ni lazima kama nchi tuchukue hatua ya kuondoa VAT kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa na viwanda vya *double refinery* ndani ya nchi ili kuijenga sekta ya mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi.

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, zao la alizeti ni kwa ajili ya mkakati wa muda mfupi na kwa ajili ya kujenga msingi wa kuwa nchi inayouza mafuta ya alizeti nje ya nchi. Aidha, katika miaka mitatu ya kwanza, Wizara itahamasisha uwekezaji wa kilimo katika maeneo mapya (*extensive agriculture*) ili kufikia lengo la hekta milioni 2.4 ifikapo 2025. Kadhalika, baada ya mwaka 2025, Wizara itahamasisha uzalishaji wa zao la alizeti kwa kuongeza tija ya zao (*intensive agriculture*). Kwenye eneo hili ugawaji wa mbegu utatumia Shilingi Bilioni 17.5 kama ruzuku.

**141.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa muda mrefu Tanzania tumekuwa tukijitangaza na kujisifia kuwa sisi ni waanzilishi wa zao la chikichi na baadhi ya mataifa yenye uzalishaji mkubwa wa zao hilo yalichukua mbegu kwetu. Ni vyema kufahamu mambo mawili ambayo ni ukweli usiokwepeka; moja, hatukuwahi kufanya uwekezaji wa kutosha kama nchi kwenye eneo la chikichi. Pia mfumo tuliokuwa tunatumia kuendeleza zao hili wa kuamini kuwa mkulima mdogo ataweza kuligharamia na kufanya litosheleze kwa mafuta ya kula haikuwa sahihi, hivyo, ni lazima tubadili namna ambavyo tunawekeza katika zao hili.

**142.** ***Mheshimiwa Spika***, Jambo la pili ni kuwa; ili kuwe na faida kwa mkulima na mchakataji wa mafuta ya chikichi, mashamba lazima yawe katika utaratibu wa mashamba makubwa ya pamoja (*Block farms)*. Ili kuongeza uzalishaji na tija, Wizara katika mwaka 2022/2023 itaanza kutumia utaratibu wa mashamba makubwa ya pamoja kwa kuchukua maeneo makubwa kuanzia hekta 2,000 hadi hekta 8,000, kuyasafisha na kuyawekea miundombinu inayostahili na kupanda miche. Kama eneo hilo litahitaji kulipiwa fidia Serikali itatwaa na kulipia fidia.

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2022/2023, Wizara imejiwekea lengo la kuanza safari ya kuzalisha mafuta ya chikichi tani 500,000 ifikapo mwaka 2030. Ili kufikia lengo hilo tunahitaji eneo la kilimo lenye ukubwa wa hekta 125,000 ambapo tutahitaji miche 15,625,000. Uzalishaji wa miche hiyo utafanywa na TARI, ASA na Sekta Binafsi. Kwa kuanzia, mikoa ambayo ni ya kipaumbele kwa ajili ya mkakati huu ni Kigoma, Katavi, Tabora na Pwani. Wakati Serikali inaendelea na mpango huu, Wizara inakamilisha mazungumzo na Kampuni kubwa mbili za Bakhresa na Wilmar ambao wameonesha nia ya kuwekeza katika mkoa wa Kigoma na Pwani.

**144.** Kwa kuwa suala la mafuta ya kula ni hitaji la kidunia, kupitia Bunge lako Tukufu, tunawakaribisha wawekezaji kuwekeza katika mpango huo. Vilevile, Wizara itafanya mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango ili kutafuta fedha Shilingi Bilioni 40 zitakazotekeleza mpango huo.

**145.** ***Mheshimiwa Spika***, Jambo hili la kuondoa tatizo la mafuta ya kula ni la muda mrefu. Kwa hiyo, ni lazima tukubali kuwekeza kimkakati kwa kuishirikisha Sekta Binafsi. Uwekezaji huo siyo hasara kwa nchi kwani soko la ndani na nje lipo, wakulima wapo na ardhi ya kilimo ipo na Serikali ya Awamu ya Sita ipo tayari kuwekeza.

**1.1.2. Zao la Ngano**

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, mahitaji ya ngano nchini ni tani Milioni 1 kwa mwaka wakati kwa sasa tunazalisha tani 70,288 ambapo tunaingiza tani laki 8 hadi 9 kwa mwaka na kutumia Shilingi Bilioni 500. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imejiwekea lengo la kuzalisha tani milioni 1 ifikapo mwaka 2030.

**147.** Katika mwaka 2022/2023, Wizara inaanza safari ya kuzalisha mbegu tani 7,200 kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. Mbegu hizo zitakazopandwa katika eneo la hekta 60,000 ambazo zitazalisha tani 150,000 za ngano. Wizara itasimamia ufufuaji wa mashamba ya ngano yaliyopo katika mikoa ya Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Njombe, Rukwa, Mbeya na Katavi yenye jumla ya hekta 40,200. Aidha, ufufuaji wa mashamba katika mikoa hiyo, utaenda sambamba na uanzishwaji wa mashamba mapya katika mikoa ya Songwe na Dodoma (Bahi).

**148.** Pia, TARI itatafiti mbegu bora za ngano zenye sifa ya kustahimili maeneo ya joto na baridi, zinazokomaa mapema na zenye kiwango cha gluteni kinachohitajika kwa uokaji. Jumla ya **Shilingi Milioni 400** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utafiti na uzalishaji wa mbegu za ngano.

**149.** Pia natumia fursa hii kukaribisha wadau wa kimataifa (*International Communities)* kushirikiana na Wizara kuzalisha ngano na mafuta ya kula. Hii ni kwa kuzingatia kwamba kwa sasa Tanzania tuko tayari kushirikiana katika kufidia mahitaji ya dunia kwa bidhaa hizo.

**1.1.3. Uzalishaji wa Miwa na Sukari**

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** mahitaji ya sukari nchini ni wastani wa tani 585,000 kwa mwaka, ambapo tani 420,000 ni sukari ya matumizi ya kawaida na tani 165,000 ni kwa ajili ya matumizi ya viwandani. Upungufu wa sukari ya matumizi ya kawaida ni wastani wa tani 50,000.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na upungufu huo, kwa mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Bodi ya Sukari itaongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 372,210 mwaka 2021/2022 hadi tani 450,000 mwaka 2022/2023 kwa kuimarisha udhibiti wa visumbufu, upatikanaji wa maji mashambani na kupunguza upotevu wa miwa kwa kuhakikisha viwanda vinafanya kazi kwa ufanisi. Mipango hiyo itaenda sambamba na kuhamasisha uzalishaji wa sukari ya viwandani.

**152.** Mpango wa muda wa kati ni kufikia tani 700,000 ifikapo 2025. Katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kusimamia upanuzi wa viwanda vya Kilombero, Kagera na Mtibwa vitakavyozalisha jumla ya tani 635,012. Wamiliki wa viwanda watatumia jumla ya Dola za **Marekani Milioni 405.55** kwa ajili ya upanuzi wa viwanda hivyo.

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, miradi mipya iliyo katika hatua za awali za kumilikishwa ardhi ya uwekezaji wa viwanda vya sukari ni ya kampuni ya Rai Group iliyopo Kasulu (Kigoma) unaotarajiwa kuzalisha tani 250,000 na mradi wa Rufiji (Pwani) wa Kampuni ya Lake Agro Ltd, unaotarajiwa kuzalisha tani 30,000.

**154.** Aidha, Bodi itaainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha miwa na uwekezaji wa viwanda vya sukari katika mikoa ya Ruvuma, Katavi, Kigoma, Tabora, Rukwa, Lindi na Mtwara na kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya wakulima wadogo wa Kilombero. Jumla ya **Shilingi Bilioni 1** zimetengwa kufanikisha lengo hilo kwa kuwa uwekezaji mkubwa utafanywa na Sekta Binafsi.

**1.1.4. Mazao ya Bustani**

**155.** ***Mheshimiwa Spika***, mazao ya bustani ni moja ya sekta zinazokua kwa haraka kati ya asilimia 9 hadi 11 ikilinganishwa na sekta ya mazao ambayo ukuaji wake ni kati ya asilimia 4 hadi 5 kwa mwaka. Vilevile, kilimo cha mazao ya bustani hutoa ajira kwa watu takriban milioni 6.5 ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi jumuishi kutokana na kuvutia wanawake na vijana katika tasnia hiyo. Aidha, mazao ya bustani yana mchango mkubwa katika kukabiliana na changamoto za utapiamlo.

**156.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya bustani yakiwemo matunda, mboga, viungo na maua ili kuongeza uzalishaji kutoka tani Milioni 7.3 mwaka 2021 hadi tani Milioni 8.5 mwaka 2022. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itasimamia uzalishaji na matumizi ya miche na vipando bora, kudhibiti visumbufu vya mazao, kutoa mafunzo kwa wakulima, kujenga miundombinu ya kuhifadhi mazao ya bustani, vituo vya huduma za pamoja (*common use facilities*) na vyumba vya ubaridi (*cold rooms*) katika maeneo ya uzalishaji.

**157.** Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itajenga *Common Use facilities* tatu (3) katika mikoa ya Iringa (Mufindi- Nyororo), Dar es salaam (Kurasini – EPZA na Kilimanjaro (Hai). Wizara inakamilisha taratibu za kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji huo. Vituo hivyo vitafanya kazi za kuchambua, kupanga, kufungasha na kusafirisha mazao yakiwa na alama ya "***Produce of Tanzania"***. Jumla ya **Shilingi Bilioni 6.2** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo hivyo.





**158.** ***Mheshimiwa Spika***, Hatua hii ya Serikali ni kulinda zao la parachichi ambalo limekuwa likinunuliwa hapa nchini na shughuli za kufungasha zinafanyika nchi nyingine na zao letu linaondoka bila alama ya Tanzania. Miundombinu hii itajengwa na Serikali na kukabidhiwa Sekta Binafsi kuiendesha na Serikali itaingia mikataba na waendeshaji ili kurudisha gharama za uwekezaji.

**159.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TOSCI itasimamia usajili wa wazalishaji wa miche ya parachichi na kuwapa cheti cha kuwa wazalishaji kwa lengo la kudhibiti ubora na kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani hususan matunda na hivyo kuondoa tatizo la uzalishaji wa miche holela ili kama Taifa tusirudie tatizo lililojitokeza katika mazao kama machungwa, nanasi na embe ambayo tumekuwa tukilaumiwa kuwa hayakidhi mahitaji ya viwanda wala masoko ya kimataifa. Miche hiyo itasambazwa kwa wakulima kwa bei ya ruzuku

**160.** Vilevile, Wizara itatoa mwongozo wa usimamizi na biashara ya zao la parachichi ili kumlinda mkulima na bei ambazo haziakisi bei za soko, mnunuzi na mchakataji. Mwongozo huo utazinduliwa Julai, 2022 na kutoa dira na mwelekeo wa namna bora ambayo biashara ya parachichi itaendeshwa ili kuondoa tatizo la uvunaji wa parachichi ambazo hazijakomaa na kuzipeleka sokoni kwani jambo hilo linahatarisha ustawi wa biashara ya parachichi. Na baada ya mwongozo kutolewa yeyote atakayevuna parachichi ambazo hazijakomaa atachukuliwa hatua za kisheria.

**4.5. Upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo**

**161.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi ambapo itakamilisha ujenzi wa masoko ya kimkakati matano (5) yaliyokuwa chini ya mradi wa DASIP. Masoko hayo yapo katika wilaya za Kahama, Ngara, Kyerwa, Tarime na Karagwe.

**162.** Vilevile, Wizara itaanzisha mnada wa chai eneo la Kurasini Dar es Salaam pamoja na kuanzisha kituo cha huduma za biashara ya mazao ya kilimo kitakachojengewa miundombinu ya uhifadhi. Lengo ni kurahisisha biashara ya mazao ndani na nje ya nchi na kuunganisha na Bandari ya Dar es salaam kwa kuwa na *Green belt* kwani sasa kusafirisha mazao ya kilimo kupitia bandari ya Dar es saalam imekuwa tatizo kubwa linalopelekea Sekta Binafsi kutumia bandari ya Mombasa.

**163.** Aidha, katika kuongeza thamani, kipato kwa mkulima na kupunguza upotevu wa zao la zabibu, Wizara itajenga viwanda vitatu (3) vya kusindika zabibu ghafi ambapo viwanda hivyo vitajenjwa katika Mkoa wa Dodoma. Kwa kuanzia Wizara imetenga kiasi cha shilingi Milioni mia mbili kwa ajili ya uwekezaji huo.

**164.** Vilevile, Wizara itaimarisha mauzo ya mazao ya kilimo kupitia vya Vyama vya Ushirika kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuanza kutekeleza makubaliano kati ya Benki ya NMB na Tume ya Maendeleo ya Ushirika ya kujenga ghala zenye thamani ya Shilingi Bilioni 20 katika mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Mtwara na Kagera, ili kukabiliana na changamoto ya ghala kwenye mazao ya korosho, pamba na kahawa.

**165.** Wizara kupitia mradi wa TANIPAC itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Udhibiti wa Visumbufu Kibaolojia (Kibaha) kwa ajili kuimarisha utafiti na uzalishaji wa wadudu rafiki ili kudhibiti visumbufu vya mazao. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa Kituo Mahiri (Kongwa) ambacho kitatumika kusambaza teknolojia za uhifadhi na usindikaji wa mazao ya chakula pamoja na kuboresha biashara ya mazao. Pia, itaanza ujenzi wa Maabara Kuu ya Kilimo kwa ajili ya kupima kiwango cha sumukuvu katika mazao ya mahindi na karanga.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwahakikishia wakulima wetu soko la mazao ya kilimo, NFRA kwa mwaka 2021/2022 imeuza tani 19,601.141 ili kupambana na mfumuko wa bei hatua iliyochangia bei ya mahindi kushuka. Katika mwaka 2022/2023, NFRA itanunua tani 100,000 za nafaka na utaratibu huu wa kununua na kuuza tutaendelea kuutumia pale ambapo bei ya mazao inashuka ili kumlinda mkulima, kuhifadhi na kuuza pale ambapo bei ya chakula inapopanda kumlinda mlaji.

**4.6. Taasisi za Fedha na Upatikanaji wa Mitaji**

**167.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kuhamasisha Taasisi za fedha kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima na itashirikiana na Taasisi za Fedha ambazo zitakuwa tayari kufanya biashara na wakulima katika mazingira yanayoendana na shughuli za wakulima.

**168.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imepanga kujadiliana na Wizara ya Fedha na Mipango na Benki Kuu ya Tanzania ili kuangalia mfumo bora ambao utaiwezesha Sekta ya Kilimo na wakulima wadogo kupata mitaji kwani mfumo wa sasa wa ukopeshaji wa Taasisi za Fedha unaendeshwa zaidi na mfumo wa kibiashara unaozingatia dhamana isiyohamishika, *Cashflow* na dhamana iliyosajiliwa (*registered assets*). Utaratibu huo unakinzana na shughuli za kiuchumi za wakulima ambazo zinaendeshwa zaidi na mfumo ambao Taasisi za Fedha na sheria za ukopeshaji katika nchi yetu haziutambui.

**169.** Aidha, siyo rahisi kwa mkulima kukopeshwa kwa hati yake ya kimila na dhamana ya mazao yake. Jambo hili litakuwa ni moja ya vipaumbele vya Wizara kutaka mabadiliko katika mfumo wa ukopeshaji nchini.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na TIRA itaendelea kukamilisha skimu kwa ajili ya Bima ya mazao ambayo itamlinda mkulima kuanzia shambani, uhifadhi na sokoni ili kuzifanya Taasisi za Fedha iwe rahisi kumpatia mikopo pale anapohitaji.

**171.** Vilevile, Wizara kupitia AGITF itatoa mikopo 285 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 7.45** kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

**4.7. Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Hifadhi ya Mazao ya Kilimo**

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, kwa kuanzia Wizara imepanga kuongeza uwezo wa kuhifadhi na kupunguza upotevu wa mazao kwa kujenga ghala ndogondogo 70 karibu na maeneo ya uzalishaji zenye uwezo wa kuhifadhi kati ya tani 300 hadi tani 1,000 kila moja. Ghala hizo zitajengwa katika mikoa mbalimbali ya uzalishaji. Jumla ya **Shilingi Bilioni 25.16** zitatumika.

**173.** Vilevile, Wizara itakamilisha ujenzi wa ghala tisa (9) na vihenge 56 vya kisasa kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi wa NFRA ili kuongeza uwezo wa NFRA wa kuhifadhi kutoka tani 251,000 hadi tani 501,000. Pia, itakamilisha ujenzi wa ghala 14 kupitia mradi wa TANIPAC zenye uwezo wa kuhifadhi tani 21,000; na itakamilisha ujenzi wa ghala la Mtimbila AMCOS lililopo Malinyi na ghala la Kijiji cha Mkula lililopo Ifakara. Aidha, itakamilisha ukarabati wa ghala 17 zilizopo katika Halmashauri za Songea (10) na Madaba (7). Jumla ya **Shilingi Bilioni 40.45** zitatumika.

**4.8. Kuhamasisha Kilimo cha Mashamba Makubwa**

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itasimamia ufufuaji na uendelezaji wa mashamba yaliyokuwa chini ya NAFCO yenye hekta 24,632.8; na mashamba saba (7) ya maua yenye hekta 797.66 yaliyochukuliwa na Serikali. Vilevile, Wizara itatekeleza mpango wa kutenga na kulinda ardhi ya kilimo kwa lengo la kuwa na benki ya ardhi kwa uwekezaji wa mashamba makubwa yatakayojengewa miundombinu muhimu. Jumla ya **Shilingi Bilioni 3** zimetengwa kwa ajili ya kuanza kutekeleza mpango huo.

**4.9. Kuimarisha Kilimo Anga**

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itakamilisha utaratibu wa ununuzi wa ndege moja (1) mpya na kukamilisha ukarabati wa ndege moja (1) ya kufanya savei ya visumbufu vya mimea na mazao ili kuondoa tatizo la kutegemea ndege kutoka nje kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu vya mazao. Hii ni kuondoa tatizo liliopo sasa tukikabiliwa na visumbufu tunahangaika kutafuta ndege katika jumuiya ambazo sisi ni wanachama, nia na madhumuni katika eneo hili ni kujitegemea. Jumla ya **Shilingi Bilioni 3** zimetengwa.

**4.10. Maendeleo ya ushirika**

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itakamilisha uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ili kuchochea maendeleo ya ushirika nchini. Vilevile, itaendelea kuhamasisha na kusimamia Vyama vya Ushirika, kufufua na kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ikiwemo viwanda vya kuchambua pamba (*ginneries*) vya Manawa, Sola na Mugango, na Buyagu (Sengerema) na kiwanda cha TANECU chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 za korosho na kutoa ajira 500. Aidha, itaimarisha usimamizi wa vyama vya ushirika kwa kununua magari manne (4) na pikipiki 50.

**177.** Aidha, itaendelea na uthamini wa mali za Vyama vya Ushirika na kurejesha mali zilizomilikishwa kwa maslahi binafsi; itaanzisha Mfuko wa Bima ya Akiba na Amana za SACCOS; itaanza kutumia Mfumo wa kielekitroniki katika kusimamia Vyama vya Ushirika na kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuanzisha kampuni ili viweze kujiendesha kibiashara.

**1.1.1. Ushiriki wa Vijana katika Sekta ya Kilimo**

**178.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa nyakati tofauti kumekuwa na dhana kuwa vijana hawapendi kilimo. Ukweli ni kwamba vijana na wanawake ni nguvukazi inayotumika katika uzalishaji kwenye Sekta ya Kilimo kwa kuzalisha na kuuza mazao ya kilimo, uuzaji wa pembejeo na uchakataji wa mazao katika ngazi ya awali.

**179.** Changamoto zinazowakabili vijana ni pamoja na; ukosefu wa mitaji, upatikanaji wa ardhi ya kilimo, uhaba wa miundombinu ya umwagiliaji, ujuzi na kukosekana kwa mazingira bora yanayovutia vijana na wanawake kushiriki katika kilimo.

**180.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua changamoto zinazowakabili vijana, Wizara imepanga kutengeneza ajira Milioni 1 za vijana katika Sekta ya Kilimo ifikapo 2025 kwa kuanzisha programu ya vijana inayojulikana kama ***Building Today for a Better Tomorrow***. Kupitia programu hiyo, Wizara itawekeza katika kuanzisha maeneo maalumu ya uwekezaji wa kilimo (*Agriculture parks*) na mashamba ya pamoja (*block farms*).

**181.** Maeneo hayo yatajengewa miundombinu ya umwagiliaji na ghala za kuhifadhi mazao. Aidha, vijana watapatiwa teknolojia za kisasa za uzalishaji, mitaji, pembejeo za kilimo na kuunganishwa na masoko. Maeneo yaliyoanza kutengwa ni pamoja na hekta 7,664 katika Halmashauri za Wilaya za Chamwino (hekta 6,179.2) na Bahi (hekta 1,484.8) mkoani Dodoma. Mazao ya kipaumbele yatakayo zingatiwa katika utekelezaji wa mpango huo ni alizeti, soya, ngano na mazao ya bustani.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi Bilioni 3** zimetengwa kwa ajili ya kuanza kutekeleza mpango huo ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 1** zitatumika kama dhamana ya mikopo kwa vijana. Jukumu la Serikali kwenye eneo hili litakuwa ni kutafuta ardhi, kuisafisha, kuiwekea miundombinu inayohitajika na kuwagawia vijana kuanzia ekari 10 hadi 50 kutegemea na zao. Lengo ni kuwapatia vijana ajira na kipato cha uhakika. Programu hiyo kwa majaribio itaanza mkoa wa Dodoma ili kubadili fikra na dhana kuwa kilimo hakilipi.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hatua hii, Wizara kupitia Tume ya Umwagiliaji itafanya kazi ya kutambua vijana waliojiajiri kwenye Sekta ya Kilimo wanaokabiliwa na changamoto za uwekezaji kwenye mifumo ya umwagiliaji na kuwawezesha. Kupitia Bunge lako Tukufu, ninaviomba viwanda vya plastiki vianze uzalishaji wa vifaa vya kilimo vya umwagiliaji ikiwemo mabomba, mabomba ya kumwagilia kwa njia ya matone na *dam liners* na sisi kama Wizara tutawapa kipaumbele wazalishaji wote wa vifaa hivyo ndani ya nchi.

**Maelezo ya kina kuhusu mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023 yanapatikana uk. wa 130 hadi uk. 224 wa kitabu cha hotuba yangu.**

**5. SHUKRANI**

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani za pekee kwa wakulima kwa kazi kubwa wanazofanya na kuendeleza kilimo na kuhakikisha usalama wa nchi kwani Taifa lolote haliwezi kuwa salama kama watu wake wana njaa. Ni wazi kuwa mafanikio ya kilimo yanatokana na juhudi za wakulima na ushirikiano wanaopata kwenye Serikali yao. Vilevile, niwape pole kwa maumivu waliyoyapata kwa msimu huu ulioisha kwa gharama za pembejeo kupanda, ninafahamu wamebeba mzigo mkubwa sana niwahakikishie Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan kuanzia tarehe 1 Julai, itawapatia ruzuku ya mbolea, ili kupunguza maumivu yaliyotokana na athari za UVIKO na vita inayoendelea ya Ukraine na Urusi na kamwe mama hatawaacha wanae wasononeke na washindwe kufanya shughuli zao takatifu za kilimo na utumishi wao kwa Taifa lao.

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwashukuru Wadau wa Maendeleo, Washirika wa Kibiashara, Sekta Binafsi, Taasisi za Fedha na Benki za Tanzania na kwa msisitizo TADB, NMB, CRDB kwa kukubali Benki hizi tatu kushusha riba kwa wakulima mpaka asilimia 9, ninawaahidi kama Waziri wa Kilimo, nitaendelea kushirikiana na ninyi na yeyote ambaye atakubali kutoa riba kwa wakulima kwa asilimia ya tarakimu moja na kupunguza masharti ya ukopeshaji ambayo siyo rafiki kwa mkulima.

**186.** ***Mheshimiwa Spika*** niendelee kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambao wameshirikiana na Wizara katika kuleta maendeleo kwenye nchi yetu. Naomba kutaja baadhi ya Nchi na Mashirika ya Kimataifa kama ifuatavyo: Washirika wa Kibiashara na Maendeleo wakiwemo Serikali za Vietnam, Israel, Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Kuwait, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Canada, Poland na Umoja wa Falme za Kiarabu.

**187.** Ninayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: WFP, FAO, USAID, UNDP, IFAD, AGRA, GIZ, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, IMF, AU, DFID, JICA, EU, ENABEL, UNICEF, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI na CABI. Nyingine ni EAC, SADC, SAGCOT, ACT, TPSF, AVRDC, KILIMO TRUST, CIP, CIAT/PABRA, UNEP, WARDA, Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA), Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu (IRLCO-CSA) na HELVETAS. Wadau wengine ni, Bill and Melinda Gates Foundation, TAHA, Gatsby Trust, Rockfeller Foundation, Clinton Foundation, Aga Khan Foundation, na Asasi zisizo za kiserikali nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja zote hapa.

**188.** ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba nirejee kumshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yake kwangu ya kusimamia Sekta ya Kilimo na msukumo wake wa kuipa Sekta ya Kilimo kipaumbele hususan katika utafiti na uzalishaji wa mbegu, umwagiliaji na huduma za ugani. Ninaahidi kuwa nitaendelea kuwa muaminifu, mtiifu na kutekeleza majukumu yangu ya Waziri wa Kilimo kwa bidii, weledi na uadilifu kwa maslahi ya nchi yetu.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** nirejee pia kumshukuru Mhe. Anthony Peter Mavunde (Mb) Naibu Waziri wa Kilimo na Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa ushirikiano wa dhati anaonipatia katika kutimiza majukumu yangu ya uwaziri.

**190.** Aidha, kipekee nirudie kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Nzega Mjini kwa namna wanavyoniunga mkono na kunipa ushirikiano wa dhati katika kuleta maendeleo ya jimbo letu.

**191.** ***Mheshimiwa Spika, kilimo ni msingi mkuu wa historia ya ustaarabu wa binadamu, msingi mkuu wa uhuru kamili wa binadamu, msingi mkuu wa mabadiliko ya kiuchumi, msingi mkuu wa maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa Taifa lolote, familia yoyote ambayo haiwezi kulisha watu wake ni sawa na mtumwa aliyefungwa minyororo. Ili tuweze kuleta mapinduzi ya kiuchumi, mapinduzi ya viwanda, elimu bora kwa jamii yetu ni lazima tuwe na uhakika wa chakula, kujilisha, kuhifadhi na kulisha wengine ili kama Taifa tuwe na uwezo wa kujiamulia na kuwaamulia wengine kwa maslahi ya Taifa letu.***

**192.** ***Mheshimiwa Spika*** sisi kama Taifa hatuuzi vifaru vya kivita, hatuuzi ndege, hatuuzi *Artificial Intelligence technology*, kitu pekee tunaweza kutoa kwa wingi duniani ni Chakula. Rais wa Awamu ya Sita Mhe. Samia Suluhu Hassan ameonesha utashi wa kisiasa na utayari wa kuwekeza kwenye kilimo. Nitumie fursa hii kuwaomba watanzania wenzangu kuitumia fursa ya Awamu ya Sita kuwekeza katika sekta ya kilimo na kutumia fursa ya ukuaji wa idadi ya watu duniani kama eneo la sisi kuondoa umasikini wa watu wetu na kuifanya Tanzania kuwa ghala la chakula kwa kuwa tutakuwa na uwezo wa kulisha wengine.

**193.** Hivyo, ninaomba watanzania wote watambue kuwa kilimo ni biashara, kilimo ni maisha.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua ukweli kuwa kilimo ni msingi wa ustawi wa maisha ya mwanadamu na kwa utashi wa kisiasa wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kuendeleza kilimo, Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2022/2023 inalengo la kukuza uchumi wa nchi kwa kuwekeza fedha katika maeneo ya kipaumbele ambayo bajeti yake imeongezeka kama ifuatavyo:-

i. Uzalishaji wa mbegu kutoka Shilingi Bilioni 10.58 hadi Shilingi Bilioni 43.03;
ii. Utafiti wa kilimo kutoka Shilingi Bilioni 11.63 hadi Shilingi Bilioni 40.7;
iii. Umwagiliaji kutoka Shilingi Bilioni 46.5 hadi Shilingi Bilioni 361.5;
iv. Ujenzi wa ghala kutoka Shilingi Bilioni 2.02 hadi Shilingi Bilioni 25.16;
v. Kuimarisha huduma za ugani kutoka Shilingi Bilioni 11.5 hadi Shilingi Bilioni 15;

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, bajeti ya mwaka 2022/2023 imejielekeza katika:

i. Kutoa ruzuku ya mbolea kwa mazao yote;
ii. Kuendeleza mashamba makubwa na kuongeza ushiriki wa vijana kwenye kilimo;
iii. Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kugharamia Sekta ya Kilimo;
iv. Kuanzisha Ofisi za umwagiliaji za Wilaya katika Halmashauri 146;
v. kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 18.6 hadi tani milioni 20.23;
vi. Kuongeza uzalishaji wa mazao yenye mahitaji makubwa hususan mazao ya alizeti, ngano na chikichi;
vii. kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani kutoka tani milioni 7.3 kufikia tani milioni 8.5;
viii. kuimarisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi;
ix. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati yakiwemo:
   o Pamba kutoka tani 144,000 hadi tani 350,000
   o Korosho kutoka tani 238,000 hadi tani 400,000
   o Tumbaku kutoka tani 58,000 hadi 95,000;
   o Kahawa kutoka tani 65,235 hadi tani 72,000
   o Zabibu kutoka tani 16,138 hadi tani 17,430
   o Mkonge kutoka tani 36,169.8 hadi tani 60,000
   o Chai kutoka tani 11,962 hadi tani 30,000
x. Uzalishaji wa mbegu za mazao ya chakula na mafuta

| Na. | Aina ya Zao | Makisio ya uzalishaji wa mazao msimu wa 2022/2023 (Tani) | Mkadirio ya mahitaji ya *Certified Seeds* 2022/2023 (Tani) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mahindi | 7,219,000 | 32,500 |
| 2 | Alizeti | 941,000 | 5,600 |
| 3 | Soya | 500,000 | 25,000 |
| 4 | Ngano | 150,000 | 7,200 |
| 5 | Mpunga | 2,832,000 | 16,000 |
| **JUMLA** | | **11,642,000** | **86,300** |

**6. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023**

**6.1. Makusanyo ya Maduhuli**

**196.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inatarajia kukusanya **Shilingi 126,117,732,000** kutokana na vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 17,732,000** zitakusanywa kupitia Fungu 43 na **Shilingi 126,100,000,000** zitakusanywa kupitia Fungu Na.05.

**197.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Bajeti ya Wizara ya Kilimo imeongezeka kwa mafungu yote matatu kutoka **Shilingi 294,162,071,000** hadi **Shilingi 751,123,280,000** sawa na ongezeko la asilimia **155.34**

**198.** ***Mheshimiwa Spika***, Sehemu kubwa ya fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, miundombinu ya uhifadhi wa mazao, kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao, kuimarisha utafiti wa kilimo, uzalishaji wa mbegu na utoaji wa ruzuku.

**6.2. Fedha kwa Mafungu yote (43, 24 na 05)**

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 751,123,280,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 kama ifuatavyo;

**6.3. Fedha kwa Fungu 43**

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 368,561,661,000** kupitia Fungu 43 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 268,906,114,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 185,978,709,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 82,927,405,000** ni fedha za nje. Aidha, **Shilingi 99,655,547,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo **Shilingi 49,403,470,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 50,252,077,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**1.1.2. Fedha kwa Fungu 05**

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 366,768,352,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 361,500,000,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 350,000,000,000** ni fedha za Ndani na **Shilingi 11,500,000,000** ni fedha za nje. Aidha, kati ya fedha zinazoombwa, **Shilingi 5,268,352,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 3,630,168,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na **Shilingi 1,638,184,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

**1.1.3. Fedha kwa Fungu 24**

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 15,793,267,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,100,000,000** ni kwa ajili kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 550,000,000** ni kwa ajili ya Tume na **Shilingi 550,000,000** ni kwa ajili ya COASCO. Aidha, kati ya fedha zinazoombwa **Shilingi 14,693,267,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 5,549,009,000** ni fedha za matumizi mengineyo ya Tume na **Shilingi 5,115,312,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Tume. Aidha, **Shilingi 2,380,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo ya COASCO na **Shilingi 1,648,946,000** ni kwa ajili ya mishahara ya COASCO.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara: ***www.kilimo.go.tz***

**7. HITIMISHO**

**204.** ***Mheshimiwa Spika***, NAOMBA KUTOA HOJA





# Halmashauri nchini zatakiwa kutunga sheria kulinda anwani

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

HALMASHAURI nchini, zimeagizwa kuandaa sheria ndogo zitakazotumika kulinda miundombinu ya anuani za makazi, ili isiharibiwe au kuhujumiwa baada ya kukamilika.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, aliyeongozana na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye kukagua uwekaji wa anuani za makazi mkoani Mbeya.

Alisema uwekaji wa anuani za makazi unatekelezwa nchi nzima na kwamba umeghârimu fedha nyingi za watanzania, hivyo miundombinu inayowekwa inastahili kutunzwa ili idumu na kutumika kwa muda mrefu.

"Zoezi la uwekaji wa anuani za makazi linakwenda sambamba na uwekaji wa miundombinu kama vile vibao vinavyoonyesha majina ya mitaa na nambari za nyumba, miundombinu hii inahitaji kutunzwa na watanzania wote, lakini haiwezi kutunzwa ipasavyo kama hakuna sheria ya kuilinda, baada ya kukamilika, wizara yangu inaziagiza halmashauri kuandaa sheria ndogo za kulinda miundombinu hii," alisema Silinde.

Akitoa taarifa ya uwekaji wa anuani za makazi mkoani Mbeya, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Juma Madito, alisema kiasi cha Sh. bilioni 1.2 kilichotolewa na serikali kilitumika kutekeleza na huku mkoa uliongeza Sh. milioni 300 kusaidia kukamilika kwake, na kwamba wamefikia asilimia 85 ya eneo husika.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema uwekaji wa anwani hizo unaendelea vizuri na wanatarajia kukamilisha Mei 22, mwaka huu.

Kwa upande wake, Waziri Nnauye aliwaagiza viongozi wa mikoa yote kukamilisha kazi hiyo bila kuwabebesha mzigo wa michango wananchi.

Aidha, alisema jambo hilo halipaswi kuwa kero kwa wananchi na badala yake la furaha kutokana na manufaa yake.



Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Bonde la Ziwa Rukwa, Thadeus Ndeseiyo (kushoto), akitoa maelezo kuhusu namna bora ya kupunguza uchafuzi wa vyanzo vya maji ndani ya bonde hilo, wakati wa jukwaa la nne la wadau wa rasilimali za maji lililowahusisha maofisa wa kilimo na umwagiliaji, wahandisi, maofisa mifugo, mamlaka za maji, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kutoka mikoa ya Rukwa, Mbeya na Katavi, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RUJUWASA yadai ankara za milioni 33/-

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

MAMLAKA ya Maji taka na Usafi wa Mazingira, Mji mdogo wa Rujewa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya (RUJUWASA), inawadai wateja wenye madeni sugu jumla ya Sh. 33,159,801, hali inayosababisha washindwe kujiendesha.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa na Mkurugenzi Mtendaji wa RUJUWASA, Lestus Linda, wadaiwa wengi ni taasisi za serikali.

Alizitaja baadhi ya taasisi na kiasi cha madeni kwenye mabano ni Jeshi la magereza (Sh. milioni 10.5), Ofisi ya Bonde la Maji la Mto Rufiji (milioni 5.6) na Hospitali ya Wilaya ya Mbarali (Shilingi 1,082,000).

Nyingine ni ofisi ya Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbarali (Sh milioni 3) na Shule ya Sekondari ya Riverside ya eneo la Lugelele (Sh. milioni moja).

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji huyo wa RUJUWASA wapo wadaiwa sugu 79, huku zikifanyika jitihada kuwakumbusha na kufuatilia walipe lakini bado hazijafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Mamlaka imekuwa ikiwapa taarifa kwa kuwapelekea ankara za maji, tumekuwa tukitumia vyombo vya matangazo kwa njia ya gari hali kadhalika tumekuwa tukiwatumia ujumbe mfupi wa maandishi na kuwapigia simu lakini uitikiaji umekuwa mdogo," alisema Linda.

Alisema kiasi hicho cha fedha kikipatikana mamlaka itapeleka maji maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao kama mtaa wa Mabanda B.

Pia, zitasaidia kuboresha huduma za maji na miundombinu chakavu, kununua pampu ya kisima cha maji Rujewa, ambacho kimeshindwa kuhudumia wananchi.

Akizungumza katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Baraza la Mamlaka ya Mji mdogo wa Rujewa, Chameta Godigodi aliwasihi wateja wa RUJUWASA kutambua kuwa Mamlaka hiyo inapaswa kujiendesha pia kwa kutumia fedha zinazokusanywa kutoka kwao, na kwamba ili huduma iwe endelevu wanapaswa kulipa ankara. Aidha, Godigodi alizitaka pia taasisi za umma zinazodaiwa kutambua wajibu wao kwa kulipa madeni hayo ili waendelee kupata huduma ya maji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Missana Kwangura aliahidi kulifanyia kazi deni la hospitali ya wilaya na kwamba hayupo tayari kuona huduma inasitishwa.

# Mil. 204/- kujenga barabara Mbarali

**Na Mwandishi wetu,** MBARALI

SERIKALI imetoa Sh. milioni 204 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Igalako Mwatenga hadi Kilambo ambayo tangu uhuru haijawahi kufanyiwa maboresho.

Barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 21 imeanza kutengenezwa na Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, inajengwa na mkandarasi wa mradi huo MS/ Ubaruku Limited.

Akizungumza jana wakati wa ziara ya kukagua matengenezo ya barabara hiyo, Meneja wa TARURA wilayani humo, Rashid Kavandama alisema hadi sasa ujenzi wa barabara hiyo umefikia asilimia 30.

Alisema fedha za mradi huo zimetokana na makusanyo ya tozo za miamala ya simu kupitia mfuko wa barabara, na kwamba Oktoba 31, mwaka 2021 ulianza kutekelezwa lakini kutokana na mvua walipunguza kasi ya ujenzi.

Aidha, alisema makubaliano ni kuwa hadi Juni 29, mwaka huu uwe umekamilika ili wananchi wapate huduma muhimu.

"Mradi huu unatekelezwa na TARURA kupitia mfuko wa barabara unaotokana na tozo za miamala ya simu jumla ya Sh. milioni 204 tulipatiwa na serikali kujenga barabara hiyo, ambayo imekuwa korofi kwa kipindi kirefu, mkandarasi anaendelea na kazi," alisema Mhandisi Kavandama.

Aliongeza kuwa kazi inayoendelea kwa sasa ni kuendelea kuinua tuta la barabara kilomita tatu, ili kuzuia barabara hiyo kumomonyoka na kuharibiwa na mvua au mifereji ya maji inayoingia kwenye mashamba ya mpunga.

Naye, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kilambo, Mwakami Matiga, alishukuru serikali kwa kuwatengenezea barabara hiyo kutokana na umuhimu wake na kwamba kipindi cha masika mawasiliano ya barabara hiyo yalikuwa yana katika na kukwamisha shughuli zote za kiuchumi ikiwamo kilimo cha mpunga, ufugaji na watoto kwenda shule.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa barabara hiyo kutachochea maendeleo, kwa kuwa wakulima watasafirisha mazao yao bila vikwazo, wananchi kupata huduma za kijamii kwa wakati.

Akikagua maendeleo ya mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alimtaka mkandarasi anayesimamia mradi huo kujenga kwa kuzingatia viwango vinavyohitajika.

Aidha, aliitaka TARURA kufuatilia na kuhakikisha matengenezo ya barabara hiyo yanakamilika kwa wakati uliopangwa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.





# 'Hakuna vikwazo biashara Bara, Zanzibar'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, amesema hakuna vikwazo vya kibiashara kati ya Tanzania Bara na Zanzibar bali kilichoko ni ushindani wa kibiashara ambao upo katika mfumo halali wa soko huria.

Shaaban alisema hayo wakati akijibu hoja zilizoibuliwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kikao cha baraza hilo, walipokuwa wakichangia makadirio mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022-2023.

Alisema hakuna tatizo la kisheria wala kikanuni katika usafirishaji na uingizaji wa bidhaa kwa wafanyabiashara kutoka Zanzibar wakati wanaposafirisha bidhaa zao kwenda Tanzania Bara.

Alisema utambulisho wa vyeti unaotolewa na Shirika la Viwango la Zanzibar (ZBS) hauna matatizo ambao unatambuliwa kwa mujibu wa sheria na Shirika la Viwango la Tanzania Bara (TBS).

Alisema bidhaa za wafanyabiashara kutoka Zanzibar zinazosafirishwa hadi Tanzania Bara zinatambuliwa na taasisi za viwango na hazijazuiliwa kuingia katika soko la Tanzania Bara.

"Mheshimiwa Spika nataka nijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliotaka kujuwa kwa nini bidhaa za biashara za wafanyabiashara kutoka Zanzibar zinapoingia Tanzania Bara zinazuiliwa...si kweli hatuna taarifa za matukio ya aina hiyo,"alisema.

Aidha, alisema yeye binafsi alifanya uchunguzi na kuwahoji wafanyabiashara mbalimbali wanaosafirisha bidhaa kwenda Tanzania Bara wanaozafirisha bidhaa za viwandani ikiwamo za vinjwaji na kujibiwa kwamba hakuna vikwazo hivyo.

"Suala la vikwazo kwa wafanyabiashara kutoka Zanzibar wanaosafirisha bidhaa zao za viwandani kwenda Tanzania Bara kwa sasa halipo tena....kero zote tumezipatia ufumbuzi mimi binafsi nafuatilia kwa kiwango kikubwa na kuwauliza wamiliki wa viwanda na kujibu kwamba hakuna isipokuwa wanakabiliwa na ushindani wa soko na ubora wa uzalishaji," alisema.

Waziri Shaaban alisema kwamba Zanzibar imejipanga kukabiliana na soko la AGOA la Marekani kwa kusafirisha bidhaa za aina 3.

Alizitaja bidhaa hizo zenye kuhimili soko la AGOA ni pamoja na viwanda vya nguo, uzalishaji wa mazao ya viungo pamoja na kazi za mikono za kinamama ikiwamo utengenezaji wa mikoba.

Kwa upande wa soko la bidhaa za viungo, alisema wameanza kuwashajihisha wakulima kuzalisha mazao ya vanila, pilipili manga na hiliki ambapo soko lake lipo la uhakika katika nchi za Ulaya na Denmark.

"Mheshimiwa Spika tumejipanga vizuri kuingia katika ushindani wa soko la AGOA la Marekani ambalo ni maalumu kwa ajili ya nchi za Bara la Afrika kwa kupeleka bidhaa za viungo na nguo katika kiwanda chetu cha Basra kiliopo Maruhubi Unguja," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2022-2023 huku uzalishaji wa kilimo cha mwani ukipewa kipaumbele.

## Wawakilishi wahoji kasi vifo kinamama, watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Wizara ya Afya kuelezea sababu za kuongezeka kwa vifo vya kinamama na watoto wachanga ambavyo vimewashtuwa wananchi licha ya wizara kuimarisha mazingira mazuri ya huduma hizo.

Wakichangia makadirio na mapato ya wizara hiyo, Mwakilishi wa Viti Maalumu, Salha Mohd Mwinjuma, alisema wamesikitishwa na taarifa za wizara kuongezeka kwa vifo vya kinamama na watoto wachanga huku wakifahamu kwamba huduma za afya zimeimarika hadi vijijini.

Alisema kwa muda mrefu mikakati ya wizara ilikuwa kupambana na vifo vya kinamama na watoto kwa lengo la kuyafikia malengo endelevu ya dunia yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa na kuwapo kwa ustawi bora wa watoto.

"Mheshimiwa tunataka uje utufahamishe kwa nini vifo vya kinamama na watoto vimeongezeka huku tukijua kwamba huduma hizo zimeimarika kwa mujibu wa bajeti ya Wizara ya Afya kwa zaidi ya miaka mitatu,"alisema.

Mwakilishi wa Mahonda, Asha Abdalla Mussa, alimtaka waziri alieleze baraza kwa nini vifo vya kinamama na watoto vimeongezeka huku serikali ikifanikiwa kujenga hospitali zenye hadhi ya kutoa huduma kwa makundi hayo Unguja na Pemba.

Mwakilishi wa Jimbo la Gando Pemba, Mariyam Juma, aliitaka wizara kuharakisha kuanza kwa ujenzi wa Hospitali ya Wete ambayo ni muhimu kwa wananchi wengi wanaotoka Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema vifo vinavyotokana na kinamama na watoto ni matokeo ya kinamama wengi kujifungulia majumbani kutokana na huduma hizo kupungua katika hospitali inayotegemewa ya Wete kushindwa kutoa huduma muhimu za afya.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othumani Masoud Othuman (wapili kulia), akipata maelezo kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alipotembelea banda la benki hiyo kwenye ufunguzi wa maonyesho ya kitaifa ya Wiki ya Ubunifu (MAKISATU), jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ukarabati Hospitali ya Wilaya ya Wete Agosti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema mradi mkubwa wa ukarabati wa Hospitali ya Wete Pemba chini ya ufadhili wa Mfuko wa Abudhabi unatarajiwa kutekelezwa Agosti mwaka huu, huku mradi wa ujenzi wa hospitali 10 za wilaya ukifikia asilimia 50.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha 2022-2023, katika Baraza la Wawakilishi Chukwani Unguja.

Mazrui alisema ujenzi wa hospitali 10 ikiwamo moja ya mkoa inayojengwa hapo Lumumba Mkoa wa Mjini Magharibi unatarajiwa kugharimu Sh.60,148,111,863.12.

Alisema ujenzi wa hospitali hizo unaendelea vizuri Unguja na Pemba ambapo tayari jumla ya Sh.24,413,483,411 zimelipwa kwa makandarasi wanaosimamia ujenzi wa miradi hiyo.

Alisema kukamilika kwa miradi ya hospitali hizo kwa kiasi kikubwa utasaidia kutoa huduma za afya na wananchi wa Zanzibar kupata matibabu na hivyo kupunguza majukumu ya wizara kusafirisha wagonjwa kwenda Tanzania Bara na nje ya nchi.

"Mheshimiwa Spika ujenzi wa hospitali za wilaya unafanyika kwa kasi kubwa ambapo matarajio yetu ifikapo mwishoni mwa mwezi wa Juni tutakuwa tumekabidhiwa serikalini,"alisema.

Mazrui alisema serikali inatarajiya kuanza kutekeleza mradi mkubwa wa ukarabati wa Hospitali ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba chini ya ufadhili wa Mfuko wa maendeleo wa Abudhabi unaotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu.

Alisema mradi huo umekwama kwa zaidi ya miaka mitano na hivyo kuzorotesha maendeleo ya sekta ya afya kwa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba wenye idadi kubwa ya wananchi.

Alizitaja hatua zilizochukuliwa kwa sasa ni pamoja na kupatikana kwa mshauri mwelekezi wa mradi huo.

"Mheshimiwa Spika napenda kutoa habari njema kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali ya Abudhabi imekubali kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa Hospitali ya Wete ambao ulikwama kwa muda mrefu na mradi utaanza kuanza Agosti mwaka huu," alisema.

Mazrui alisema kwa mwaka wa fedha 2022-2023 wizara imejipanga kutekeleza vipaumbele 9 ikiwamo kuanzisha Bima ya Afya, kuongeza huduma za kinamama wajawazito na watoto ili kukabiliana na vifo pamoja na kuimarisha kitengo cha utafiti wa maradhi mbalimbali kilioko Binguni Wilaya ya Kati Unguja.

Waziri aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha jumla ya Sh.154,035,109,000 kwa kazi za kawaida na maendeleo pamoja na shughuli za utafiti.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF BUKOBA
AT BUKOBA
MISC CIVIL APPL 3/2022

ANDREW KALYANGO......APPLICANT
VERSUS
BUPUNGU INVESTMENT COMPANY LIMITED.........................1ST RESPONDENT
YASIN MSISI................2ND RESPONDENT
IVENICO AUCTION MART & BROKERS LTD...3RD RESPONDENT

**NOTICE OF HEARING**

**TO: YASIN MSISI OF MUTUKULA-RAKAI**
**+256 77811121 RAKAI**

**TAKE NOTE** that the mentioned case has been set down for hearing on the 27th day of May,2022 at 8:30 morning,your presence is therefore required on the date and time indicated.
**Given under my hand and the seal of the court this 16th day of May,2022**

May, 2022.
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA
RESIDENT MAGISTRATE BUKOBA

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 77/ 2022
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DANIEL NASONI MBOGOLI of IHUMWA within Dodoma Region.
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SEHEWA DANIEL MBOGOLI
GENERAL CITATION
(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 16 Day of 6, 2022

**Date at Dodoma this 16 day of 5, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIA ODILO MORISI**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya Gari yenye namba ya usajili **T 888 BMS** aina ya canter Mitsubishi.Maria Odilo Morisi huyu ni mke na msimamizi wa mirathi ya marehemu Epharahimu Rudiael. Yeyote atakaeiyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu
**0714700150/0693110091**
**MOR/MOR/RB/176578/2022**

---

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**PARMENA MKUU**
Anatangaza kupotelewa kwa Ofa ya kiwanja **PLOT NO.605 BLOCK 'B' TUNGI** Mkoani morogoro Yeyote atakaeiyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu
**0763003679**
**MOR/MOR/RB/179754/2022**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA, KAGERA LILILOPO BUKOBA
MAOMBI NA: 12/2022
JULIAN JOHN ICHULIKA –The Administor of the Estate of late JOHN BULITI ICHULIKA ......................MWOMBAJI
DHIDI YA

1. ANORD EMMANUEL
2. ERICK APPOLINARY
3. VICTOR GERVASE
4. AJIRATH KAGASHANI
5. ELIUD MAKIKO
6. DENNIS AMAN
7. AMANI SEMI
8. AMOS KAMUGISHA
9. GRATION KOLUGENDO (WAJIBU MAOMBI)

**KWA:- ERICK APPOLINARY, VICTOR GERVASE, AJIRATH KAGASHANI, ELIUD MAKIKO, DENNIS AMAN, AMOSI KAMUGISHA NA GRATION KOLUGENDO (POPOTE MLIPO)**

Mnaarifiwa kuwa maombi Na. 12/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 16/06/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi. Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja na hukumu kutolewa. Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 12/05/2022.

..............................................
**MWENYEKITI - BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA BUKOBA**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**DICKSON W. MAKOMBE**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 919 BQH.**
**Chasis Namba: MBX-0002CFUB41860787**.
Yeyote atakaeiona ate taarifa kituo cha polisi.
**TAARIFA POLISI:**
**IRI/IRI/193052/2022.**

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

# YETU MICROFINANCE BANK PLC

## TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DECEMBER 2021

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 Disemba 2021.
Kiwango kwa Tzs.

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-21 TZS | Mwaka Uliopita 31-Dec-20 TZS |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 187,859 | 1,209,570 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 99,362 | 229,958 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 | Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 27,603 | 102,062 |
| 5 | Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja zilizokubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | | |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi iliyopo | 13,630,215 | 15,449,608 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,615,492 | 1,002,168 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | | |
| 14 | Limbikizo la Mali Kodi | 1,001,760 | 701,445 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 857,686 | 952,051 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **17,419,977** | **19,646,862** |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 18 | Amana za Wateja | 2,274,439 | 2,389,612 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | |
| 20 | Amana Maalumu | 1,418,705 | 1,517,501 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | | |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mteja | | |
| 25 | Mtaji wa Wahisani | | |
| 26 | Mapato yalioingia ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | 277,852 | 176,774 |
| 28 | Madeni | 6,103,966 | 7,000,000 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **10,074,962** | **11,083,887** |
| 30 | **MALI/{DHIMA} HALISI** | **7,345,015** | **8,562,975** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 6,056,497 | 6,056,497 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | | |
| 34 | Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | 1,226,400 | 2,439,474 |
| 35 | Akaunti zingine za Mtaji | - | 0 |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa chache | 62,118 | 67,005 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **7,345,015** | **8,562,976** |
| | | **17,419,977** | **19,646,863** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | | |
| 39 | Mikopo chechefu | 3,708,669 | 1,244,182 |
| 40 | Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | 1,006,413 | 1,184,439 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | % | % |
| i | Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 42% | 44% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 25% | 7% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 396% | 426% |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 78% | 79% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 78% | 79% |
| vi | Ongezeko la Amana | 0% | 0% |
| vii | Ongezeko la Mali | 0% | 0% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 Disemba 2021.
Kiwango kwa Tzs.'(000)'

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-21 TZS | Mwaka Uliopita 31-Dec-20 TZS |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 4,817,514 | 4,013,146 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,012,656 | 800,676 |
| **3** | **Mapato Halisi (1 kutoa 2)** | **3,804,858** | **3,212,470** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo | 1,150,811 | 53,204 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **907,552** | **700,746** |
| | | 0 | 0 |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 417,822 | 539,365 |
| | 6.3 Gawio | | |
| | 6.4 Mapato Mengine | 489,730 | 161,381.10 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **4,987,487** | **4,174,438** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 2,567,939 | 2,279,724 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 47,115 | 30000 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 2,372,433 | 1,864,714 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,425,888)** | **(314,425)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 300,315 | 259,442 |
| 10 | **Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,125,573)** | **(54,983)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | | **0.00** |
| 12 | **Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **(1,125,573)** | **(54,983)** |
| | | 0 | |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | **127** | 125 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | **-** | - |
| 15 | Idadi ya Matawi | **3** | 3 |
| | BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | |
| (i) | Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | **22%** | 16.35% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | **52%** | 37.52% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | **131%** | 129.94% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | **28%** | 20.79% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DECEMBER 2021
Kiwango kwa Tzs '(000)'

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-21 TZS | Mwaka Uliopitia 31-Dec-20 TZS |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **(1,425,888)** | **(314,385)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | |
| | - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | **(87,500)** | 442,003 |
| | -Uchakavu wa Mali za Kudumu | **265,887** | 230,534 |
| | -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | | |
| | -Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | **-** | - |
| | -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | | |
| | | **(1,247,501)** | **358,152** |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | **-** | - |
| | - Badiliko Halisi katika Mikopo | **1,819,393** | 261,246 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | **-483,324** | (34,561) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | **(213,969)** | (376,431) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | **-** | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | **116,321** | (232,323) |
| | | **(9,080)** | **(23,917)** |
| | - Kodi Iliyolipwa | **(130,000)** | (150,000) |
| | Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | **(139,080)** | **(173,917)** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | **(157,850)** | (331,155) |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | **(13,671)** | -201288.00 |
| | Mengineyo Amana za kudumu | | |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | | |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa** | **(171,521)** | **(532,443)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | **(896,035)** | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | **-** | 500,000 |
| | Mtaji Kutokana na Utoaji wa Wahisani | **(4,887)** | 68319.00 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | | |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | **(15,243)** | (272,551) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | **-** | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha* | **(916,165)** | **295,768** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana | **(1,226,766)** | **(410,592)** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo | **1,541,590** | 1,952,182 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo | **314,824** | **1,541,590** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2021

| Kiwango kwa Tzs.'(000)' | Mtaji wa Hisa | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | Akaunti zingine za Mtaji | Tengo la ziada ya jumla | Jumla Tzs |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la wa mwaka 01/01/2020** | **6,056,497** | **-** | **-** | **69,693** | **2,332,349** | **8,458,539** |
| Rekebisho : | | | | | | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha mwaka | - | - | - | - | - | - |
| Toa: Mapato mengine | - | - | - | (69,693) | | (69,693) |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | - | - | | - | - |
| Mtaji wa kisheria | | | - | 67,005 | 434,619 | 501,624 |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | (54,944) | (54,944) |
| Gawio lililolipwa | | | | | (272,551) | (272,551) |
| **Salio kwa mwaka 31.12.2020** | **6,056,497** | **-** | **-** | **67,005** | **2,439,473** | **8,562,975** |
| **Salio la mwaka 01.01.2021** | **6,056,497** | **-** | **-** | **67,005** | **2,439,473** | **8,562,975** |
| Rekebisho : | - | | | | | - |
| Toa: Mapato mengine | - | - | | (4,887) | - | (4,887) |
| Limbikizo la mali mtaji kwa mwaka Jana | | | 1,250,256 | - | (1,250,256) | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | | | (1,125,573) | (1,125,573) |
| Toa: Marekebisho ya mwaka uliopita | - | | | | (87,500) | (87,500) |
| **Salio kwa mwaka 31.12.2021** | **6,056,497** | **-** | **1,250,256** | **62,118** | **(23,856)** | **7,345,015** |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2021

AINA YA BIDHAA

| 1. AKAUNTI ZA AKIBA | | 2. Mkopo | |
|---|---|---|---|
| Kima cha chini cha kufur | 5000/= | Mikopo ya biashara | 36% PA |
| Ada ya mwezi | BURE | Mikopo ya kuboresha nyumba | 18% PA |
| Taarifa ya Akaunti | BURE | Ada ya Mkopo | 2.5% |
| Kuuliza salio | BURE | Bima ya mkopo | 2% |
| Kufunga akaunti | 5000/= | Mkop wa Pembejeo | 30% PA |
| Gharama za kuendesha | 5000/= | Mkopo wa Kilimo | 30% PA |
| Gharama za kuweka fed | BURE | Mikopo ya Staff | 15% PA |
| Account maintanance ch | FREE | Mikopo ya Maji | 26% PA |
| Account maintanance ch | FREE | | |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Taarifa za fedha zimekaguliwa na HLB MEKONSULT na kutoa Hati safi.

**Kuthibitishwa na:**

*Ernest K. Ndimbo* *Mwenyekiti wa Bodi* .............................. *16.05.2022*

*Altemius Millinga* *Mkurugenzi Mtendaji* .............................. *16.05.2022*

# BOREGA SISTERS WATWAA VIKOMBE MICHUANO KUOGELEA YA FK BLUE

**Na Mwandishi Wetu**

WAOGELEAJI wa familia moja Leyna Borega (8) na Lorita Borega (10), wameibuka kidedea katika nafasi ya kwanza kwenye mashindano ya FK Blue Marlins na kushinda vikombe mwishoni mwa wiki.

Wakati Leyna akishinda kikombe kwa waogeleaji wenye miaka nane na kushuka chini, Lorita alishinda taji hilo kwa waogeleaji wenye miaka tisa na 10 katika mashindano hayo yaliyoshirikisha jumla ya waogeleaji 233 kutoka klabu 15 za Tanzania Bara na Zanzibar.

Leyna alifanikiwa kushinda medali nane, mbili kati ya hizo zikiwa ni za dhahabu, tano za fedha na moja ya shaba. Pia mwogeleaji huyo mwenye kipaji cha hali ya juu, alizawadiwa kikombe cha mshindi wa kwanza.

Kwa upande wa Lorita, mbali ya kuwa mshindi wa jumla na kuzawadiwa kikombe, alishinda medali sita, nne kati ya hizo zikiwa ni za dhahabu na mbili za fedha.

Akizungumza baada ya mashindano hayo, Lorita alisema siri ya mafanikio yao ni kufanya mazoezi zaidi na kuzingatia mafundisho kutoka kwa walimu wao.

Alisema wamekuwa wakifanya mazoezi chini ya walimu bora wa Klabu ya FK Blue Marlins na vile vile mwalimu wa shule yao ya kimataifa ya Dar es Salaam Independent School (DIS), Haleluya Mpango.

Leyna anasoma darasa la nne katika shule hiyo na Lorita anasoma darasa la tano.

"Mashindano yalikuwa magumu sana na kila muogeleaji alikuwa anataka kushinda kama ilivyokuwa kwetu. Tunawashukuru waogeleaji wa Klabu ya FK Blue Marlins na makocha wetu kwa kutupa hamasa na mafunzo na vile vile walimu bora wa shule yetu ya kimataifa Dar es Salaam Independent School kwa mafunzo mazuri, mbali ya darasani, pia katika michezo na kutuwezesha kufanya vema," alisema Lorita.

Alisema matokeo hayo yamewapa hamasa kubwa ya kufanya vizuri zaidi katika mashindano yajayo na vile vile katika timu ya Taifa ya Tanzania.

Waogeleaji wengine walioibuka washindi katika makundi ya miaka yao ni Ariel Sykes wa Klabu ya Champion Rise ambaye alishinda kwa waogeleaji wenye miaka chini ya nane kwa wanaume, Maxi Missokia (miaka 9-10, Dar Swim Club), Raya Angemi (miaka 11-12, Taliss-IST), Mulenga Cole (miaka 11-12 wanaume, DSC), Isabela Angemi na Sydney Hardeman (miaka 13-14, Taliss -IST) na Romeo Mwaipasi (miaka 13-14 wanaume, Taliss-IST).

Pia wamo Aravind Raghavendran (miaka 15-16, Taliss-IST), Sofia Latiff (miaka zaidi ya 15, Taliss-IST) na muogeleaji nyota nchini, Collins Saliboko wa Klabu ya DSC aliyeshinda kikombe kwa waoge-



Waogeleaji Leyna Borega (kushoto) na dada yake Lorita wakipozi katika picha baada ya kukabidhiwa zawadi zao za mshindi wa kwanza kwenye mashindano ya FK Blue Marlins mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Ni vita Ligi Daraja la Kwanza Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

VITA ya kutafuta nafasi ya kupanda daraja ili kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao, imeendelea kupamba moto Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja inayoendelea visiwani hapa.

Katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 ambapo nne za chini katika msimamo zitashuka daraja na kurudi katika ligi za mikoa ziliyotoka, Kundemba FC ndiyo inayoongoza ligi hiyo kwa kuvuna alama 43, ikifuatiwa na Klabu ya Dulla Boys yenye alama 41 huku Chuoni FC ikiwa nafasi ya tatu na pointi zake 39 baada ya timu zote kushuka dimbani mara 21 na kila moja ikibakiza mechi tisa.

Kwa upande wa timu ambazo zipo mkiani na bado zitakuwa na nafasi ya kupanda juu endapo zitashinda michezo yao iliyosalia ni timu ya Kilimani City yenye alama 23, African Coast pointi 17, Mchangani FC alama 16 alama sawa timu inayoburuza mkia, Bridge Star.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa timu ya Kilimani City, Abrahaman Salum, alisema tatizo kubwa la timu yao kufanya vibaya linatokana na mgogoro wa uongozi uliopo kwa sasa.

Alisema licha ya mgogoro huo, yeye kama katibu atajitahidi kuwajenga wachezaji kisaikolojia ili kuhakikisha matatizo hayo ya viongozi hayaathiri michezo yao ya ligi na kuwafanya kujilinda kushuka daraja.

Hata hivyo, amewataka wachezaji kuendelea kupambana kwa bili na kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo yao iliyobaki kabla ya msimu kumalizika ili kuweza kufikia malengo yao.

# Yanga kambini kuiwinda Mbeya Kwanza

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Yanga tayari kimeingia kambini kujiwinda na mchezo ujao wa Ligi Kuu ya NBC utakaopigwa Jumamosi wiki katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga ambayo Jumapili iliyopita, imetoka kushinda ugenini dhidi ya Dodoma Jiji katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 60, 11 mbele ya watani wao wa jadi, Simba waliopo nyuma kwa mchezo mmoja.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema kikosi chao kimerejea kambini kikiwa na ari ya ushindi.

"Timu yetu tayari imeingia kambini leo baada ya kupewa mapumziko tulipotoka Dodoma kwenye mechi iliyopita dhidi ya wenyeji, Dodoma Jiji," alisema Bumbuli.

Alisema baada ya kupata pointi tatu kwenye mchezo huo uliopita, wanaelekeza nguvu katika mechi ijayo dhidi ya Mbeya Kwanza ambayo wanaamini itakuwa ngumu.

Bumbuli alisema lengo lao ni kupata pointi tatu katika mchezo huo ambao wanahitaji kufanya vizuri ili kuendelea kuongoza mbio za ubingwa kwa alama nyingi zaidi.

"Mikakati tuliyonayo ni kushinda katika michezo yetu yote iliyopo mbele yetu tukiwa na lengo la kubeba ubingwa msimu huu wa Ligi Kuu ya NBC," alisema.

Alisema wachezaji wote wameahidi kufanya vizuri katika mchezo huo na kuomba mashabiki waendelee kuwaunga mkono Ili watimize malengo yao.

Kuhusu kauli ya Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi baada ya kupangwa tarehe ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu FA Cup, Bumbuli alisema amefurahi kuona ratiba ya mchezo huo imetoka mapema, hivyo baada ya kuvaana na Mbeya Kwanza, wataanza kuwatafutia dawa wapinzani wao, Simba.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Klabu ya Mbeya Kwanza, Mbwana Makata, amesema wataivaa Yanga kwa tahadhari kubwa kwa kuwa ni timu ngumu.

"Tutaingia kwa tahadhari katika mchezo huo, unafahamu tunakutana na timu ngumu ambayo haijafungwa mpaka sasa," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LEWANDOWSKI AGOMBEWA

KLABU ya Chelsea inaweza kuungana na Barcelona katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich na Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33. ***(Guardian).***

### MOURINHO ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wanataka kumshawishi kocha wa Roma, Jose Mourinho kutua St James Park msimu huu licha ya mafanikio ya hivi majuzi ya kocha wa sasa wa 'Magpies', Eddie Howe (***Marca via Express)***

### TEN HAG NA UNITED

KOCHA ajaye wa Manchester United, Erik ten Hag amesema alikuwa na "chaguo la kufanya kazi katika klabu tofauti, yenye msingi bora" lakini akachagua kuchukua kazi Old Trafford. ***(De Telegraaf, kupitia Manchester Evening News)***

### MBAPPE SAFARI MADRID

REAL Madrid wamefikia makubaliano ya mkataba wa miaka mitano na mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 atahamia klabu hiyo ya Hispania mkataba wake na Paris St-Germain utakapokamilika msimu huu wa majira ya joto. ***(Marca)***

### DEMBELE KUTUA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich ina nia ya kumchukua mshambuliaji wa Barcelona, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 25, huku mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa na klabu hiyo ya Hispania ukikamilika mwezi ujao. ***(Sky Sports)***

### NDOMBELE KURUDI SPURS

KLABU ya Lyon haitarajiwi kumsajili kiungo wa kati wa Tottenham na Ufaransa, Tanguy Ndombele kwa mkataba wa kudumu, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, akitarajiwa kurejea London Kaskazini baada ya muda wake wa mkopo na klabu hiyo ya Ufaransa. ***(Football Insider)***

### PHILLIPS AGOMBEWA ENGLAND

KLABU ya Newcastle na Aston Villa zinaongoza katika mbio za kumnunua kiungo wa kati wa Leeds na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26, msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### BRONZE KUHAMA CITY

MKATABA wa beki wa England, Lucy Bronze na Manchester City unakamilika msimu wa majira ya joto na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, anatarajia kuhamia Ligi Kuu ya Marekani. ***(Telegraph)***

### STANWAY, BAYERN SAFI

KIUNGO wa kati wa Manchester City na England, Georgia Stanway mwenye umri wa miaka 23, amekubali makubaliano ya mkataba wa miaka miwili na Bayern Munich. ***(Sky Sports)***

### MARQUINHOS NA ARSENAL

KLABU ya Arsenal imefikia makubaliano ya kumnunua winga wa Sao Paulo, Mbrazil Marquinhos mwenye umri wa miaka 19, katika mkataba wenye thamani ya euro milioni 3.5 ambao utadumu hadi mwaka 2027. ***(Fabrizio Romano).***

### CAMPBEL KUINOA RANGERS

MLINZI wa zamani wa England na Arsenal, Sol Campbel mwenye umri wa miaka 47, anatarajiwa kupewa mikoba ya ukocha Queens Park Rangers. ***(Mchezo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# XHAKA: ARSENAL HAIWEZI KUFUZU MICHUANO UEFA

●●●Kama ukicheza hivi, hustahili Ligi ya Mabingwa Ulaya, hata Ligi ya Europa ni ngumu sana...

**LONDON, England**

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Granit Xhaka, alikasirika baada ya timu yake kufungwa mabao 2-0 na Newcastle kwenye Ligi Kuu England, akisema timu hiyo ya kocha Mikel Arteta "haistahili" kufuzu Ligi ya Mabingwa baada ya matokeo mabaya.

Bao la kujifunga la Ben White liliwapa 'Magpies' uongozi, kabla ya Bruno Guimaraes kuifungia Newcastle la pili na kufifisha matumaini ya Arsenal kumaliza kwenye nne bora na kutinga Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Arsenal sasa wako pointi mbili nyuma ya Tottenham kwenye msimamo huku kukiwa na mechi moja iliyobaki, ambapo Spurs wakipoteza dhidi ya Norwich City watawapa nafasi 'Washikabunduki' hao kurejea katika nafasi nne za juu.

Akizungumza na Sky Sports baada ya kupoteza, Xhaka aliwashutumu wachezaji wenzake na kudai kuwa timu hiyo haistahili kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ni vigumu sana kupata maneno sahihi baada ya mchezo," alisema. "Tulikuja hapa kuonyesha mchezo tofauti, lakini kuanzia dakika ya kwanza hadi dakika 90 hatukustahili kuwapo uwanjani leo (juzi).

"(Kama) ukicheza hivi hustahili Ligi ya Mabingwa Ulaya, hata Ligi ya Europa. Ni ngumu sana kuikubali kwa sasa, sijui kwa nini hatufanyi kile ambacho kocha anatuomba."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 200,

MECHI KALI
AZAM
VERSUS
SIMBA
1 | 3.70
X | 2.87
2 | 2.08

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KANE SASA ATAKA CONTE ABAKI SPURS

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Tottenham, Harry Kane, anatumai Kocha Mkuu, Antonio Conte atabaki klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu, akisema yeye na wachezaji wenzake wanafurahi kufanya kazi na Muitaliano huyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, bila shaka amenufaika kutokana na kuinuliwa kwa Spurs tangu Conte achukue usukani Novemba mwaka jana baada ya Nuno Espirito Santo kutimuliwa.

Wakiwa wameshinda mara tano pekee na kufunga mabao tisa katika mechi 10 za Ligi Kuu chini ya kocha huyo wa zamani wa Wolves, Tottenham wameshinda mechi 16 kati ya 27 za ligi chini ya Conte, wakifunga mabao 55.

Hata hivyo, uvumi umebainisha kuwa Conte anaweza kushawishika kuhamia kwingine mwishoni mwa msimu huu, huku Paris Saint-Germain ikitajwa kuhusishwa naye.

Hata hivyo, Kane ameiambia Standard Sport kwamba, anafurahia kufanya kazi na Conte na anatumai atabaki London Kaskazini.

Alipoulizwa kama alifikiri Conte bado angekuwa kwenye dimba la Spurs msimu ujao, Kane alijibu: "Sijui kuwa mkweli, huo ni uamuzi wake.

"Lakini amefanya kazi kwa bidii sana wakati yupo hapa, ni mtu mzuri sana, mtu mwenye mapenzi ya dhati kwa hiyo uamuzi wake wowote unatakiwa kuuheshimu. Hakika ninafurahia.

"Nimesema mimi ni shabiki wake mkubwa na tunaendelea vizuri, hivyo bila shaka, itakuwa vizuri kwa klabu ikiwa atabaki.

"Lakini kama nilivyosema huo ni uamuzi wake, nina uhakika atazungumza na klabu na kuamua juu ya mustakabali wake. Kwa mtazamo wetu, sote tunafurahia kufanya kazi naye."




# Klopp: Liver haiwezi kumsajili Mbappe

**LIVERPPOL, England**

KOCHA Jurgen Klopp ana nia ya kumsajili Kylian Mbappe, lakini amekubali Liverpool haiwezi kushindana na Real Madrid kuwania saini ya mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain.

Mbappe mkataba wake na PSG unamalizika mwezi ujao na alifichua kuwa wiki iliyopita anakaribia kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake.

Madrid ndio wanaopewa nafasi kubwa ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, huku Liverpool ikiwa ni miongoni mwa klabu zinazomuwania.

Kwa mujibu wa Sky Sport, Liverpool ilifanya jaribio la kutaka kumsajili Mbappe atue pale Santiago Bernabeu.

Lakini wakati Klopp ni shabiki wa




Mbappe, amesisitiza Liverpool hawana nia ya kujaribu kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 katika dirisha lijalo.

"Bila shaka tunavutiwa na Kylian. Sisi sio vipofu," alisema kabla ya mechi muhimu ya Jumanne ya Ligi Kuu dhidi ya Southampton.

"Sina la kusema kuhusu (mawasiliano yaliyoripotiwa) kati ya Kylian na Liverpool... yote ni sawa.

"Tunampenda na kama humpendi basi unapaswa kujiuliza. Lakini hatuwezi kuwa sehemu ya vita hivi; lazima kuwe na klabu nyingine. Bado ni mchezaji mzuri."

Mbappe amefunga mabao 36 na kutoa pasi za mabao 21 kwa PSG msimu huu, na kuwafanya Waparis hao kunyakua taji la 10 la Ligue 1 katika historia ya klabu hiyo.

## HABARI MICHEZO


,000,000

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/05/22 | 18:00 | Crystal Palace vs Manchester Utd | 2.89 | 3.32 | 2.31 |
| 02. 22/05/22 | 18:00 | Brentford vs Leeds | 2.28 | 3.42 | 2.87 |
| 03. 22/05/22 | 18:00 | Burnley vs Newcastle | 2.34 | 3.22 | 2.92 |
| 04. 22/05/22 | 18:00 | Brighton vs West Ham | 2.45 | 3.30 | 2.71 |
| 05. 22/05/22 | 18:00 | Brondby vs Silkeborg | 2.48 | 3.59 | 2.54 |
| 06. 22/05/22 | 18:30 | Kalmar vs Djurgardens IF | 2.77 | 2.97 | 2.48 |
| 07. 22/05/22 | 18:30 | Elche vs Getafe | 3.05 | 2.95 | 2.49 |
| 08. 22/05/22 | 19:00 | Stromsgodset vs Valerenga | 2.64 | 3.29 | 2.54 |
| 09. 22/05/22 | 19:00 | Jerv vs Odd Ballklubb | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 10. 22/05/22 | 21:00 | Ham-Kam vs Rosenborg | 2.53 | 3.27 | 2.68 |
| 11. 22/05/22 | 23:00 | Real Sociedad vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 12. 22/05/22 | 23:00 | Barcelona vs Villarreal | 2.47 | 3.60 | 2.58 |
| 13. 22/05/22 | 23:00 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.35 | 3.35 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 18/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4939 | Consadole Sapporo vs Sagan Tosu | 2.05 | 3.31 | 3.21 |
| 13:00 | 4958 | Ulsan Hyundai vs Jeju Utd | 1.97 | 3.26 | 3.51 |
| 13:00 | 5157 | Shimizu S Pulse vs Sanfrecce Hiroshima | 2.97 | 3.21 | 2.21 |
| 13:00 | 5566 | Gamba Osaka vs Kashima Antlers | 3.70 | 3.50 | 1.84 |
| 13:30 | 2660 | Bucheon vs Gyeongnam | 1.85 | 3.41 | 3.75 |
| 13:30 | 2862 | Seongnam Ilhwa vs Suwon City | 2.62 | 2.96 | 2.62 |
| 13:30 | 4003 | Gangwon vs FC Seoul | 2.93 | 3.17 | 2.26 |
| 13:30 | 4847 | Urawa Red Diamonds vs Yokohama F Marinos | 2.57 | 3.25 | 2.48 |
| 13:30 | 5152 | Ansan Greeners vs Chungnam Asan | 3.70 | 3.07 | 1.99 |
| 14:30 | 2117 | Dinamo Barnaul vs NoSta | 2.49 | 3.25 | 2.80 |
| 14:45 | 4602 | Kokand 1912 vs Pakhtakor | 6.23 | 3.99 | 1.45 |
| 14:45 | 5594 | Surkhon Termez vs Sogdiyona Jizzax | 5.05 | 3.01 | 1.76 |
| 15:15 | 5725 | Johor Darul Takzim vs Pahang FA | 1.25 | 5.45 | 8.37 |
| 16:00 | 1635 | Welayta Dicha FC vs Sidama Bunna SC | 2.68 | 2.78 | 2.73 |
| 17:00 | 1966 | ES Hammam Sousse vs Sportive Zarzis | 1.55 | 3.21 | 7.01 |
| 17:00 | 2817 | Olympique de Beja vs ES Metlaoui | 1.65 | 3.30 | 5.24 |
| 17:00 | 4989 | Sportivo Iteno vs CS 2 de Mayo | 2.73 | 3.02 | 2.48 |
| 17:30 | 1145 | Paide Linnameeskond vs Trans Narva | 1.28 | 5.44 | 7.38 |
| 17:30 | 2352 | Nassaji Mazandaran vs Havadar | 2.25 | 2.40 | 4.18 |
| 18:00 | 1583 | Africain vs ES Sahel | 2.43 | 2.62 | 3.26 |
| 18:00 | 1976 | SK Super Nova vs Spartaks Jurmala | 4.48 | 3.36 | 1.73 |
| 18:00 | 1991 | Hearts of Oak vs Bibiani Gold Stars FC | 1.33 | 4.40 | 11.00 |
| 18:00 | 2146 | CR Belouizdad vs ES Setif | 1.70 | 3.26 | 4.86 |
| 18:00 | 5025 | Mamry Gizycko vs GKS Wikielec | 2.75 | 3.30 | 2.45 |
| 18:00 | 5439 | Slovacko vs Sparta Prague | 2.53 | 3.02 | 2.68 |
| 19:00 | 1251 | Fenerbahce U19 vs Galatasaray U19 | 2.47 | 3.44 | 2.47 |
| 19:00 | 2543 | Hajer Club vs Al Qadisiyah | 2.50 | 2.80 | 3.15 |
| 19:00 | 2744 | Zeljeznicar vs Borac Banja Luka | 2.98 | 2.88 | 2.39 |
| 19:00 | 3143 | Azam vs Simba | 3.70 | 2.87 | 2.08 |
| 19:00 | 3330 | Siroki Brijeg vs FK Sloga Simin Han | 2.23 | 2.86 | 3.30 |
| 19:00 | 3585 | Vifk Vaasa vs GBK Kokkola | 1.28 | 5.44 | 7.38 |
| 19:10 | 5372 | AL Draih vs AL Jeel | 2.32 | 2.90 | 3.40 |
| 19:20 | 2344 | AL Ain vs Al Jabalain | 3.06 | 2.86 | 2.36 |
| 19:30 | 1112 | FC Helsingor vs Lyngby | 2.06 | 3.36 | 3.17 |
| 19:30 | 1876 | Nykobing FC vs Horsens | 7.02 | 5.07 | 1.32 |
| 19:30 | 1973 | Nomme Kalju vs Levadia Tallinn | 4.27 | 3.49 | 1.73 |
| 19:30 | 2238 | Esbjerg vs Fremad Amager | 2.13 | 3.41 | 2.97 |
| 19:30 | 5443 | Hvidovre IF vs FC Fredericia | 2.25 | 3.46 | 2.73 |
| 19:45 | 2317 | Al Orubah vs AL Akhdood | 2.43 | 2.85 | 3.25 |
| 19:45 | 3224 | SBV Excelsior vs Heracles Almelo | 2.92 | 3.67 | 2.15 |
| 20:00 | 1656 | Utsiktens BK vs Landskrona Bois | 1.92 | 3.63 | 3.78 |
| 20:00 | 2130 | Brescia vs Monza | 2.10 | 3.22 | 3.42 |
| 20:00 | 2222 | Skovde Aik vs Orebro SK | 2.92 | 3.38 | 2.37 |
| 20:00 | 2493 | Asarums IF FK vs Kristianstads FF | 4.76 | 3.98 | 1.56 |
| 20:00 | 3578 | Forsbacka IK vs Sandvikens AIK FK | 3.91 | 3.81 | 1.72 |
| 20:00 | 5358 | Vasteras SK vs Jonkopings Sodra | 2.04 | 3.59 | 3.43 |
| 20:00 | 5460 | Orgryte IS vs Trelleborgs FF | 2.46 | 3.39 | 2.79 |
| 21:00 | 5193 | National Bank vs Al Ahly Cairo | 5.97 | 3.53 | 1.60 |
| 21:45 | 2565 | Northampton vs Mansfield | 2.37 | 3.12 | 2.97 |
| 22:00 | 4021 | Eintracht Frankfurt vs Rangers | 2.27 | 3.39 | 2.99 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# 'PRISONS HAKUNA KUKATA TAMAA HADI KIELEWEKE'

**Na Adam Fungamwango**

KIPIGO cha bao 1-0 ilichokipata Tanzania Prisons juzi nyumbani kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Kagera Sugar, kimezidi kuiweka timu hiyo kwenye hali mbaya, huku Kocha Msaidizi, Shaaban Mtupa akidai bado hawajakata tamaa.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Mtupa, straika wa zamani wa timu hiyo, alikiri kupoteza mechi hiyo kumewaweka kwenye wakati mgumu, lakini wanafarijika kuona hakuna yeyote mwenye uhakika wa kubaki kwa timu 14, ukiondoa timu za Simba na Yanga tu.

"Tumefungwa, ni kweli hali yetu ni mbaya, lakini hii haitufanyi kukata tamaa, tutapambana, tumebakisha mechi sita, lolote linaweza kutokea, hakuna timu yenye uhakika wa kubali Ligi Kuu kwa timu 14, kwa hiyo sisi kwa mechi zilizobaki tutafanya vema, tutabaki," alisema.

Lilikuwa ni bao lililowekwa wavuni na mtaalam wa kupiga mipira ya faulo, David Luhende, akifanya hivyo dakika tatu kabla ya mechi kumalizika.

Prisons iliyopanda Ligi Kuu mwaka 1995, kabla ya kushuka mwaka 2009, ilifanikiwa tena kurejea Ligi Kuu 2011, ambapo mafanikio yake makubwa ni kutwaa ubingwa wa Muungano mwaka 1999.

Hata hivyo, kama Prisons isipojirekebisha, inaweza kushuka kutokana na mwenendo wake usioridhisha msimu huu. Kwa sasa inashika nafasi ya 15, ikiwa na pointi 23, ikicheza mechi 24, kushinda sita, sare tano na kupoteza michezo 13.




Wachezaji wa Kagera Sugar, wakimpongeza, David Luhende baada ya kuifungia bao pekee dhidi ya Tanzania Prisons dakika ya 88, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Lule apania kuipeleka Mbeya City kimataifa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, amepiga hesabu za kuibuka na pointi tatu dhidi ya KMC FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lengo lake likiwa ni kuongeza presha ya kuwania nafasi nne za juu kwenye ligi hiyo.

Mbeya City ambayo imeshuka dimbani mara 24, ipo nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 32 sawa na Azam FC iliyopo nafasi ya tatu baada ya kucheza mechi 23.

Timu hizo zinazidiwa pointi mbili na Geita Gold FC iliyopo nafasi ya tatu baada ya kushuka dimbani mara 24 kwenye ligi hiyo ambayo Yanga ipo kileleni ikiwa na pointi 60, 11 zaidi ya Simba iliyopo nafasi ya pili.

Kikosi cha Mbeya City tayari kimewasili Dar es Salaam tangu jana na kesho kitashuka Uwanja wa Uhuru kuwavaa wenyeji wao, KMC FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, baada ya mazoezi waliyofanya katika Uwanja wa Uhuru, Lule alisema wamejiandaa vizuri na mchezo huo kuhakikisha wanatafuta pointi tatu muhimu.

Alisema wachezaji walikuwapo katika safari yao wote wako fiti na tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu zitakazowaweka katika mazingira mazuri ya kumaliza msimu wakiwa nafasi nne ya msimamo wa ligi hiyo.

"Tumekuja kutafuta pointi muhimu katika mchezo wetu dhidi ya KMC FC, mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu tunahitaji alama tatu ili kujiweka katika malengo yetu na wapinzani wetu wanahitaji kutumia vizuri uwanja wao wa nyumbani kutafuta ushindi," alisema Lule.

Alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kuanzia nafasi ya tatu hakuna mwenye uhakika wa kudumu katika nafasi hiyo kwa sasa.

"Tunapoenda kucheza mechi yoyote malengo ya kwanza ni kushinda iwe nyumbani au ugenini, ili kujihakikishia nafasi tuliyopo au kupanda juu katika msimamo," alisema kocha huyo ambaye amedhamiria kuiona timu hiyo inacheza michuano ya kimataifa msimu ujao.

# Michezo

Jumatano Mei 18, 2022
Nipashe



## Xhaka: Arsenal haiwezi kufuzu michuano Uefa

KAZI KAZI LEO...



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini, timu hiyo itashuka Uwanja wa Azam Complex, Chamazi leo kuwavaa wenyeji, Azam FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

# FAINALI UEFA LIVER, MADRID MUBASHARA DARAJANI DAR

●●●Serikali yasema siku hiyo itaonyeshwa katika Daraja la Tanzanite pamoja na Filamu ya Royal Tour huku...

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA mechi ya Fainali ya 67 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya (Uefa Champions League Fainal 2022) itakayopigwa Uwanja wa Stade de France nchini Ufaransa Mei 28, mwaka huu, Watanzania watapata fursa ya kushuhudiwa mtanange huo mubashara katika daraja la jipya la Tanzanite jijini Dar es Salaam sambamba na Filamu ya Royal Tour, imeelezwa.

Serikali ndiyo iliyotoa kauli hiyo kupitia kwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, ambaye amesema mechi hiyo ya fainali itaonyeshwa mubashara nchini kwenye Daraja la Tanzanite kupitia DStv ambapo vivutio mbalimbali vya utalii pia vitaonyeshwa moja kwa moja, hivyo kutoa fursa kwa mamilioni ya wapenzi wa soka kutoka nchi zote za Afrika na dunia kushuhudia mechi hiyo na vivutio vya utalii kutoka Tanzania.

Akizungumza kupitia kipindi cha Powerbreakfast kinachorushwa na Kituo cha Redio cha Clouds Fm, Dar es Salaam jana, Mchengerwa alisema mbali na kurusha mubashara mechi hiyo yenye mvuto mkubwa hapa nchini na duniani kote pia Filamu ya Royal Tour itaonyeshwa kabla ya kuanza mchezo huo ambapo ametoa wito kwa wananchi kujitokeza kushuhudia tukio hilo la kihistoria.

Mchengerwa alifafanua kuwa wakati wa filamu hiyo ya kihistoria iliyomshirikisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ambayo imefungua Tanzania duniani, kutachezeshwa droo ambapo washindi watatu watakaopatikana watatembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini kwa ufadhili wa Bodi ya Utalii nchini (TTB) na Kampuni ya Heinken.

Aidha, amesema dhamira ya serikali kwa sasa ni kuendelea kutumia sekta za michezo na sanaa kuitangaza Tanzania na vivutio vyake duniani kwa kuwa zimebeba idadi kubwa ya rasilimali za Tanzania na kuongeza kuwa sekta hizo ndiyo nguvu shawishi ya serikali zinazowapa Watanzania wengi zaidi furaha na faraja.

"Nipende kumpongeza rais wetu kwa kazi kubwa sana na mikakati thabiti anayoifanya hivi sasa ya kuifungua Tanzania kupitia sanaa na michezo ambapo hivi karibuni ameandika historia kwa kushiriki moja kwa moja katika kuandaa Filamu ya Royal Tour," alisema Mchengerwa.

Alitaja baadhi ya mikakati mingine inayofanywa na Rais Samia kuwa ni kuifungua na kuitangaza Tanzania duniani kupitia sanaa na michezo kuwa ni pamoja na kuandaa mashindano makubwa barani Afrika ya tuzo za wasanii ili yafanyike hapa nchini yanayojulikana kama MTV Afrika Awards hapo mwakani, kuandaa mkutano wa marais wa mashirikisho ya soka utakaohudhuriwa na zaidi ya nchi 54 za Afrika jijini Arusha ambapo Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Gianni Infantino, anatarajiwa kuhudhuria pamoja na kufikiria kuandaa mashindano makubwa ya soka Afrika kuanza kufanyika hapa nchini.

Pia, ameongeza kuwa tayari serikali kupitia wizara anayoiongoza inakamilisha michoro kwa ajili ya kujenga kumbi za kisasa za michezo na maonyesho ya sanaa ambapo moja inatarajiwa kuchukua takriban watu 20,000 jijini Dar es Salaam na nyingine yenye uwezo wa kuchukua watu 15,000 jijini Dodoma.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Heinken nchini ambayo ndiyo mdhamini mkuu wa tukio hilo, Fatma Mnaro, amefafanua kuwa lengo la kuonyesha mubashara kilele cha UEFA 2022 hapa nchini kupitia DSTv ni kutaka kuwafanya wapenzi wa soka walione shindano hilo kwa ubora wa hali ya juu kama ambavyo watakavyoshuhudia wale ambao watahudhuria mtanange huo jijini Paris, Ufaransa.

Mnaro aliongeza kuwa pamoja na kurushwa mubashara kwenye Daraja la Tanzanite, kuna sehemu mbalimbali za majiji makubwa ambazo pia zitaonyesha ikiwa ni pamoja na The Cask jijini Mwanza, City Pub jijini Mbeya, Arusha na Capetown Fish Market, Samakisamaki na Triple 777 jijini Dar es Salaam.

## Simba yafunguka adhabu moto CAF

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wakishuka dimbani leo kuvaana na Azam FC, wameomba radhi kwa wanachama na mashabiki wake, baada ya kupatikana na kosa lililoitwa 'mila hatarishi' na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa kuwasha moto uwanjani kwenye mechi robo fainali ya mkondo wa pili ya Kombe la Shirikisho Afrika, uliochezwa Aprili 24, mwaka huu nchini Afrika Kusini.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema halikuwa tukio zuri, hivyo wanaomba radhi wanachama na mashabiki wa Simba waliojisikia unyonge au kuhisi kukwazika na jambo hilo, akiahidi halitojirudia tena.

Meneja Habari na Mawasiliano huyo alisema hayo jana, baada ya juzi jioni CAF kuipiga faini ya dola 10,000 sawa na Sh. milioni 23 za Tanzania kwa kile ilichokiita kufanya 'mila hatarishi' uwanjani kwa kuwasha moto katikati ya uwanja kwenye mechi dhidi ya Orlandi Pitares, iliyopigwa Uwanja wa Orlando, Afrika Kusini na Simba kutolewa kwa mikwaju 4-3 ya penalti, baada ya sare ya bao 1-0, kila timu ikishinda nyumbani.

**"Hiyo haina mjadala, adhabu imetoka CAF na iliyobaki ni kuitekeleza, ilitoka jana (juzi) jioni wakati ofisi zimefungwa, leo (jana), tunakwenda kujadili na kufanya maamuzi, kama ni kukata rufani au kulipa na baada ya hapo tutatoa maamuzi," alisema Ahmed.**

Kuelekea mechi ya leo dhidi ya Azam, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema mchezo huo utakuwa mzuri kutokana na wachezaji aliokuwa nao na aina ya uwanja ambao wanaenda kuutumia.

Alisema kikosi chake kipo tayari kuhakikisha kinapambana kutafuta pointi tatu ambazo zitawaweka katika mazingira mazuri ya kutetea ubingwa wao.

"Azam FC ina wachezaji wazuri, lakini hata benchi la ufundi lao liko vizuri tunaenda kupambana kuhakikisha tunapata matokeo chanya ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kutetea ubingwa wetu," alisema Pablo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >